

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao Cha Ishirini na Sita – Tarehe 13 Julai, 2005

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mheshimiwa Pius Msekwa) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA UJENZI:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Baraza la Taifa la Ujenzi kwa Mwaka 2002/2003
(The Annual Report and Accounts of the National Construction Council for the Year 2002/2003)

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Makandarasi kwa Mwaka 2003 *(The Annual Report and Accounts of the Contractors Registration Board for the Year 2003)*

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA (K. n. y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):

Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa Mwaka wa Fedha uliopita pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

**MHE. MOHAMED JUMA KHATIB (K. n. y. MSEMADI WA UPINZANI
BUNGENI WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA):**

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa Mwaka wa Fedha uliopita pamoja na Maoni yake kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 245

Barabara ya Songambele – Chitowe

MHE. ARIDI MWANACHE ULEDI aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Songambele – Maratani – Chitowe inahitaji matengenezo makubwa baada ya kuharibiwa na mvua kwa miaka kadhaa mfululizo, na kwa kuwa madaraja na makalvati mengi kwenye barabara hiyo ni mabovu hivyo kufanya barabara hiyo kuitika kwa taabu:-

(a) Je, Serikali itakarabati lini barabara hiyo?

(b) Je, madaraja na makalvati kwenye barabara hiyo yatatengenezwa lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI
ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aridi Mwanache Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Songambele – Chitowe yenyeye urefu wa Kilomita 40 ni barabara ya Halmashauri ya Masasi na ni kweli kwamba hajafanyiwa matengenezo makubwa kwa muda mrefu na hivyo kufanya iwe katika hali mbaya. Kutofanyiwa matengenezo kwa barabara hii ni kutokana na ufinyu wa Bajeti ukilinganisha na mahitaji halisi ya matengenezo ya barabara Wilayani Masasi.

Pamoja na kutokuwa na fedha za kutosha za kuifanya matengenezo makubwa barabara hii, Serikali katika mwaka 2001/2002 ilitoa fedha kiasi cha shilingi 7,650,000/- kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi na matengenezo ya kawaida. Fedha hizi zilitumika kuchonga barabara hii kwa kutumia *grader* kuchimba mifereji ya maji ya mvua, kufyeka sehemu ya barabara hii katika maeneo ya Ngupe na Maratani na kuweka changarawe baadhi ya sehemu korofi. Kutokana na matengenezo haya barabara hii iliweza kuitika vizuri kwa kipindi cha Mwaka 2002 na 2003.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2005/2006 Serikali imepanga kuifanyia matengenezo barabara hii kwa gharama ya shilingi 22,020,000/. Fedha hizi zitatumika kufanya matengenezo ya kawaida kilomita 30 na matengenezo ya muda maalum kilomita moja.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali imetenga shilingi 5,000,000 - kwa ajili ya kujenga makalvati mawili ya zege yenye kipenyo cha sentimita 90 kila moja. Fedha za matengenezo hayo zitatoka kwenye Mfuko wa Barabara.

Serikali kupitia Mfuko wa Barabara itaendelea kuzifanyia matengenezo barabara za Halmashauri zote nchini kulingana na vipaumbele vyao na pia upatikanaji wa fedha.

MHE. ARIDI MWANACHE ULEDI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Swali la kwanza: Kwa kuwa kazi zingine katika barabara hiyo ni ukataji wa nyasi na ufukiaji wa mashimo madogo madogo; na kwa kuwa kazi hizi zinaweza zikafanywa na wananchi wanaokaa kandokando ya barabara hiyo. Je, Serikali sasa itakuwa tayari kuwatumia wananchi hao ili kupunguza gharama ambazo zingetumika kwa kutumia *grader*?

Swali la pili, kwa kuwa kuna barabara iliyojengwa kwa ufadhili wa *TASAF* kuanzia Maratani kwenda Lipupu hivyo kuwahamasisha wananchi wa Lipupu, Mtawatawa, na Namijati ili kuweza kujijengea barabara; na kwa kuwa wananchi hao walikwishaanza kukata miti kwa ajili ya kupitisha barabara hiyo. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuwaunga mkono kwa kuwasaidia katika ujenzi wa barabara hiyo ili kuwapunguzia adha wananchi wa Namijati na Kata yote ya Mkonona wanapokwenda Masasi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS , TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza la kutumia wananchi kufanya kazi ndogo ndogo kama vile za ufyekaji na ufukiaji wa mashimo madogo madogo; tunachoweza kusema tu kama Serikali ni kwamba taratibu zilivyo hivi sasa ni utumiaji wa Makandarasi na wengine ni Makandarasi wadogo lakini tumekuwa muda wote tunashauri kwamba watumie wananchi wa maeneo hayo wakati wa matengenezo hayo ya barabara zinazopita katika maeneo hayo.

Lakini bado tunatoa wito na tumekuwa tukifanya hivi sehemu nyingi, si vizuri wananchi wakaa muda wote wanangojea mpaka Serikali ifukie mashimo madogo madogo au ufyekaji wa majani madogo madogo. Ni jukumu lao vile vile kufanya hizo kazi kwa sababu ni sehemu ya barabara ambazo zinawahudumia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, kwanza tunaomba tuishukuru sana *TASAF* imefanya kazi kubwa sana kitaifa, mchango wake ni wazi kabisa ni mkubwa kabisa. Lakini ninachoweza kumwomba Mheshimiwa Aridi M. Uledi ni kwamba katika kuongeza nguvu sasa kwa upande wa *TASAF* na kwa kuzingatia kwamba uwezo wa

Serikali si mkubwa sana, jambo hili basi liwasilishwe katika Halmashauri yetu pale waliingize katika mpango wetu wa kawaida wa mapendekezo ya barabara, Serikali itafikiria ione namna ya kuchangia nguvu za wananchi kwa sababu hatuna chanzo kingine isipokuwa kupitia Mfuko wa barabara. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa TAMISEMI naomba kuongeza katika majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI juu ya swali la Mheshimiwa Aridi M. Uledi kuhusu kuwatumia wananchi ambao wako kwenye Vijiji wakati barabara inatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, sera ambayo ipo ni kwamba wananchi hawa wanatakiwa wajiunge kwenye vikundi ili waombe kwa Mkandarasi ama kwa *Regional Manager* ama kwa *DED*, halafu pesa ziweze kuhesabiwa (*accounted for*) kwamba zimelipwa kwenye kikundi, lakini wakiwa watu binafsi wanakuwa tabu sana kupata kazi kwa Mkandarasi sababu inakuwa ni hiari yake mara nyingi. Kwa hiyo, wakiwa kwenye vikundi hata kina mama ni rahisi kusaidiwa sana. Hiyo ndiyo sera yenye we hasa kusaidia vikundi, wananchi kutaka kutengeneza barabara.

Na. 246

Barabara Kutoka Kijiji cha Bulima

MHE. PAUL N. MAKOLO aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya kutoka Kijiji cha Bulima Idukilo – Usule na Mwadui/Luhumbo ni muhimu kwa usafirishaji wa zao la Pamba na ni muhimu kwa usafiri wa wananchi wa sehemu hiyo; na kwa kuwa barabara hiyo sasa ni mbovu na inapitika kwa shida;

Je, Serikali ina mpango gani kusaidia ujenzi wa barabara hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul N. Makolo Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Bulima, Idukilo, Usule na Mwadui/Luhumbo alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge pamoja na kijiji cha Wishiteleja ni mionganoni mwa Vijiji vinavyounganishwa na barabara inayoanzia kijiji cha Mipa hadi kijiji cha Ngundangali. Barabara hii ni ya Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu na ina urefu wa kilomita 58. Ninakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ni muhimu kwa usafirishaji wa zao la Pamba na pia kwa usafiri wa wananchi wa sehemu hiyo.

Aidha, kwa kutambua umuhimu wa barabara hiyo, viongozi wa Wilaya akiwemo Mheshimiwa Mbunge waliwasilisha mapendekezo ya jinsi ya kutengeneza barabara hiyo. Ofisi yangu ilituma wataalam wa barabara kwenda Shinyanga ili kubainisha matengenezo yanayotakiwa pamoja na gharama zake. Kutowana na zoezi hili imebainika kwamba eneo kati ya Kijiji cha Mipa na Kijiji cha Wishiteleja kilomita 18 ni nzuri kiasi na inatengenezeka.

Aidha sehemu ya barabara ya kuanzia kijiji cha Wishiteleja kupitia Vijiji vya Bulima, Idukilo, Usule, Mwadui/Luhumbo hadi Ngundangali alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge yenye urefu wakilomita 40 ndiyo inahitaji matengenezo makubwa. Inakadiriwa kwamba matengenezo hayo yatagharimu kiasi cha shilingi 427, 203,000.00

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa Fedha 2005/2006 sehemu ya barabara ya Wishiteleja hadi Mipa imetengewa shilingi milioni 4.12 kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara (*Routine Maintenance*) ya kilomita 10, shilingi milioni 8 kwa ajili ya sehemu korofii (*Spot Improvement*) ya kilomita 6 na shilingi milioni 21.3 kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum (*Periodic Maintenance*) ya kilomita 2.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha cha shilingi 427,203,000/- zinazohitajika kwa ajili ya matengenezo ya sehemu ya barabara ya Wishiteleja – Ngundangali ni kikubwa kuweza kupatikana kutoka kweye Mfuko wa barabara, hata Halmashauri ya Wilaya yenye. Hata hivyo kwa kutambua umuhimu wa barabara za vijijini kwa wananchi katika kupambana na umaskini, Ofisi yangu imeshirikiana na Shirika la Maendeleo la Norway (*NORAD*) kubuni Mpango wa Taifa wa matengenezo ya barabara Vijijini Ndani ya mradi huu jumla ya kilomita 3,250 zimepangwa kukarabatiwa hadi kiwango cha changarawe.

Mradi huu utaanza katika mwaka wa Fedha 2005/2006, hivyo namshauri sana Mheshimiwa Mbunge pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kuipa kipaumbele barabara hii wakati wakuwasilisha mapendekezo ya ukarabati wa barabara katika Wilaya yao.

MHE. ESHA H. STIMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi hii ili niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri yenye matumaini ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wanawake wa eneo hilo ambalo barabara mpaka dakika hii inachelewa kutengenezwa hupata tabu sana wanapokwenda *Clinic* au Zahanati kwa ajili ya kujifungua.

Je, Serikali inasema nini kuhusu tatizo la wanawake wa maeneo hayo ambao ndiyo wakulima wakuu wa Pamba na ndiyo wanaleta kipato katika nchi hii ili wawze kuwa salama na watoto wao wanapokwenda kujifungua na *Clinic*, naomba jibu. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, matatizo ya barabara yako nchi nzima na kwa kweli

kama Serikali wote tuna masikitiko kwa tabu nyingi ambazo wananchi wanazipata kwa ujumla wakiwemo akina mama ambao ndiyo sehemu kubwa ya wafanyakazi. Lakini naomba nirudie kauli ile ile kwamba juhudzi za Serikali nadhani ni dhahiri, na wote mnaona jitihada zinazofanyika na ndiyo maana nimesema katika suala hili la Kishapu, ufumbuzi peke yake tulionao kwa sasa ambao tunauona ni dhahiri ni kupitia huo Mpango wa matengenezo ya Barabara Vijijini. Naomba nikuhakikishie Mama Stima, kama mtawasilisha jambo hili mapema, sisi tutajitahidi kushinikiza Ofisi iweze kuhakikisha kwamba wanatenga kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya eneo hilo.

Na. 247

Unit za Umeme Majumbani

MHE. THOMAS NGawaiya aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika Mkutano wa Bajeti wa Mwaka 2004/2005 tulikubaliana kuwa *Units* za Umeme zitakazopatiwa ruzuku kwa watumiaji wa majumbani ni kuanzia *Unit 1* hadi 100:-

- (a) Je, ni lini tena Serikali iliwahi kuleta hoja hiyo Bungeni na kuamuliwa vinginevyo?
- (b) Je, jambo lolote likishaamuliwa Bungeni linaweza kubadilishwa na chombo chochote zaidi ya Bunge lenyewe?
- (c) Je, ni nani aliyebadilisha na kuamua kuwa *Unit* zenye ruzuku majumbani ni *Unit 50* badala ya 100 ilivyoamuliwa Bungeni na kibali cha kufanya hivyo amekipata wapi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, masuala ya kupanga bei za Umeme ni ya Kisheria ambapo *Board* ya *TANESCO* inaruhusiwa kurekebisha bei kwa asilimia 5 bila kuomba kibali Serikalini. Endapo ongezeko linalohitajika ni zaidi ya asilimia 5, Bodi ya *TANESCO* inatakiwa kumwomba Waziri wa Nishati na Madini ambaye naye kwa kushirikiana na Mheshimiwa Waziri wa fedha ambao kwa pamoja wanayo mamlaka ya kurekebisha bei kwa asilimia 10 na hivyo kufanya marekebisho ya bei za umeme yasiyozidi asilimia 15 bila kufika katika Baraza la Mawaziri kuomba kibali.

Mheshimiwa Spika, endapo ongezeko ni zaidi ya asilimia 15, badiliko hili ni lazima lipitishwe na Baraza la Mawaziri. Mabadiliko au Marekebishi yote yaliyofanywa huko nyuma yalizingatia sheria. Chini ya kifungu cha 83 cha sheria ya umeme yaani

Electricity Ordinance Cap 131, Waziri anaye husika na masuala ya Nishati ana mamlaka ya kutunga sheria ndogo ndogo yaani *Regulations* kwa ajili ya kuendesha shughuli za uzalishaji na usambazaji wa umeme.

Mnamo Januari, 2004 yalifanyika marekebisheso ya bei za umeme kwa asilimia 4.2. Mnamo Julai, 2004 mapitio mengine ya asilimia 4.8 yalifanyika.

Mheshimiwa Spika, maamuzi yoyote yanayochukuliwa katika kufanya marekebisheso ya bei za umeme kutoka *Unit 100* na kwenda *Unit 50* kwa watu wa kipato cha chini yalizingatia sababu za kiuchumi. Bunge likishatunga sheria halihusiki na kufanya marekebisheso ya bei za umeme. Kimsingi mabadiliko ya bei za umeme hufanywa kwa mujibu wa sheria na hayakiuki mgawanyo wa madaraka ya kikatiba kati ya Bunge na Serikali.

MHE. THOMAS NGAWAIYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri, amesema kama mabadiliko ni asilimia 5 tu basi haina haja ya kufika Bungeni, lakini kutoka *Unit 100* mpaka kuja kwenye 50 ni zaidi ya asilimia 5. Je, Waziri anasemajie kwa hilo?

La pili, kwa kuwa umeme ni chombo muhimu sana cha kupunguza umaskini; na kwa kuwa sasa tuna gesi ambayo imezaliwa nchini mwetu na tulikuwa tunatumia hela nyingi sana kwa *Matalban* yaliyokuwa Ubungo. Je, sasa hivi Serikali inasema kwa kupata hiyo gesi ni asilimia ngapi imepungua kwa ile gharama ya kwanza ya mafuta? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, wakati najibu swali la msingi sikuzungumzia masuala ya mabadiliko ya bei kwa asilimia 5 na 10 kufikishwa Bungeni.

Nilizungumzia mtiririko wa maamuzi ndani ya Serikali kuanzia *Board* ya *TANESCO* hadi kwa Waziri wa Nishati na Madini akishirikiana na Waziri wa Fedha hadi kwenye Baraza la Mawaziri. Nikazungumzia pia umuhimu uliotokea wa kubadilisha kutokana na sababu hasa za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano zile *Unit 50*, kutokana na hali mbaya ya hewa, ya ukame; iliilazimu *TANESCO* ipate mapato zaidi ili iongeze pamoja na fedha za ruzuku ambazo zilikuwa zinatolewa na Serikali ambazo jana nilizitaja zilikuwa karibu shilingi bilioni 40 na nyingine za misaada kama shilingi bilioni 50 ili kuweza kukabiliana na hali ya ukame na kuzalisha umeme.

Kutokana na hiyo ilibidi kupunguza hizi kwa asilimia 50 kwa maana ya *Unit 50* ili kuweza kupata shilingi bilioni moja kwa mwezi. Isinge kuwa hivyo tungelazimika kuongeza bei za umeme kwa asilimia 5 kwa watumiaji wote pamoja na hao wa kiwango

cha chini ili kuweza kukabili matumizi ya uzalishaji wa umeme kwa sababu *TANESCO*, katika shilingi bilioni 22 ambazo inakusanya sasa, shilingi bilioni 20 zinakwenda kwenda kwenye matumizi. Katika hizo bilioni 20, bilioni 13 zinatumika katika kununua umeme *IPTL* na *SONGAS*.

Nataka niseme kwamba Serikali hii inajali sana wananchi wake wa kipato cha chini na ndiyo maana bado ikaweka hizo *Unit 50* ziendelee kubaki na kiwango hiki ni bora zaidi kuliko kilichoko katika nchi jirani. Kuhusu matumizi ya gesi, labda nitoe mfano tu kwamba katika kutumia mafuta, tulikuwa tunatumia miezi ya hivi karibuni, shilingi bilioni 90. 40 zilikuwa zinatoka kwenye ruzuku ya Serikali na hizi nyingine 50. Sasa hivi ruzuku hiyo haitolewi na *TANESCO* ina uwezo wa kuendelea kununua umeme kutoka *SONGAS* na kutoka *IPTL*, na hiyo ndiyo faida inayopatikana kutokana na matumizi ya gesi kwamba gharama zimepungua na hata uwezo wa *TANESCO* umeongezeka wa kuweza kuendesha nchi.

Na. 248

Mikoa Isiyokuwa na Umeme

MHE. ALHAJ AHAMADI HASSAN MPEME aliuliza:-

Kwa kuwa mpango wa kupeleka umeme wa uhakika Wilayani na Vijijini unakwenda vizuri; na kwa kuwa pamoja na kazi hiyo nzuri lakini bado ipo Mikoa ambayo hata Makao yake Makuu hayajapatiwa Umeme wa uhakika, jambo ambalo linazorotesha Maendeleo ya Mikoa hiyo;

Je, Serikali haioni kwamba upo umuhimu mkubwa sasa wa kupeleka umeme katika Mikoa hiyo iliyobaki ili kunusuru Maendeleo yake yanayoendelea kushuka kutokana na kukosekana kwa huduma hiyo muhimu ya umeme?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alhaj Ahamadi Hassan Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa mpango wa kupeleka umeme wa uhakika kwenye Miji Mikuu yote ya Mikoa. Mfano kwa sasa, Makao Makuu ya Mikoa ambayo haina umeme wa gridi na ambayo mingine haina umeme wa uhakika ni Mji wa Songea, Kigoma, Mtwara na Lindi ingawa katika Songea na Mtwara tayari *TANESCO* imenunua injini mpya za kuzalisha umeme ili kuongeza hali ya umeme katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Upembuzi Yakinifu wa kupeleka umeme wa gridi ya Taifa wa msongo wa kilovoti 132 kutoka Makambako hadi Songea unaanza mwezi Agosti 2005. Vile vile Serikali inaendelea kufanya majadiliano na Kampuni ya *Artumas* ya Canada kwa ajili ya uzalishaji umeme kwa kutumia gesi ya *Mnazi Bay* kwa ajili ya Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mkoa wa Kigoma, Serikali ikishirikiana na *TANESCO* imekuwa ikichambua njia mbali mbali za kupeleka umeme wa uhakika huko Kigoma. Pamekuwa na mapendekezo yafuatayo:-

Kuendeleza umeme wa gridi ya Taifa kutoka Urambo hadi Kigoma yaani Urambo - Kaliua hadi Kigoma, pindi mradi wa Umeme wa Urambo – Kaliua utakapokamilika mwaka huu, kuendeleza Gridi ya Taifa kutoka Kahama kupitia Kibondo, Kasulu hadi Kigoma, Ujenzi wa *main hydro* kwenye Mto Malagarasi, Kupata umeme kutoka nchi jirani ya Burundi, kupata umeme kutoka maporomoko ya Mto Rusumo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali tayari imeomba msaada kutoka Serikali ya Sweden kugharimia Upembuzi Yakinifu kwa Mradi wa kupeleka umeme Kigoma kutoka Urambo – Kaliua. Taratibu za kumpata mtaalam yaani *Consultant* atakaye fanya kazi hii zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Utafiti umefanywa chini ya Mradi wa ushirikiano wa nchi za Bonde la Mto Nile (*Nile Basin Initiative*). Utafiti huo umependekeza kuipatia Mikoa ya Magharibi ya Tanzania umeme kutoka Mto Rusumo. Makubaliano yamefikiwa kati ya Tanzania, Rwanda na Burundi juu ya uendelezaji wa Mradi wa kuzalisha umeme kwenye Mto Rusumo. Taratibu za kupata wafadhili wa mradi huo zinaendeshwa kwa pamoja na nchi hizo. (*Makofit*)

MHE. ALHAJ AHAMADI HASSAN MPEME: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini naomba pia niulize swalii dogo la nyongeza. Kwa kuwa makusudio makubwa ya Serikali kupeleka umeme hadi vijijini ni kuharakisha maendeleo ya wananchi na kwa kuwa wananchi wanaokusudiwa kuharakishiwa maendeleo yao pia na hali zao ni maskini kwa mfano vijijini hali zao si nzuri.

Lakini kwa kuwashawishi kwamba wautumie umeme huo na kutokana na gharama kubwa sana ya umeme, watashindwa kutumia. Je, Serikali haioni kwamba ni vizuri kuharakisha utaratibu wa kupunguza gharama za matumizi ya umeme ili kuwawezesha wananchi wa Tanzania ambao hali zao si nzuri kuweza kutumia umeme? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, napenda niseme tu kwa ufupi kwamba ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba umeme unapatikana kwa bei nafuu na kwa kweli ndiyo sera yenye.

Mheshimiwa Spika, lakini kama ambavyo tunesema mara nyingi hapa Bungeni, kufikiwa kwa lengo hili kunategemea sana na ubadilishaji wa mfumo mzima wa uzalishaji wa umeme nchini na ndiyo maana Serikali imekuwa ikichukua hatua mbali

mbali ya kuhakikisha kwamba mfumo wa uzalishaji unabadilishwa na kugundua vyanzo vingine kama vya gesi na kadhalika..

Kuhusu umeme vijijini, Serikali inatambua uwezo mdogo wa wananchi vijijini na ndiyo maana basi katika kuweka mpango maalum wa kufikisha umeme vijijini pameanzishwa Taasisi hii ya kuwa Wakala wa umeme vijijini na Mfuko Maalum utakaoanzishwa umeme wa vijijini na katika mpango mzima huo ambao jana nimeusema wa kupeleka umeme vijijini unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Ni mpango ambao utatilia maanani uwezo mdogo wa wananchi kupata umeme kwa njia hizi za kawaida kwa bei hizi za kawaida ambazo zipo hivi sasa.

MHE. BERNADINE R. NDABOINE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa huu upembuzi yakinifu umechukua miaka 20 sasa, kwa sababu Mheshimiwa Rais Ali Hassan Mwinyi alipokuwa anagombea alitoa ahadi kwamba Kasulu watapata umeme, baadaye Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa naye alisema watapata umeme na Mheshimiwa Marehemu Teddy Magayane aliwahi kupata hata *Generator*. Kwa nini basi wakati hatujapata umeme wa gridi, Kasulu na Kibondo wasipewe umeme wa *Generator?* (*Makofi*)

SPIKA: Hilo ni jipyä lakini kama una majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri endelea.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kadhia ya ukosefu wa umeme katika Miji ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge na kwa hakika pale Kasulu pana ka-kimradi kidogo cha kuzalisha umeme ambao Serikali imekuwa ikishirikiana na wafadhilli katika kuhakikisha kwamba kinaanzishwa. Lakini nataka niseme tu kwamba suala la kupeleka *Generator*, uzalishaji wa umeme kwa kutumia mafuta ni ghali sana.

Nadhani tufanye subira kidogo katika kasi hii ambayo Serikali inaenda nayo ya kuhakikisha kwamba Mkoa wa Kigoma unaunganishwa ama na gridi ya Taifa - na kwa kweli siyo gridi ya Taifa tu lakini hata ile njia ambayo nimeizungumzia kupata umeme kuititia nchi jirani au maporomoko ya Mto Rusumo. Yote haya yatawezesha kuboresha hali ya umeme katika Mkoa wa Kigoma kwa hiyo tufanye subira kidogo.

Na. 249

Athari za Vita vya Msumbiji kwa Mkao wa Mtwara

MHE. LYDIA T. BOMA aliuliza: -

Kwa kuwa, vita vya Msumbiji vilichangia kwa kiwango kikubwa kudumaza maendeleo ya Mkoa wa Mtwara kwa sababu yalikuwa ni maeneo ya wapiganaji kwa muda mrefu hadi Uhuru wa nchi hiyo ulipopatikana:-

- (a) Je, Serikali inatambua vipi mchango wa Mkoa huo hasa baada ya vita kumalizika kwa kuzingatia kuwa wakati wa vita Mikoa mingine ya Tanzania ilikuwa inaendeleza maendeleo yake wakati Mkoa wa Mtwara ukishiriki mapambano?
- (b) Je, Askari mashujaa wa Tanzania waliokufa wakati wa vita, wakiwemo wale waliozikwa Kitaya, familia zao zinatunzwaje?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K. n. y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Lydia Boma; Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kwanza napenda kutoa maelezo yafuatayo: -

Tanzania iliamua kutoa mchango wake wa hali na mali katika ukombozi wa Bara la Afrika kutokana na hekima, busara na upeo mkubwa wa Muasisi na Baba wa Taifa Marehemu Mwalimu Julius K. Nyerere. Mwalimu aliutangazia ulimwengu kwamba Uhuru wa Tanzania haukuwa na maana iwapo ndugu zetu wa Msumbiji, majirani zetu na nchi nyingine za Bara la Afrika bado zipo katika makucha ya ukoloni na bado wanaendelea kukandamizwa, kutumikishwa na kudhulumiwa na ubepari wa kikoloni.

Watanzania katika Mikoa yote nchini waliunga mkono vita vya Ukombozi wa Bara la Afrika. Tanzania inajivunia mchango wake katika Ukombozi wa Bara la Afrika hasa ukombozi wa ndugu zao wa Msumbiji dhidi ya ukoloni mkongwe wa Wareno uliowakandamiza na kuwatumikisha kwa miaka 500.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kawaida ya mapambano ya aina yoyote, athari haziepukiki. Athari walizopata ndugu zetu wa Mikoa ya Kusini ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Mtwara ni pamoja na Wananchi kupoteza maisha yao kutokana na mabomu, milipuko na mashambulizi ya ndege za kivita, uchumi uliathirika, huduma za jamii nazo ziliathirika hivyo kuathiri maendeleo ya Mikoa ya Kusini pamoja na Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Lydia Boma; Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na inathamini mchango mkubwa wa Wananchi wa Mikoa ya Kusini ukiwemo Mkoa wa Mtwara katika ukombozi wa Wananchi wa Msumbiji dhidi ya ukoloni mkongwe wa Wareno uliowakandamiza na kuwatumikisha kwa miaka 500. Kwa kutambua mchango wa Wananchi wa Mikoa wa Mtwara, mnamo Septemba, 2004 Serikali iliamua kurejesha mabaki ya miili ya mashujaa wetu waliopoteza maisha yao nchini Msumbiji na Zimbabwe na kuzikwa upya hapa

nchini kwa heshima zote za Kitaifa katika uwanja mpya wa kisasa wa Mashujaa ulioko Naliendele Mtwara, sherehe zilizoongozwa na Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua athari zilizotokana na vita vya Ukombozi wa Msumbiji Mkoani Mtwara, Serikali baada ya vita ilichukua na inaendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuinua uchumi kwa kujenga upya miundombinu na kuboresha huduma za jamii hii yote ni katika kuboresha na kuendeleza Mkoa wa Mtwara.

Hatua hizo ni pamoja na uanzishwaji wa miradi mbalimbali kama vile ujenzi wa barabara, miradi ya maji, mradi wa umeme kule *Mnazi Bay*, miradi ya simu, elimu, elimu ya ufundi – kuna chuo cha *VETA* pale kikubwa kuliko vyuo vyote nchini, miradi ya afya, uwanja wa ndege, mradi wa ujenzi wa daraja la Umoja litakalounganisha Tanzania na Msumbiji katika Mto Ruvuma.

Vile vile, kuna mpango kabambe wa kuinua uchumi wa nchi nne jirani unaojulikana kama *Mtwara Development Corridor* na uimarishaji wa Bandari ya Mtwara.

(b) Mheshimiwa Spika, katika maeneo yote ya mapambano ambayo JWTZ walishiriki, Askari wetu walipoteza maisha wakitekeleza majukumu yao ya kazi. Katika kuwashumudia jamaa na wahanga wetu hawa malipo yafuatayo hutolewa na Serikali yetu kwa kuzingatia sheria na kanuni za Jeshi la Ulinzi: -

(i) Malipo ya Kiinua Mgongo (*Death Gratuity*) ambayo hutolewa kwa familia ya Mwanajeshi ye yote anapofariki.

(ii) Malipo ya Wategemezi (*Survivor's Benefits*). Ni malipo ya miaka mitatu ambayo hutolewa kwa Mwanajeshi aliyetumikia Jeshi kwa miaka 20 na kuendelea. Malipo hayo hulipwa kwa mke/mume wa Marehemu na watoto chini ya miaka 21.

(iii) Malipo ya Rambirambi (*Interim Allowance*). Malipo haya hutolewa kwa familia ya Marehemu ikiwa ni mishahara ya miezi sita ya Marehemu, hulipwa kwa mkupuo mmoja.

MHE. LYDIA T. BOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza. Lakini kabla sijauliza maswali hayo, napenda niipongeze Serikali kwa jinsi walivyoamua kuchukua miili ya wale Wanajeshi waliofariki vitani na kuja kuzika Mtwara Kitaifa. (*Makofi*)

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mikoa ya Kusini, hususan Mtwara Serikali ilisema kwamba Wafanyakazi wa Mikoa hiyo watapata motisha na Wanajeshi wanatii amri ya Serikali, hawawezi kukataa. Je, ni msaada/motisha gani wanapewa kama vile gari au pikipiki?

(b)Mheshimiwa Spika, kutokana na Wanajeshi wengine kukaa nje ya makambi kwa kukosa makazi. Je, Serikali inajua hiyo? Kama inajua, inachukua hatua gani kuhakikisha Wanajeshi wetu wanapata nyumba nzuri na wanaishi vizuri? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K. n. y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA): Mheshimiwa Spika, kwanza zile pongezi alizozitoa Mheshimiwa Mbunge ninazipokea kwa niaba ya Serikali kwamba pale sasa itakuwa ni historia ya kudumu. Vizazi na vizazi vitatambua Mtwara kwamba ni sehemu ambayo ilishiriki katika mapambano ya kuikomboa Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalilake la kwanza la motisha maalum kwa Wanajeshi wanaopelekwa Mikoa ya Kusini, Mwanajeshi unapoingia katika kazi ya Jeshi unakula kiapo cha kuilinda Tanzania mahali popote na wakati wowote. Kwa hiyo, hakuna tofauti ya motisha kwa Mikoa. Mwanajeshi yuko tayari kufanya kazi popote, Mkoa wowote na kwa maslahi ambayo yameainishwa katika sheria kwa wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wanajeshi wanaoishi nje ya makambi, ni kweli kwamba sasa hivi upo mpango maalum wa kujenga nyumba kwa Wanajeshi ili Wanajeshi wote wa Jeshi la Ulinzi wakae *barracks* na katika Hotuba yetu ya Bajeti ambayo tutaisoma wiki ijayo, tutafafanua kwa vizuri zaidi kwa mwaka huu wa fedha tutajenga nyumba katika makambi yapi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, subiri Hotuba yetu ya Bajeti itafafanua kuhusu mpango mzima wa kujenga nyumba za Askari.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Swalil la msingi linahusu Mapambano ya Ukombozi Kusini mwa Afrika na kwa kuwa katika mapambano hayo Askari wa Msumbiji kupitia Chama chao cha Frelimo, Zimbabwe, Askari wa ANC, Askari wa Angola na Namibia waliishi Kongwa na kupata mafunzo Kongwa kwa ajili ya kuwaandaa kwenda kukomboa nchi zao. Je, Serikali ina mipango gani ya kuhifadhi kumbukumbu hii muhimu ya ukombozi wa Afrika kwa ajili ya vizazi vijavyo pale Kongwa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K. n. y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kongwa kilikuwa ni kituo muhimu sana cha mafunzo kwa wapigania uhuru wa nchi mbalimbali alizozitaja na ni nia ya Serikali kudumisha historia ile ili vizazi vijavyo wajue umuhimu wa Kongwa na hata hivi karibuni Rais wa Namibia alitoa kauli kwamba inafaa tushirikiane Tanzania na nchi za jirani tuone ni namna gani ya kuweka kumbukumbu ya kudumu pale Kongwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, taratibu zinaendelea kwa Tanzania tukishirikiana na nchi zilizokaa pale Kongwa ili tuone ni namna gani nzuri ya kuweka kumbukumbu na historia ya kudumu. (*Makofi*)

Mauaji ya Mwanafunzi Adili Oronu

MHE. AGGREY D. J. MWANRI aliuliza: -

Kwa kuwa mwezi Machi, 2005 mwanafunzi Adili Uronu wa Shule ya Sekondari Siha inayomilikiwa na Kanisa la KKKT Dayosisi ya Kaskazini, alipigwa risasi na kufariki muda mfupi tu baadaye katika Hospitali ya Kibong'oto na kwa kuwa, katika kikao cha wadau wakuu wakiwemo wazazi wa marehemu na Mbunge wa Jimbo la Siha walikaa kinyume kabisa na kitendo cha mauaji ya mwanafunzi huyo na kuitaka Dola ichukue hatua madhubuti za kisheria dhidi ya wale wote waliohusika na mauaji hayo: -

- (a) Je, ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya wahalifu hao waliofanya mauaji ya mwanafunzi huyo?
- (b) Je, kuna mikakati gani ya kuharakisha ufuatiliaji wa suala hilo ili haki itendeke kwani haki inayocheleweshwa ni sawa na haki iliyokataliwa yaani *Justice delayed is justice denied?*
- (c) Kwa kuwa taarifa ya Mkuu wa Shule hiyo inaonyesha kuwa mauaji hayo yalitokana na mgogoro wa maji kati ya shule na wakorofii wachache toka kijiji jirani. Je, ni hatua gani zimechukuliwa za kuhakikisha kuwa shule hiyo inapatiwa maji ya kudumu ili kuondokana na hatari kama hiyo iliyotokea?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mnano tarehe 27/2/2005 majira ya saa 5.00 asubuhi huko katika Shule ya Sekondari ya Siha iliyopo katika Kijiji cha Samaki Maini, Jimbo la Siha, Wilaya ya Hai, mwanafunzi Adili Abuu Uronu (miaka 17) wa kidato cha pili, alipigwa risasi kifuanii na shingoni na kufariki. Baada ya msako mkali, Polisi walifanikiwa kumkamata mtuhumiwa mmoja anayeitwa Raphael Mbojo Lukumay pamoja na bunduki aina ya *shotgun* namba 21799 ikiwa na risasi tatu. Aidha, ganda la risasi iliyomuua Marehemu pia lilipatikana.

(b) Mheshimiwa Spika, mtuhumiwa katika kesi hiyo, yaani Bwana Raphael Lukumay, tayari amefikishwa mahakamani, Mahakama ya Wilaya ya Hai kwa kosa la mauaji na kesi inaendelea. Aidha, Polisi wanaendelea na uchunguzi iwapo wapo wahusika wengine katika tukio hilo.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa chanzo cha mauaji haya ni mgogoro wa kugombea maji kati ya shule na Wanakijiji toka kijiji cha jirani. Baada ya tukio hilo la mauaji, Viongozi wa Serikali Wilaya ya Hai akiwemo Mheshimiwa Mbunge Aggrey

Mwanri, Viongozi wa Kijiji pamoja na Viongozi wa Shule, walifanya kikao cha pamoja kujadili tatizo la maji lililosababisha uhasama ndani ya jamii na wakafikia muafaka juu ya namna bora ya kumaliza tatizo hilo.

Aidha, Mamlaka ya Maji Wilaya ya Hai ndiyo inasimamia utekelezaji wa muafaka huo na hivi sasa maji yanapatikana shulenii bila matatizo yoyote. Hali ya amani imerejea na Wanafunzi wanaendelea na masomo kama kawaida.

Kwa niaba ya Serikali, napenda kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa jinsi alivyotumia diplomasia ya hali ya juu kupusha uhasama na mapigano ya kulipiza kisasi baina ya pande mbili zilizokuwa zinagombania maji. (*Makofi*)

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa pongezi ambazo amezitoa kwangu kwa kazi hiyo ambayo tumekuwa tunaendelea kuifanya.

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza kwamba, kwa vile muda unaendelea kupita, suala hilo lilitokea mwezi Machi na sasa tunakwenda huu ni mwezi wa Saba na inaonekana kwamba kwa kweli jambo hili haliedi kwa haraka kama ilivyokuwa imekusudiwa na ilivyokuwa imetarajiwaa na Wananchi wenyewe. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuharakisha kesi hii ili haki iweze kutendeka?

(b) Kwa kuwa ni kweli kwamba tatizo lililotokea pale na lililosababisha hali hii linatokana na tatizo la maji na kwa kuwa sasa hivi Serikali imepeleka mradi wa Levish katika eneo hili la Siha Sekondari. Je, Serikali inatoa maagizo gani kwa mkoa wa Kilimanjaro na hususan Wilaya ya Hai ya kuharakisha mradi wa Levish ambao unaendeshwa na *KfW* ili maji ya kudumu yaweze kupatikana katika eneo hili? (*Makofi*)

(a) Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ile kesi kuwa imechelewa, nataku tu kusema kwamba, Polisi waliishafanya kazi yao ya kufanya upelelezi, kumkamata yule aliyefanya mauaji na bunduki yake na risasi zake na Polisi wameishafikisha kesi hii mahakamani.

Sasa pale kinachoendelea ni taratibu za Mahakama kwa sababu Mahakama nayo ina taratibu zake na hapo inapokuwa ni kesi ya mauaji taratibu zinakuwa ndefu kuliko kesi hizi za kawaida. Kwa hiyo, nafikiri tuiachie Mahakama ili mkondo wa sheria uchukue nafasi yake.

(b) Kuhusu swali la maji naona Waziri ameishasimama kule atakujibu vizuri zaidi. (*Kicheko/Makofi*)

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, napenda kuongeza majibu mazuri sana ya Naibu Waziri kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwanri, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali ya Ujerumanî na Kanisa la KKKT kwa kusaidia maji katika Mkoa wa Kilimanjaro. (*Makofi*)

Pili, nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Mwanri (Mbunge) kwa sababu anafuatilia sana masuala ya maji kwa ajili ya Wilaya yake. Napenda kumhakikishia kwamba tutafanya kila linalowezekana ili maji hayo yapatikane mapema kadri itakanavyowezekana. (*Makofi*)

Na. 251

Makao Makuu ya Polisi – Lushoto

MHE. CHARLES H. KAGONJI aliuliza: -

Kwa kuwa Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya Mjini Lushoto ni ya kihistoria kama ilivyo kwa Wilaya yenyewe ya Lushoto na kwa kuwa wakati fulani katika historia ya utawala wa kikoloni Polisi Lushoto ilitambulika kama Makao Makuu ya Polisi nchini, yaani *Tanganyika Police Force Headquarters* na kwa vile Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya hiyo yanositisha kama siyo kutisha: -

(a) Je, Serikali inaifahamu hali mbaya na ya kutisha ya kizamani ya majengo ya Makao hayo Makuu ya Polisi Mjini Lushoto?

(b) Je, hivi yuko Kiongozi yejote wa ngazi ya Wizara kama vile Waziri/Naibu Waziri au Katibu Mkuu ambaye amewahi kutembelea Lushoto na kuona hali hiyo ya majengo?

(c) Kama yupo aliywahi kufika, Serikali kupitia Wizara hii inawaambia nini Wananchi wa Lushoto, Mkoa wa Tanga na Watanzania wote kupitia mpango kabambe na wa haraka sana wa kuondoa kabisa hali hiyo mbaya na kusikitisha?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa majengo ya kituo cha Polisi Wilaya ya Lushoto kama yalivyo majengo ya Vituo vya Polisi vya Wilaya nyingine nchini ni ya kurithi kutoka kwa wakoloni na kwa kuwa majengo haya hayajafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu, sasa ni machakavu na hayana hadhi ya kuwa Vituo vya Polisi vya Wilaya.

Serikali inalifahamu tatizo hili kwani Viongozi Wakuu wa ngazi ya Wizara yangu hufanya ziara mikoani kukagua shughuli za Wizara pamoja na Vituo vya Polisi. Kwa mfano, Naibu Waziri alitembelea Kituo cha Polisi cha Lushoto tarehe 14 Machi, 2005 na aliona hali halisi ya uchakavu wa kituo hicho.

Kwa kufahamu hali mbaya ya Vituo vya Polisi vya Wilaya mbalimbali hapa nchini, Serikali kwa dhati imeazimia kujenga kwa awamu majengo ya kisasa katika vituo vyote vya Polisi vya Wilaya. Wilaya ambazo ofisi za Polisi tayari zimejengwa ni 58 kati ya Wilaya 118.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2005/2006 zimetengwa fedha za ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Wilaya Sh.280,000,000/= na katika kipindi hicho ujenzi utafanyika katika Wilaya za Morogoro, Namtumbo, Mpanda na Hanang.

Juhudi za kujenga Vituo vya Polisi katika Wilaya nyingine kwa awamu zinaendelea hadi Wilaya zote zitakapokuwa na majengo ya vituo vya kisasa ikiwa ni pamoja na Lushoto.

MHE. CHARLES KAGONJI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu hayo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kufahamu kwamba, katika huo mpango wa ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Wilaya, Wilaya ya Lushoto inaangukia muda gani?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba, ujenzi unakwenda kwa awamu kwa sababu fedha za kujenga vituo vyote vya Wilaya kwa mara moja hazipo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba tutafika lini Lushoto, kwa kweli inategemea na maandalizi ya wao wenyewe. Mfano, nilipotembelea kituo hicho mapema mwaka huu nilikuta hata kiwanja tu bado hakijapatikana! Bahati nzuri tulikuwa na Viongozi wa Halmashauri, tulikuwa na *DC*, tukaagizana kwamba kwa sababu pale tulipo sasa hivi ni pafinyu ni lazima tutafute eneo pana la kujenga kituo chenyewe na *barracks* ya nyumba za Askari.

Kwa hiyo, Lushoto hata tu ule uwanja wa kutupatia tujenge hiso nyumba bado. Niliwaambia kwamba wakamilishe hivyo na wakiweza hata kuanza tu *harambee* ya kufyatua matofali vile vile ni moja ya kigezo ambacho kitafanya wapate mradi huo kwa haraka zaidi. Kwa hiyo, wafanye maandalizi, tuko tayari kufika Lushoto.

Ununuzi wa Kivuko

MHE. JACOB D. SHIBILITI aliuliza: -

Kwa kuwa juhudi nzuri za Serikali za kujenga Barabara Kuu za Mikoa zimeonyesha mafanikio mazuri na kumeongeza Pato la Taifa kwa kupitisha magari mengi kwenda nchi jirani za Rwanda, Burundi na Congo (*DRC*) na kwa kuwa ongezeko la magari katika maeneo hayo kumesababisha msongamano wa magari kushindwa kuvushwa kwa wakati katika kivuko cha Kigongo upande wa Misungwi na Busisi upande wa Sengerema na kwa kuwa Serikali katika Bajeti yake ya mwaka 2004/2005 ilitenga Shilingi bilioni 2 kwa ajili ya ununuzi wa kivuko kipyta: -

- (a) Je, kivuko kipyta kitapatikana lini na imefikia hatua gani kwa sasa?
- (b) Je, Serikali imetenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya kukifanya matengenezo kivuko kilichopo kwa sasa ili kiweze kufanya kazi kwa ufanisi wakati tukisubiri kivuko kipyta?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Shibiliti; Mbunge wa Misungwi, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza tunamshukuru sana Mheshimiwa Dalali Shibiliti kwa jinsi anavyofuatalia vivuko hasa vya Kanda ya Ziwa na hasa hiki cha Kigongo. Yeye anafuatalia sana na anajitahidi kweli kweli. Ameshawahi kuja wizarani mara nyingi sana kufuatalia kivuko hiki.

Mheshimiwa Spika, Kivuko cha Kigongo - Busisi kipo kwenye barabara ya Usagara - Sengerema – Geita hadi Biharamulo. Kivuko hicho kinahudumia magari mengi yanayopeleka mafuta kwenye migodi na nchi za jirani. Ni kutokana na ongezeko hilo la magari, Serikali katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2004/2005 imeanza kutenga fedha kiasi cha Shilingi bilioni 2.0 kwa ajili ya kununulia kivuko kipyta ili kuboresha huduma ya kivuko katika eneo hilo.

Baada ya kivuko hiki kuwasili, utaratibu wa kutenganisha abiria na mizigo ya mafuta wakati wa kuvuka utafanyika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Shibiliti, kama ifuatavyo: -

- (a) Mheshimiwa Spika, Mkataba wa ununuzi wa kivuko kipyta ulitiwa sahihi tarehe 10/05/2005 kati ya Wizara na Mkandarasi anayeitwa *Sinnautic International* wa Uhlanzi. Kivuko kitapatikana baada ya miezi 14 kutoka tarehe ya kusaini Mkataba.

(b) Kivuko cha Sengerema ni kati ya vivuko vitano vitakavyofanyiwa matengenezo kwenye mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia na Zabuni ya Mkataba huo itatangazwa hivi karibuni. Kivuko hicho baada ya matengenezo kitatumika kwenye kivuko cha Kigongo – Busisi kusaidiana na kivuko kipyä ili kuboresha huduma ya kivuko.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swalı moja la nyongeza.

Kwa kuwa sasa kivuko hicho kinafanya kazi kwa muda mfupi na hakitoshelezi mahitaji pale. Je, mnawenza kuongeza muda kwamba kivuko hicho kifanye kazi kwa muda wa saa 24 kusudi magari yasiwe yanalala pale na kupata usumbufu mkubwa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kivuko hiki tunakipunguzia muda wa kufanya kazi ili kiweze kuchukua muda wa kutosha kuhudumia Wananchi mpaka kivuko kipyä kitakapofika na wakati huo baada ya kufika kivuko kipyä hiki kitakuwa kwenye matengenezo. Kwa hiyo, si vizuri kukitumia muda wa saa 24 halafu kikaja kikaharibika kabisa tukashindwa kupata kivuko.

Na. 253

Mserereko wa Shilingi

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (K. n. y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED) aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikieleza mafanikio ya kuzuia mserereko wa Shilingi ya Tanzania: -

- (a) Je, ni mambo gani yanayosababisha kuserereka au kutoserereka kwa Shilingi?
- (b) Je, kwa nini katika kipindi cha miezi sita Shilingi imekuwa ikiporomoka ikilinganishwa na Dola ya Kimarekani na Paundi ya Uingereza:

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi yanayoweza kusababisha kuserereka au kutoserereka kwa Shilingi ambayo ni pamoa na:-

(i) Urari wa biashara ya nje ya nchi (*balance of trade*), ambapo nakisi kubwa katika urari wa biashara husababisha mahitaji makubwa ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza bidhaa na huduma nyingine kutoka nje ya nchi. Hivyo, thamani ya Shilingi

hushuka kwa sababu mahitaji ya fedha za kigeni huwa makubwa kuliko mapato yatokanayo na mauzo nchi za nje.

(ii) Mfumuko wa bei (*inflation*), ambapo pamoja na mambo mengine husababishwa na ongezeko kubwa la ujazi wa fedha kuliko uzalishaji wa bidhaa na huduma mbalimbali katika nchi. Hivyo, thamani ya fedha hupungua iwapo mfumuko huo ni mkubwa kuliko mfumuko wa bei katika nchi tunazofanya nazo biashara. Kwa mantiki hiyo, thamani ya Shilingi inaweza kuimarika endapo kutakuwa na mfumuko wa bei ulio sawa ama mdogo kulinganisha na nchi tunazofanya nazo biashara.

(iii) Tofauti za misimu (*seasonal factors*) katika upatikanaji wa fedha za kigeni kutokana na biashara ya nje. Kwa mfano, Shilingi huonyesha kutoserereka katika kipindi cha kati ya Julai na Desemba kwa kuwa ni kipindi cha mavuno na utalii kuwa kwenye kilele. Aidha, huonyesha kuserereka katika kipindi cha maandalizi ya kilimo, kati ya Januari na Juni.

(iv) Mabadiliko ya hali ya hewa. Kwa kuwa kilimo chetu hutegemea kwa kiasi kikubwa hali ya hewa, hali ya ukame au mvua kubwa kupita kiasi husababisha upungufu wa fedha za kigeni zinazotokana na mauzo ya mazao nje ya nchi na huongeza mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza chakula kutoka nje ya nchi.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika kipindi cha miezi sita iliyopita, Shilingi ya Tanzania imekuwa ikiporomoka kufuatana na taratibu za nguvu za soko la fedha. Thamani ya Shilingi ilishuka kutoka wastani wa Sh.1,048.1 kwa Dola ya Marekani mwezi Desemba 2004 hadi kufikia Sh.1,129.2 mwezi Juni, 2005. Aidha, kati ya kipindi cha Desemba 2004 na Juni 2005, thamani ya Shilingi ilishuka kwa asilimia 7.7 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kilichoishia Juni 2004 ambapo thamani ya Shilingi ilishuka kwa asilimia 4.8.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ni ongezeko kubwa la bei ya mafuta katika soko la dunia. Hali hii imesababisha kuongezeka kwa gharama za kuagiza mafuta, hivyo, kuongeza mahitaji ya fedha za kigeni ambayo yalisababisha kuperomoko kwa Shilingi.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza katika maelezo yake hapa kuwa, moja katika *factor* inayosababisha Shilingi kuanguka ni mahitaji ya fedha za kigeni. Kwa sasa nchi yetu ina soko la fedha za kigeni kiasi kwamba mara nyingine zinashindwa hata kununuliwa. Je, kwa kuwa Serikali inasema kila mara kuwa uchumi unakua na kwa kuwa hizo fedha za kigeni bado zipo, haoni kuwa hiyo sababu ya fedha za kigeni haichukui nafasi hapa katika kuiangusha Shilingi yetu?

(b) Pia, ameeleza katika miezi ambayo inafanya Shilingi isianguke ni kuanzia Julai mpaka Desemba hasa kwa sababu ya mambo ya utalii na mambo ya kilimo. Je, anasemaje kuhusu nafasi ya Shilingi hiyo hivi sasa kwa sababu tayari tuko kwenye mwezi Julai, 2005? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika, soko la fedha za kigeni liko huru kama ambavyo tumeamua kwamba Serikali haitajiingiza tena katika upangaji wa bei ikiwemo na bei ya kubadilisha fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu ambayo ndiyo ina dhamana ya kuangalia kwamba Sekta ya Fedha imetulia, ina majukumu ya kuangalia na kufanya *interventions* na kuingilia kati inapoona kwamba kuna mserereko mkubwa. Kwa mfano, kwa kutumia *Open Market Operations* Benki Kuu huwa inaangalia, ikiona kuna matatizo kwenye soko inakwenda kama mdau kwa maana ya ku-*inject* ama ku-*withdraw excess*, fedha zilizozidi katika soko la dunia. Hayo ni mambo mengine ambayo yanafanywa katika utaratibu wa *free hand* siyo kwamba inapanga bei.

Kwa hiyo, sababu nilizositaja zinafanya kazi katika soko huru na ukikuta kuna matatizo makubwa basi yamesababishwa na sababu ambazo ni nje ya uwezo wa soko (*external factors*).

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kwamba kwa nini sasa hivi ni Julai, 2005 na hali bado ni mbaya, nilisema ni Julai mpaka Desemba na Julai, 2005 ndiyo inaanza, kwa hiyo tutegeme krama kadri tunavyoolekea Desemba mambo yataendelea kuwa mazuri.

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kufahamu tu kama juhudzi za Serikali kufuatana na uchumi wetu unavyokua, sasa pamba inaongezeka kuzalishwa, maua yanaongezeka kuzalishwa kwa hiyo tunafanya biashara na nchi za nje.

Kwa msimamo wa Serikali wa sasa wa kusimamia mfumuko wa bei, tutumie njia ipi ili tuzidi kuongeza uzalishaji huu katika nchi ili tuweze kuuza nje zaidi kwa kuona *exchange rate* tutaichukulia hatua kama Serikali?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Kazi kwa kazi nzuri anayofanya Jimboni kwake. (*Kicheko/Makofi*)

Pili, kuhusu suala la kwamba tufanyeje ili kuongeza uzalishaji, Serikali ya Awamu ya Tatu imejitahidi kushusha mfumko wa bei kutoka asilimia 27.5 mwaka 1995 mpaka 4.5 hivi sasa. Kwa hiyo, hii ni *centive* katika uzalishaji na uwekezaji pia. Uzalishaji wa mazao ya kilimo umeweza kuongezeka kama tutakavyosoma kwenye jedwali lililotolewa jana kwenye hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini kwamba madini yanayouzwa nje ni asilimia zaidi ya 50.

Lakini pia mazao mengine kama korosho, pamba yameongezeka. Kwa hiyo, ili tuweze kuongeza uzalishaji Serikali inaendelea kuweka mazingira muafaka katika uwezekaji, wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa kutoka nje. Lakini uzalishaji mkubwa katika kilimo utatokana na Shirika mpya ya Ardhi ambayo itahamasisha wazalishaji na wakulima kuingia katika kilimo cha kibashara. Hali hiyo, ndio itasababisha kuongezeka zaidi kwa mazao ya kilimo na hatimaye uuzaji wa bidhaa nchi za nje.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha, hakuna matangazo ya vikao vya Kamati kwa leo niliyofetewa. Kwa hiyo tunaendelea na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006

Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa Bungeni na Mheshimiwa Athuman Janguo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa likubali kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, kwa Mwaka wa Fedha wa 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kuishukuru kwa dhati Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Athuman Janguo, Mbunge wa Kisarawe, iliyochambua kwa makini malengo na makusudio ya Bajeti ya Wizara hii na hatimaye kuafiki na kuipitisha kifungu kwa kifungu. Mchango uliotolewa na Kamati kwa ujumla pamoja na ushauri wa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo umesaidia sana kuiboresha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii pia kuwakumbuka na kuwaombea dua wenzetu ambao wamelitumikia Taifa kuitia Bunge hili ambao wametangulia mbele ya haki. Wabunge hao ni Hayati Margaret Bwana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, kuitia CCM, Hayati Theodos James Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, Hayati Frank Michael Mussati aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki, Hayati Balozi Ahmed Hassan Diria aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo na Hayati Abubakar Towegale Kiwanga aliyekuwa Mbunge wa Kilombero. Nawapa pole familia zao na wananchi wa Majimbo yao na namwomba Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema peponi roho zao - Amin.

Mheshimiwa Spika, huu ni mkutano wa ishirini na wa mwisho wa Bunge hili la Serikali ya Awamu ya Tatu. Naamini kuwa wananchi watakulaliana nami kwamba kumekuwa na mafanikio makubwa ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni yaliyopatikana wakati wa Serikali ya Awamu ya Tatu. Wengine wetu tunarudi tena kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba, Sheria, Kanuni na Taratibu kuomba ridhaa yao ya kurudi katika Bunge la Serikali ya Awamu ya Nne. Nina matumaini makubwa kuwa wananchi watatambua mafanikio hayo yaliyotokana na Serikali ya Awamu ya Tatu na kuturudisha tena katika ukumbi huu katika awamu ijayo. (*Makofî*)

Aidha, Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Rais Benjamin William Mkapa kwa uongozi wake mzuri na madhubuti ambao umeleta mafanikio haya makubwa. Aidha, nampongeza Dr. Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mzuri.

Pia, nampongeza Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Mbunge wa Jimbo la Hanang na Waziri Mkuu, kwa kusimamia vizuri na umakini mkubwa shughuli za Serikali Bungeni. Wote hao ninawatachia kila la kheri baada ya uongozi wao mzuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile, kulipongeza Bunge lako Tukufu chini ya Uongozi wako, kwa mchango mkubwa ambao umewezesha Wizara na Serikali kwa ujumla kupatikana kwa mafanikio makubwa kwa kipindi chote cha uhai wake. Aidha, napenda kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza kwa makini na uhodari mkubwa Bunge lako Tukufu. Pia Nawapongeza Mheshimiwa Naibu Spika, na Wenyeviti wote wa Bunge. Wote nawatachia kila la heri na fanaka. (*Makofî*)

Pia naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Jimbo la Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuteuliwa kwake kuwa mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM na Dr. Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mgombea Mwenza. Vile vile, ninampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa kuwa Mgombea wa Urais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, katika Uchaguzi Mkuu ujao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako Tukufu linavyoolewa, majukumu ya Wizara yangu ni kusimamia utoaji haki, udumishaji wa haki za binadamu na kuishauri Serikali katika masuala ya Sheria kwa lengo la kudumisha amani, utulivu na kuweka mazingira mazuri ya maendeleo, hasa wakati huu ambapo nchi yetu imeingia katika mfumo wa uchumi wa soko huria na utandawazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imejizatiti kutekeleza majukumu yaliyoainishwa kwa kuongozwa na Dira ya Haki kwa Wote na kwa Wakati. Lengo la Dira hii ni kuleta maendeleo ya Haki kwa Jamii, Usawa na Utawala wa Sheria kutokana na kuwepo kwa huduma bora za kisheria zitakazopatikana kwa wote na kwa muda muafaka. Wizara yangu inao Mkakati wa Kujenga Mfumo wa Sheria ambao utakidhi mahitaji mapya ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na maendeleo ya kisayansi ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, Wizara imepata mafanikio ambayo yameiwezesha na kusaidia Tanzania kupata mafanikio makubwa ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Mafanikio hayo ambayo yameelezwa katika hotuba za Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha yametokana na utekelezaji mzuri wa Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria katika Serikali ya Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu, umuhimu wa Sekta ya Sheria katika maendeleo ya nchi uliendelea kutiliwa mkazo na kupewa kipaumbele ili kudumisha na kuendeleza Utawala Bora. Katika kipindi hicho Serikali ilijitahidi kuongeza Bajeti ya Sekta ya Sheria mwaka hadi mwaka ili kutekeleza mipango mbalimbali kwa lengo la kuboresha Wizara na asasi zake. Mathalani, Bajeti ya Wizara imekuwa ikiongezeka kila mwaka kutoka Shs.4.4 bilioni Mwaka 1995/96 hadi Shs.49.98 bilioni Mwaka 2005/06. Kwa ujumla, hali hii imewezeza kupatikana mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria (*Legal Sector Reform Programme*).

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu kwa upande wa Wizara ni pamoja na yafuatayo:-

- (a) Kuweka misingi imara katika utoaji haki na kuimarisha taaluma na nidhamu ya utoaji Haki kwa wananchi;
- (b) Kuweka misingi imara ya Sheria mbalimbali zinazosimamia Haki za Binadamu na Sheria zinazoweka mazingira mazuri ya Maendeleo ya Uchumi tulivu katika nchi;
- (c) Kuweka misingi imara ya haki za binadamu na utawala bora kwa kuanzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;
- (d) Kuboresha na kuendeleza utafiti wa Sheria mbalimbali za nchi na kuziboresha ili ziende na wakati na mabadiliko ya kiuchumi ulimwenguni;
- (e) Kupatikana na kuimarisha miundo mbinu ya utoaji haki;
- (f) Kuweka misingi mizuri ya kuendelea na utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria; na
- (g) Kuboresha mazingira ya kazi na kujenga uwezo na ujuzi wa utendaji kazi wa watumishi kwa kuwapatia mafunzo muhimu katika stadi zao.

Mheshimiwa Spika, nguzo kuu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii ni Utawala Bora na Utawala wa Sheria. Katika kipindi cha miaka kumi ya Serikali ya Awamu ya

Tatu, Wizara imetekeleza kwa dhati uwekaji wa misingi imara ya Utawala Bora na Utawala wa Sheria. Uwekaji na utekelezaji wa misingi hii ulizingatia Dira ya Wizara ambayo ni Haki kwa Wote na kwa Wakati. Misingi hii imara imesaidia kuongezeka kwa uzalishaji mali na kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imechukua hatua kadhaa ili kuboresha utendaji katika asasi zinazosimamia haki. Hatua hizo zimeongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza ni uimarishaji wa mfumo wa utoaji Haki, Mfumo wa Mahakama: -

(i) Kuanzishwa utaratibu wa Usuluhihi Mbadala ndani ya Mahakama *Alternative Dispute Resolution (ADR)* unaorahisisha na kuharakisha usuluhihi wa mashauri ya madai katika Mahakama Kuu na Mahakama za Wilaya;

(ii) Utaratibu wa kila Jaji na Hakimu kujipangia ratiba ya usikilizaji wa mashauri (*individual calendar*) tangu mwanzo ili waweze kuyafatilia na kuyakamilisha;

(iii) Kuimariswa Kamati za Kusukuma Mashauri (*Case flow Management Committees*) kuanzia ngazi ya Taifa hadi Wilaya ili ziweze kuchangia katika mkakati wa kupunguza mlundikano wa mashauri;

(iv) Mahakama maalumu za Biashara na Ardhi zilianzishwa mwaka 1999 na 2002. Mahakama hizi ni Vitengo vya Mahakama Kuu vilivyoanzishwa kwa lengo la kuongeza kasi ya kusikiliza na kutatta migogoro ya biashara na ardhi ili kuharakisha utoaji haki na kupunguza msongamano wa kesi katika Mahakama zetu nchini;

(v) Kanda ya Mahakama Kuu ya Sumbawanga imeanzishwa na hivyo kuongeza Kanda za Mahakama Kuu kutoka kumi na moja (11) hadi kumi na mbili (12);

(vi) Kuimariswa kwa ukaguzi wa Mahakama (*Court Supervision*);

Mfumo wa Huduma za Kisheria:-

(i) Ofisi tatu za Kanda za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali zimefunguliwa Dar es Salaam, Bukoba na Sumbawanga na kufanya jumla ya Ofisi za Kanda kuwa kumi na mbili (12)

(ii) Kuimariswa kwa ukaguzi wa Ofisi za Kanda za Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na

(iii) Kuimariswa kwa uwezo wa Tume ya Kurekebisha Sheria ili iweze kukidhi mahitaji ya mabadiliko ya Sheria nchini.

Haki za Binadamu:-

- (i) Kuanzishwa kwa Idara ya Mambo ya Katiba na Haki za Binadamu mwaka 1998 ambayo inashughulikia masuala ya Katiba na Haki za Binadamu;
- (ii) Kuanzishwa kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora mwaka 2002 ambayo inashughulikia masuala ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Uendeshaji Mashtaka:-

- (i) Maandalizi ya kutenganisha jukumu la kuendesha mashtaka na lile la upelelezi yamekwisha anza na yanatarajiwu kukamilika ifikapo Juni, 2006.

(b) Uimarishaji wa Miundombinu ya Utoaji Haki:-

- (i) Mahakama ya Rufani ilipata jengo ambalo linafanyiwa ukarabati kwa ajili ya shughuli za Kimahakama na ofisi;
- (ii) Mahakama iliongeza majengo manne (4) kwa ajili ya shughuli za Mahakama Kuu katika miji ya Mbeya, Iringa, Moshi, Sumbawanga na Songea;
- (iii) Majengo ya Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Kinondoni (Kivukoni) na Sumbawanga yamejengwa;
- (iv) Majengo mapya ya Mahakama ya Wilaya katika Wilaya za Kongwa, Ludewa na Mbarali yamejengwa;
- (v) Majengo ya Mahakama katika Wilaya za Mbinga, Maswa, Lindi na Mwanza yamefanyiwa ukarabati;
- (vi) Majengo mapya 13 ya Mahakama za Mwanzo yamejengwa na majengo 302 ya Mahakama za Mwanzo kufanyiwa ukarabati. Aidha, jumla ya majengo ya Mahakama za Mwanzo 51 yanaendelea kujengwa na kukarabatiwa katika Wilaya 43 za Tanzania Bara; (*Makofî*)
- (vii) Jengo la Mahakama ya Biashara ambalo likiwa jengo la Mahakama ya Hakimu Mkazi, Kivukoni lifanyiwa ukarabati na kuwekewa vitendea kazi vya kisasa na ujenzi wa jengo jipya la tawi la Mahakama ya Biashara mjini Arusha ulikamilika na kuanza kutumika;
- (viii) Ujenzi wa Mahakama ya Watoto ya Kisutu umefanyika na maandalizi ya ujenzi wa Mahakama za Watoto Mbeya na Mtwara unaendelea;
- (ix) Majengo mawili yamenunuliwa kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Kanda za Songea na Mtwara;

- (x) Jengo jipya la Nyumba ya Haki (*Haki House*) linalotumiwa na Tume ya Kurekebisha Sheria na Tume ya Haki za Binadamu limejengwa;
- (xi) Aidha, Mahakama mbali mbali zimepatiwa vitendea kazi kila hali ya kifedha iliporuhusu;
- (xii) *Tanzania Law Reports* za kila mwaka kuanzia 1983 hadi 1997 zilichapishwa na kusambazwa.

Mafunzo ya Wafanyakazi

- Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kwa ajili ya kutoa mafunzo ya Stashahada ya Sheria na Cheti cha Sheria kilianzishwa mwaka 2000. Serikali imeendelea kukiimarisha Chuo hicho kwa kuongeza wanafunzi wanaosomea Stashahada na Vyeti vya Sheria kutoka 12 mwaka 2001/2002 hadi kufikia 198 mwaka 2004/2005.
- Maandalizi ya mpango wa kuanzisha *Law School* kwa ajili ya mafunzo ya vitendo kwa wahitimu wa Sheria yanaendela.
- Mpango Endelevu wa Mafunzo Kazini umebuniwa kwa ajili ya asasi za kisheria ambao unalenga kuboresha ufanisi wa Watendaji na uwezo wa Vyuo vya Mafunzo ya Sheria kutoa elimu endelevu.
- Mafunzo ya vitendo yahusuyo taaluma mbalimbali za uwakili, haki za binadamu, uongozi, menejimenti na mipango yameendelea kutolewa.

Mheshimiwa Spika, sera za maendeleo ya kiuchumi na kijamii hutekelezeka panapokuwapo misingi imara ya sheria zinazoweka mazingira mazuri ya utekelezaji wake. Serikali ya Awamu ya Tatu kuitia Wizara yangu imekuwa ikiimarisha shughuli za utafiti wa Sheria, usimamiaji wa uandishi, kutafsiri na kufanya mabadiliko ya Sheria na kanuni mbalimbali za nchi. Katika kipindi cha miaka kumi, Wizara, kwa eneo hili imetekeleza yafuatayo:-

- (a) Sheria arobaini (40) zilizotajwa katika Tume ya Jaji Nyalali kuwa zinazuia ukuaji wa demokrasia zilifanyiwa utafiti ambapo kati ya hizo sheria ishirini na tisa (29) zilihusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Sheria kumi na moja (11) zilihusu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
- (b) Sheria 29 za Serikali ya Muungano zilizofanyiwa mapitio na tayari zimefanyiwa marekebisco;
- (c) Sheria zinazogusa makundi maalum kama Wanawake, Watoto na wasiojiweza zilifanyiwa utafiti;

- (d) Sheria za mienendo ya Utoaji Haki – *Flow of Justice*, Sheria za Polisi na Magereza zilifanyiwa utafiti ili ziweze kukidhi matakwa ya kulinda haki za binadamu;
- (e) Ripoti ya utafiti wa Sheria ya Kuzuia Rushwa imewasilishwa Serikalini mapema mwaka huu;
- (f) Sheria kuu 11 zilitafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitafsiriwa katika lugha ya Kiingereza ili kuwawezesha Wadau mbalimbali kuzitumia;
- (g) Sheria 599 zilichujwa na kufanyiwa urekebu na kubakiwa na jumla ya Sheria 418 ambazo zimetolewa katika Toleo la Sheria za Tanzania la mwaka 2002 (*Revised Laws of Tanzania*), linalojumuisha Sheria zote zilizokuwepo na zilizotungwa hadi kufikia Julai 2002 lilichapishwa, kusambazwa na kuanza kutumika mwaka 2005;
- (h) Jumla ya Miswada ya Sheria 211 ilipitishwa na Bunge na sheria ndogo 5,578 zilichapishwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu, kuitia Wizara yangu iliendelea kuimarisha huduma za utoaji ushauri wa Kisheria kwa Serikali na Taasisi zake katika nyanja za madai na Sheria za Kimataifa. Aidha, Wizara iliendelea kuiwakilisha Serikali na Taasisi zake katika mashauri yaliyopo Mahakamani na kwenye Mabaraza. Pia, iliendelea kuishauri Serikali kisheria katika masuala yote yanayohusu mikataba ya ndani na Kimataifa na ushirikiano wa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa udhamini, mirathi, usajili wa ndoa na talaka, masuala ya watoto wa kuasili, usajili wa vizazi na vifo, ufilisi na usimamizi wa mali zisizo na mwenyewe uliendelea kuimarishwa na kutiliwa mkazo katika Serikali ya Awamu ya Tatu. Katika eneo hili, mambo yafuatayo yalitekelezwa:

- (a) Huduma za usajili wa ndoa, vizazi na vifo zimesambazwa katika Wilaya 120 za Tanzania Bara;
- (b) Usajili wa ndoa uliimariswa na jumla ya ndoa 816,832 zilisajiliwa nchi nzima chini ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971;
- (c) Vyama vya hiari 1,516 vimesajili Wadhamini chini ya Sheria ya Usajili wa Wadhamini (*Trustees Incorporation Ordinance*) Sura ya 375 ya Sheria za nchi;
- (d) Jumla ya watoto wa kuasili (*adoption*) thelathini (30) wamesajiliwa chini ya Sheria ya Kuasili (*Adoption Ordinance*), Sura ya 335;
- (e) Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za kuifanya Ofisi hii kuwa Wakala wa Serikal ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma chini ya Mpango wa Kuboresha Huduma kwa Umma.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na jitihada kubwa za Serikali ya Awamu ya Tatu katika kuboresha mazingira ya kazi na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wake kwa nia ya kuboresha utendaji na kuongeza tija. Katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, Wizara ilichukua hatua mbalimbali za kuboresha mazingira ya kazi ikiwa ni pamoja na kuboresha miundo ya Wizara na Mahakama na kutoa mafunzo kwa watumishi wake kama ifuatavyo:

- (a) Idara mbili za Mambo ya Katiba na Haki za Binadamu na Sera, Mipango na Habari ziliundwa ili kuimarisha na kuboresha huduma za katiba, haki za binadamu na kusimamia na kuratibu mipango ya Wizara;
- (b) Muundo wa Mahakama umefanyiwa uchambuzi wa kutenganisha shughuli za Mahakama na za Kiutawala ili kuleta ufanisi katika utoaji wa haki;

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu katika Sekta ya Sheria, Sera ya Taifa ya Sekta ya Sheria imeanza kuandaliwa na inatarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2007. Sera ya Taifa ya Sekta ya Sheria inaandaliwa katika msingi wa mtazamo wa hali halisi yaani *evidence-based policy* ili iweze kukidhi matakwa ya Sekta katika kuboresha utoaji wa huduma za kisheria hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2004/2005, Sekta ya Sheria imeainisha maeneo ya kipaumbele katika kuongeza kasi ya upatikanaji wa haki pamoja na kukidhi mabadiliko ya kisera na mageuzi ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia. Hili lilitokana na Ripoti ya Mwaka 1997 ya *Legal Task Force* iliyotoa mapendekezo ya namna bora ya kuboresha utoaji haki na kuwasilishwa Serikalini. Mapendekezo haya yalikuwa ni mengi na mapana na utekelezaji wake ulikuwa wa gharama kubwa kwa wakati ule. Ripoti hii imekuwa ni changamoto kwa Wizara yangu na Sekta nzima ya Sheria, hasa katika kuangalia tuanzie wapi na twende wapi ili tufanikishe Dira yetu ya “Haki kwa Wote na kwa Wakati. Tumetumia kila uwezo na fursa tulipopata katika kuweka misingi imara ya kuleta mabadiliko katika Sekta ya Sheria kwa:-

- (a) Kuzindua Mkakati wa muda wa Kati wa 2000 - 2005 wa Programmu Kuboresha Sekta ya Sheria mwaka 1999. Mkakati huu umesaidia kuainisha maeneo ya kipaumbele katika kuboresha kasi ya utoaji haki, kuweka misingi ya uratibu baina ya asasi za kisheria ikiwa ni pamoja na uratibu baina ya wadau wa kimaendeleo, *Development Partners*; uainishaji wa majukumu ya Asasi mbalimbali na mabadiliko ya miundo na kisheria, na uboreshaji wa miundo mbinu kama nilivyoeleza awali. Yote haya yalitekelezwa chini ya Miradi iliyobuniwa chini ya Mkakati huu. Miradi hiyo ni *FILMUP* uliokoma Disemba 1998, *Establishment of Commission of Human Rights* uliokoma Oktoba, 2004 na umeongezwa muda hadi Aprili, 2006, *Capacity Building* uliokoma January 2004, *Quick Start* uliokoma Disemba 2004, *Law Reform Commission Capacity Building* ambao utekelezaji wake utakoma mwaka huu na maandalizi ya Mradi wa Tanzania, *Accountability, Transparency and Integrity Project* yatakayokamilika ifikapo Septemba 2005; na

(ii) Uzinduzi wa Mkakati wa Kati 2005/2006-2007/2008 wa Mpango wa Programu Kuboresha Sekta ya Sheria, Machi 2005 ambao unashirikisha asasi nyingi zaidi, unatoa fursa ya uwajibikaji kwa kila asasi tekelezi. Aidha, Mkakati unaweka mazingira mazuri ya utekelezaji wa pamoja.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2004/2005. Baada ya maelezo kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu, napenda sasa nirejee katika utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2004/2005. Kwa ujumla, utekelezaji wa mpango wa mwaka 2004/2005 ulikuwa wa mafanikio. Wizara yangu ilitekeleza shughuli ambazo zililenga kutekeleza malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), ushauri na maelekezo mbali mbali yaliyotolewa wakati wa kikao cha Bajeti cha Bunge kwa mwaka 2004/2005. Hali ya utekelezaji kwa maeneo muhimu ilikuwa kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na suala la upunguzaji wa mlundikano wa kesi Mahakamani, Mahakama ya Rufani ilifanya vikao 14 ikilinganishwa na Vikao 12 vilivyopangwa kufanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2004/2005. Pia, Mahakama Kuu ilifanya Vikao 97 ikilinganishwa na vikao 88 vilivyopangwa kufanyika. Vikao vya kawaide vya Mahakama viliendelea kufanyika kwa siku tano kwa wiki kwenye ngazi zote za Mahakama. Hali hii imewezekana kufuatia usambazaji mzuri wa vitendea kazi kwenye Mahakama zote.

Mheshimiwa Spika, Kamati za Kusukuma Mashauri kwenye ngazi za Kanda za Mahakama Kuu, Mkoa na Wilaya, vikihusisha watendaji kutoka Mahakama, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Polisi na Magereza zilifanya jumla ya vikao vinne (4) kwa kila Kamati.

Aidha, Kamati ya Taifa ya Kusukuma Mashauri (*Case Flow Management Committee*) ilifanya Vikao viwili (2) vya Kitaifa. Vile vile, Mahakama ya Tanzania imeendelea kuimarisha mfumo wa utoaji haki kwa kuanzisha Kanda mpya ya kumi na mbili (12) ya Mahakama Kuu, Sumbawanga. Sambamba na uanzishwaji huo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu nayo imefungua Ofisi ya Kanda mpya ya Sumbawanga. Uanzishwaji wa Kanda hii unalenga kuongeza kasi ya kupunguza mlundikano wa kesi kwenye Kanda ya Mbeya na kusogeza huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2004/05, Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara kilipokea mashauri mapya 142 na katika kipindi hicho mashauri 162 yalitolewa maamuzi ikiwa ni pamoja na yale ambayo yalikuwa hayajatolewa maamuzi. Aidha, kuna mashauri 91 yanayosubiri kusikilizwa. Vile vile, Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi kilisikiliza na kuamua migogoro 170 kati ya migogoro 535 iliyofunguliwa katika Mahakama hiyo katika Mwaka wa Fedha wa 2004/05.

Mheshimiwa Spika, katika kuinua ufanisi wa utendaji wa usimamiaji na utoaji wa haki, Wizara yangu ilifanya yafuatayo:

- (a) Majaji 5 wa Mahakama Kuu waliteuliwa na Rais na kufanya idadi ya Majaji wa Mahakama Kuu kuwa 38;
- (b) Mahakimu Wakazi 45 walijiriwa na kufanya idadi ya Mahakimu Wakazi kuwa 203;
- (c) Mawakili wa Serikali 6 walipandishwa vyeo na kuwa Mawakili Wakuu wa Serikali na kufanya idadi ya Mawakili Wakuu wa Serikali kuwa 31;
- (d) Mawakili wa Serikali 28 wameajiriwa na kufanya jumla yao kuwa 120;
- (e) Mawakili wapya 35 walisajiliwa na hivyo kufanya idadi ya Mawakili nchi nzima kuwa 758;
- (f) Mawakili wa Serikali 12 walipatiwa mafunzo kwa kiwango cha Shahada ya Uzamili na Mawakili wa Serikali 80 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi;
- (g) Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 31 walijiriwa na kufanya idadi kuwa 699;
- (h) Tume ya Haki za Binadamu na Utwala Bora imeajiri Wakurugenzi 4 kati ya sita (6) wanaohitajika, watumishi 20 wa ngazi ya utawala na Wachunguzi 25;
- (i) Tume ya Haki za Binadamu na Utwala Bora imewapeleka Makamishna na watumishi wengine wa Tume kwenye mafunzo kuhusu Haki za Binadamu na Utwala Bora;
- (j) Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 68 wamepatiwa udhamini wa mafunzo ya kozi ya Stashahada ya Sheria na Makarani wa Mahakama 20 wamedhaminiwa katika Cheti cha Sheria kwenye Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto;
- (k) Kutungwa na kupitishwa na Bunge Sheria ya Utumishi wa Mahakama (*Judicial Service Act, 2005*) ili kusimamia masuala ya utumishi katika Mahakama ikiwa ni pamoja na nidhamu na ajira yamelenga kuboresha huduma za utoaji haki;
- (l) Kutungwa na kupitishwa na Bunge Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (*The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Act, 2005*)

ambayo ina ainisha utaratibu wa kutoa huduma za kisheria ina lengo la kuboresha na kuimarisha masuala ya utendaji wa Mawakili wa Serikali na Wanasheria wengine wanaotoa huduma hiyo katika Wizara na Taasisi za Serikali; na

- (m) Watumishi wengine 239 wa kada nyingine katika Wizara na Taasisi zake wamepatiwa udhamini katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililieleza Bunge lako Tukufu juu ya hatua zinazochukuliwa na Wizara katika kuimarisha na kuboresha huduma za uendeshaji mashtaka nchini hadi ngazi za Wilaya ambapo shughuli za upelelezi wa Jinai na Uendeshaji Mashtaka utatenganishwa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika Mwaka wa Fedha wa 2004/2005, Wizara iliendesha upembuzi yakinifu na kuchagua mikoa mitano (5) itakayoanza kufanyiwa majoribio ya awali (*pilot scheme*). Mikoa hiyo ni: Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, Utafiti na Uandishi wa Sheria, Wizara yangu iliendelea na shughuli za Utafiti na Uandishi wa Sheria. Jumla ya miswada 17 ilipitishwa na Bunge na Sheria ndogo ndogo 475 zilihakikiwa na kuchapishwa katika gazeti la Serikali.

Kati ya Sheria hizo, Sheria 3 zilitafsiriwa katika Kiswahili nazo ni Sheria ya Haki za Binadamu; Sheria ya Misitu na Sheria ya Dhamana na Mikopo ya Serikali. Wizara inaendelea kutafsiri Sheria 2 ambazo ni; Sheria ya Mazingira na Sheria ya Ardhi. Aidha, Bunge liliweza kuridhia Mikataba na Itifaki 32 ya Kimataifa katika kipindi cha 2004/05.

Mheshimiwa Spika, katika mchakato wa kuboresha uandishi wa Miswada, Sheria na nyaraka mbalimbali katika viwango vinavyohitajika, Wizara yangu imenunua mtambo maalum ambao utarahisisha na kuboresha uchapaji. Mtambo huo maalum unaunganisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mpiga Chapa wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2004/05, shughuli za utafiti ziliendelea ambapo Tume ya Kurekebisha Sheria ilikamilisha utafiti wa Sheria katika maeneo 5 na ambayo taarifa husika zimekwisha wasilishwa katika Mkutano huu ni:-

- (a) Sheria zinazohusu Polisi na Magereza;
- (b) Sheria Kuhusu Rushwa;
- (c) Mtiririko wa haki za mtuhumiwa tangu anakamatwa hadi kuhukumiwa (*Flow of Justice*);
- (d) Uwezekano wa kuwa na Sheria ya kumwezesha Waziri mwenye dhamana kurekebisha kiwango cha faini kwa kuzingatia thamani ya fedha kwa wakati huo bila kusubiri kupeleka muswada Bungeni (*Currency Points*);

- (e) Uwezekano wa kuwa na Sheria itakayoruhusu watuhumiwa kwenye Mahakama za Mwanzo kuwakilishwa katika kesi zao na watu wenye ujuzi wa sheria lakini hawana Shahada ya Sheria (*Paralegals*).

Mheshimiwa Spika, Madai na Sheria za Kimataifa, Wizara iliendelea kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali na taasisi nyingine za Serikali. Wizara ilisimamia mikataba mbali mbali inayohusu mikopo ya Serikali, Ugavi, Ubinafsishaji na Uwekezaji, Ushirikiano wa Kimataifa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Wizara imeendelea kuiwakilisha Serikali katika mashauri ya madai Mahakamani na kwenye Mabaraza. Mashauri 225 yalifunguliwa na kuendeshwa katika Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu. Kati ya mashauri hayo, mashauri 49 yalitolewa maamuzi na yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa.

Huduma za Kabidhai Wasii, katika Mwaka wa Fedha wa 2004/05, Wizara, kwa msaada wa *UNICEF* ilikamilisha uenezaji wa Mradi wa Usajili wa Ndoa, Vizazi na Vifo katika Wilaya 120 za Mikoa ya Tanzania Bara. Katika hatua za kuimarissha utendaji, Wilaya 80 zilikaguliwa na mafunzo kutolewa kwa watumishi kuhusu namna ya kuimarissha usajili na ukusanyaji wa mapato. Pia, katika Mwaka wa Fedha wa 2004/2005, jumla ya ndoa 82,092 zilisajiliwa. Aidha, Wizara inaendelea kukamilisha taratibu za kuifanya Ofisi ya Kabidhi Wasii kuwa Wakala wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kushughulikia masuala ya Haki za Binadamu na Mambo ya Katiba kama ifuatavyo:-

- (a) Taarifa moja ya utekelezaji wa Haki za Binadamu iliwasilishwa katika Kamati ya Kamisheni ya Haki za Binadamu inayosimamia utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa Dhidi ya Ubaguzi wa Rangi;
- (b) Imeendelea kutoa ushauri wa kisheria kwa Wizara, Idara na taasisi za Serikali kuhusu uzingatiaji wa Katiba na masuala ya Haki za Binadamu;
- (c) Imesimamia mashauri ya Kikatiba 13 Mahakamani na malalamiko 4 kwenye Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;
- (d) Imeshiriki Mkutano wa 36 wa Kamisheni ya Haki za Binadamu ya Afrika;
- (e) Imeandaa rasimu ya taarifa ya Haki za Binadamu kuhusu Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Haki za Watu ambayo itawasilishwa kwenye Kamisheni kabla ya mwisho wa mwaka huu;
- (f) Kwa kushirikiana na Taasisi ya Raul Wallenburg ya Chuo Kikuu cha Lund, Sweden na *UNDP* iliendesha mafunzo kuhusu uandishi wa taarifa kuhusu haki za binadamu chini ya mkataba wa Kimataifa

kuhusu haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni (*Economic, Social and Cultural Rights*);

- (g) Iliandaa miswada ya Sheria ya Mabadiliko ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Sheria ya Utumishi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2004/05, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imetembelea Magereza 15 na Vituo vya Polisi 24 katika Wilaya 15 za Tanzania Bara kwa lengo la kukagua na kujionea hali za wafungwa na mahabusu waliopo. Pia Tume imetembelea Tarafa, Kata na Vijiji katika Wilaya 15 za Tanzania Bara na kufanya mikutano ya hadhara kwa lengo la kuwaelimisha wananchi kuhusu huduma zitolewazo na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Taarifa ya ziara za Tume Wilayani na Ulaguzi wa Magereza na Vituo vya Polisi kwa mwaka 2003/04 ilikwishaandaliwa na kusambazwa kwa mamlaka husika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mfuko wa Elimu kwa Watoto (*UNICEF*) imezindua mradi wa Uchunguzi Shirikishi kuhusu vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Uchunguzi huu utafanyika katika Wilaya 11 zilizoteuliwa Tanzania Bara. Wilaya hizo ni pamoa na Moshi Vijijini, Morogoro Vijijini, Kinondoni, Mafia, Magu, Kibondo, Kilwa, Lushoto, Mbeya Mjini, Mbinga na Tabora Mjini. Vile vile, Tume iliandaa na kusambaza vipeperushi vinavyoelezea mradi huo. Aidha, katika mwaka wa 2004/2005, Tume ilishughulikia jumla ya malalamiko 6,859 na kati ya hayo, malalamiko 1,564 yalikamilishwa. Uchunguzi wa malalamiko 5,295 kwa upande wa Tanzania Bara bado yanaendelea kushughulikiwa na upo katika hatua mbali mbali. Malalamiko 136 ya Tanzania Visiwani (Zanzibar) bado hayajashughulikiwa kutokana na taratibu za kisheria.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2004/2005, Wizara iliendelea kuimarisha miundombinu ya utoaji haki kama ifuatavyo:

- (a) Ukarabati wa majengo ya Mahakama Kuu, vituo vya Songea, Mwanza na Sumbawanga ulikamilika;
- (b) Ukarabati wa Jengo la Forodhani ambalo litakuwa makao ya muda ya Mahakama ya Rufani unatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa Mwaka wa Fedha wa 2005/2006;
- (c) Ukarabati wa majengo ya Mahakama Kuu Iringa na Moshi bado unaendelea.
- (d) Utaratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Mahakama Kuu Bukoba umekamilika;
- (e) Ujenzi wa majengo ya Mahakama ya Wilaya Kongwa, Mbarali na Ludewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi, Sumbawanga umekamilika;

- (f) Ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya za Hai, Ludewa, Bunda na Mpwapwa umekwisha anza;
- (g) Ujenzi wa jengo jipya eneo la Sinza kwa ajili ya matumizi ya Mahakama ya Mwanzo ya Manzese, Dar es Salaam upo katika hatua za mwisho;
- (h) Kufuatia Mpango endelevu wa ujenzi na ukarabati majengo ya Mahakama za Mwanzo, majengo 51 ya Mahakama hizo yanajengwa na mengine yanafanyiwa ukarabati katika Wilaya 43 nchini;
- (i) Ukaguzi wa Mahakama uliimariswa kwa kuzipatia usafiri Mahakama zote za Hakimu Mkazi nchini;
- (j) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imenunua majengo mawili kwa ajili ya Ofisi za Kanda za Songea na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria (*Legal Sector Reform Programme*). Katika Mwaka wa Fedha wa 2004/2005, Wizara yangu ilikamilisha uhuishwaji wa Mkakati wa Kati 2000-2005 na kuwa na Mkakati wa Muda wa Kati wa 2005/2006 - 2007/2008 uliopitishwa na Kamati ya Uongozi - *Steering Committee* mwezi Desemba 2004 na kuzinduliwa Mwezi Machi 2005. Mkakati huu ambao utaanza kutekelezwa katika Mwaka huu wa Fedha, utahusisha asasi zote zinazosimamia haki au kuchangia katika kuleta mazingira bora ya upatikanaji wa haki.

Asasi hizo ni; zile zilizo chini ya Wizara yangu kwa maana ya Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Tume ya Kurekebisha Sheria; Wizara ya Mambo ya Ndani kwa maana ya Ofisi ya Usajili wa Vyama Hiari, Polisi na Magereza, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa maana ya Usajili wa Mali isiyohamishika au Msajili wa Hati, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa maana ya usajili na utoaji wa leseni za biashara chini ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni, Wizara ya Sayansi Technologia na Elimu ya Juu kwa maana ya Vyuo vyote vinyavyotoa elimu ya Kisheria, na Wizara ya Kazi, Maendelo ya Vijana na Michezo kwa maana ya huduma za Ustawi wa Jamii hususan zile za Watoto Watukutu na wale wanaoishi katika mazingira magumu. Aidha, asasi zisizo za Kiserikali (*NGOs*) ambazo zinashughulika na huduma za Msaada wa kisheria (*legal aid*), usambazaji wa habari za kisheria na mafunzo ya kisheria nazo zimehusishwa katika utekelezaji wa Makakati huo.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, Mkakati unalenga kuboresha maeneo ya kipaumbele yafuatayo:

- (a) Mfumo wa Sheria za Nchi: lengo ni kuboresha Sheria zitoe haki na fursa sawa ya usalama na maendeleo ya kijamii, kutenganisha jukumu la upeletezi na mashtaka, kuboresha uwezo wa upeletezi na mashtaka na kuboresha ubora wa tafiti/tathmini katika mfumo wa Sheria za nchi;

- (b) Haki kwa Wasiojiweza: kuboresha haki kwa walio rumande (watu wazima na watoto), usambazaji wa kumbukumbu za kisheria, haki vijijini na haki kwa watoto walio katika mazingira magumu;
 - (c) Haki za Binadamu na za Kiutawala, kuimarisha uwezo wa asasi zinazota haki katika kuzingatia haki za binadamu, kuimarisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kuzingatia uwazi na kupunguza mienendo ya rushwa katika asasi za Sekta ya Sheria na kuimarisha na kuboresha utendaji wa Mabaraza ya Usuluhihi yanayoundwa na Sheria mbalimbali;
 - (d) Ujuzi na Taaluma ya Uanasheria, kujenga uwezo wa kutoa elimu inayokidhi matakwa ya mabaliko nchini, kuboresha elimu ya vitendo kwa wahitimu wa Shahada ya Sheria na kujenga uwezo kwa kutoa elimu endelevu (*continuing educational programme*);
 - (e) Huduma katika Taasisi za Sheria: kuimarisha menejimenti na uratibu katika taasisi, uwezo, motisha na maadili ya watendaji na mazingira ya kazi;
 - (f) Uongozi, Udhibiti na Uratibu wa *Programme*: kuongeza kasi ya utekelezaji na usimamizi wa *Programme*, uwezo wa kisera na Mikakati ya Uongozi katika taasisi, usambazaji wa taarifa za mafanikio na matakwa ya maboresho na uwezo wa kuleta mabadiliko sahihi katika Sekta.
- Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2004/05, Wizara ilikamilisha maandalizi ya Mradi wa *Tanzania Accountability Transparency and Integrity (ATIP)* ambao lengo lake ni kuboresha maadili na uwajibikaji nchini. Chini ya mradi huu, maandalizi yafuatayo yalikamilishwa:-(i) Mpango wa kuboresha uwezo wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (*NBAA*) katika kujenga mazingira bora ya Utawala Bora wa kitaaluma na katika usimamizi wa fedha;
- (ii) Mpango wa kuimarisha Idara ya Nyaraka, Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Umma na kuanzisha kituo cha Nyaraka (*National Records Centre*);
 - (iii) Mpango wa muda mrefu wa kuboresha majengo ya Mahakama unaainisha mahitaji ya majengo, fedha za matengenezo na wajibu wa kila mdau;
 - (iv) Mpango wa kuanzisha mfumo wa mawasiliano baina ya asasi zinazosimamia haki (*Legal Sector Integrated Management Information System*);
 - (v) Mpango wa kuanzisha *Law School*;
 - (vi) Mpango wa kuboresha uwezo wa asasi za hiari katika kuhamasisha uzingatiaji wa Utawala Bora nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wizara inaendelea kukamilisha tathmini ya athari za kimazingira na muongozo wa namna ya kutoa rasilimali kwa asasi za hiari. Tathmini hizi zinatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Agosti, mwaka huu, ili hatimaye mradi uwasilishwe kwenye Bodi ya Benki ya Dunia kwa majadiliano na maafikiano.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *Quick Start* ulikoma mwezi Desemba, 2004. Chini ya mradi huo tafiti mbalimbali zilifanyika ikiwa ni pamoja na mapitio na uhuishaji wa Sheria zinazoongoza taasisi za Sheria, uboreshaji wa miundo ya kiutawala, usimamizi na mgawanyo wa kazi na utafiti wa kuinua mapato yatokanayo na Sekta ya Sheria. Tafiti hizi zimeandaa mipango ya uboreshaji inayoainisha vipaumbele majukumu ya kila mdau na gharama ambayo ni sehemu ya Mkakati wa Muda wa Kati wa 2005/2006 – 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, michoro na makadirio ya gharama za uboreshaji wa Mahakama za Watoto za Mtwara na Mbeya ilikamilika chini ya mradi huo. Aidha, mradi wa majaribio wa ujenzi na ukarabati wa Mahakama za Mwanzo chini ya Mradi wa *Quick Start* mkoani Manyara na Arusha haukukamilika. Hivyo, mradi huu umejumuishwa kwenye Mkakati wa Muda wa Kati wa 2005/2006 – 2007/2008 utakaoanza kutekelezwa mwezi Julai, 2005.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Sekta ya Sheria mwaka jana nilieleza hatua iliyofikiwa katika maandalizi ya utayarishaji wa Sera ya Taifa ya Sekta ya Sheria. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Mshauri Sanifu (*Consultant*) amekwisha wasilisha Rasimu ya Sera hiyo Wizarani kwa mapitio na hatimaye kuwasilishwa kwenye Warsha ya Wadau kwa ajili ya kujadiliwa na kupata maoni yao kati ya Julai na Desemba, 2005.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu sote, Taifa letu linaendelea na vita dhidi ya umaskini na rushwa. Masuala haya ni moja ya vipingamizi katika kufanikisha kukua kwa uchumi wetu na kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Aidha, masuala haya ni pingamizi katika Utawala Bora. Katika vita dhidi ya rushwa, jumla ya Semina 12 ziliendeshwa kwa ajili ya Watumishi wa Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti UKIMWI iliendesha semina ya kuwaelimisha watumishi kuzingatia masuala ya UKIMWI katika mipango na bajeti ya Wizara. Vile vile, Semina 3 zimeendeshwa kwa ajili ya kuwaelimisha watumishi wa Wizara yangu namna ya kujikinga na kuhudumia waathirika wa UKIMWI. Hali kadhalika, Wizara imeandaa Mkakati wa Muda wa Kati wa UKIMWI ambao utasaidia kubuni mbinu za kukabiliana na janga hili. (*Makofî*)

Aidha, ripoti ya mapitio ya Sheria mbalimbali zinazoathiri masuala ya huduma na tiba kwa walioathirika na UKIMWI, Wanawake na Watoto yatima ilizinduliwa mwezi Januari, 2005. Ripoti hii imebainisha mapungufu yaliyopo katika Sheria mbalimbali na

kutoa mapendekezo ya kuziboresha. Hata hivyo, lengo la baadaye ni kuwa na Sheria moja ya kudhibiti uenezaji wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikieleza juu ya utafiti wa Sheria za Ndoa, Watoto na Mirathi takriban miaka miwili sasa. Masuala haya yanahusu na kugusa maslahi na imani za Watanzania wengi. Kutokana na hali hiyo, Serikali imeona umuhimu wa kupata maoni zaidi kutoka kwa wananchi kuititia utaratibu wa *white paper*. Hivyo, Wizara yangu bado inaendelea kuyafanya kazi mapendekezo ya Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mirathi na Sheria ya Watoto na itaendelea kusimamia shughuli ya ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wadau mbali mbali kuhusu uboreshaji wa Sheria hizi ili ziweze kukidhi matakwa ya jamii. Aidha, suala la Mahakama ya Kadhi nalo litafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2004/05 ulikuwa wa mafanikio makubwa. Pamoja na mafanikio hayo mazuri, Wizara kwa ujumla wake imeendelea kukabiliwa na matatizo ambayo yanaathiri kasi na ufanisi wa utendaji. Matatizo hayo yanatokana hasa na Bajeti ya Serikali kutoweza kukidhi mahitaji halisi ya asasi za Wizara. Baadhi ya sehemu ambazo bado zinaendela kuathirika ni pamoja na: Ubovu na uchakavu wa vitendea kazi; Uchakavu, uhaba na ukosefu wa majengo na ofisi na Uhaba wa miundombinu ya kisasa. Aidha, kumeendelea kuwa na upungufu wa watumishi hasa Majaji, Mahakimu na Mawakili wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea mafanikio na matatizo katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2004/2005 sasa napenda nilezee Mpango na Malengo ya mwaka 2005/2006. Katika Mwaka wa Fedha wa 2005/2006, utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria umepewa kipaumbele na Serikali. Mwelekeo huu wa Serikali tunaojivunia, una umuhimu wa pekee kwa sababu masuala yanayohusu Wizara yangu yanagusa maeneo yote ya Kiuchumi na Kijamii kwa njia ya kutoa haki na kuhakikisha jamii inaishi kwa usalama na amani. Aidha, mabadiliko yanayoendelea hapa nchini na duniani kote katika Sera za kiuchumi na kijamii yanategemea sana kuwepo kwa Utawala Bora na Utawala unaozingatia Sheria. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo na ili kufanikisha azma ya Taifa ya Mkakati huo, Wizara, katika Mwaka wa Fedha wa 2005/2006 imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

A: Kuimarisha Mfumo wa utoaji Haki

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2005/2006, Wizara imepanga kuendelea kuboresha huduma zake za kisheria ili kuimarisha Utawala Bora na Utawala wa Sheria. Katika kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa mashauri nchini, mambo yafuatayo yamepangwa kutekelezwa:-

Mfumo wa Mahakama

- (i) Kuwa na mfumo wa Maafisa Utawala wa Mahakama (*Court Administrators*);
- (ii) Kuendelea kuziwezesha na kuziimarisha Kamati za Kusukuma Kesi (*Case Flow Management Committees*);
- (iii) Utaratibu wa kila Jaji na Hakimu kujipangia ratiba ya usikilizaji wa mashauri (*individual calendar*) utaendelea kuimariswa;
- (iv) Mahakama imeweka mkakati wa kuajiri Mahakimu Wakazi 50 na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 40;
- (v) Ukaguzi wa Ofisi za Kanda utaendelea kuimariswa kwa kuongeza mzunguko wa ukaguzi;
- (vi) Kitengo cha Biashara cha Mahakama Kuu kinafanya maandalizi ya kufungua Masjala ya kuandikisha mashauri ya biashara katika Kanda ya Mahakama Kuu Mwanza, chini ya Mradi wa *Business Environment Strengthening for Tanzania (BEST)*.

Mfumo wa Huduma za Kisheria

- (i) Ukaguzi wa Ofisi za Kanda utaendela kuimariswa;
- (ii) Kutekeleza mkakati wa kuajiri Mawakili wa Serikali 35;
- (iii) Kukamilisha taratibu zitakazowezesha Mawakili wa Serikali kuendesha kesi za jinai hadi ngazi za Mahakama za Wilaya;
- (iv) Kuendelea kuiimarisha Tume ya Kurekebisha Sheria;
- (v) Kuendelea kufanya mabadiliko katika Sheria za Mienendo ya Mashauri ya Madai na Jinai ili kuboresha upatikanaji haki kwa wakati chini ya Mradi wa *Business Environment Strengthening for Tanzania (BEST)*.

Haki za Binadamu:-

- (i) Kuendelea kuimarisha zaidi suala la utoaji elimu kwa umma kuhusu Haki za Binadamu ili wananchi na watendaji waelewe haki za msingi na namna ya kuzingatia masuala ya Haki za Binadamu zaidi;
- (ii) Kuendelea kuandaa na kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa Mikataba mbalimbali ya Kimataifa juu ya Haki za Binadamu nchini;
- (iii) Kuratibu masuala yahusuyo Katiba na Haki za Binadamu na kuendesha kesi za Kikatiba Mahakamani;

(iv) Kusimamia Serikali katika chunguzi zinazoendeshwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora nchini, kusimamia mashauri yanayosikilizwa na Tume ya Haki za Binadamu na Haki za Watu Barani Afrika; na katika Tume zilizoundwa chini ya mikataba mbalimbali ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa;

(v) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itaendelea kuongeza kasi ya uchunguzi wa malalamiko ya wananchi na kutembelea Magereza na vituo vya Polisi katika Wilaya zilizobaki kuhakikisha kuwa Haki za Binadamu na misingi ya Utawala Bora inaheshimiwa na kulindwa.

(B) Kuimarisha Miundombinu ya utoaji haki

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililieleza Bunge lako Tukufu nia ya Serikali ya kuviboresha na kuvirudishia hadhi vyombo vya utoaji haki nchini. Katika Mwaka wa Fedha wa 2005/2006, Wizara itaendela kutekeleza yafuatayo:

(i) Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi katika ofisi zote, yaani Mahakama, Ofisi ya

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Tume ya Kurekebisha Sheria;

(ii) Kuendeleza utekelezaji wa Mpango Endelevu wa Mahakama za Mwanzo;

(iii) Kuendelea kuzipatia vitendea kazi muhimu Mahakama zote na ofisi zote; na

(iv) Kuendelea kuboresha na kuimarisha upatikanaji wa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na vifaa vya ofisini, usafiri, majengo ya Mahakama na Ofisi.

(C) Utafiti na Uandishi wa Sheria:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2005/2006, Wizara itaendelea na majukumu yake ya uandishi wa miswada ya Sheria na sheria ndogo ndogo.

Aidha, uandaaji na uchapishaji wa miswada mbalimbali utaboreshwu kwa kiwango cha hali ya juu kutokana na uwekaji wa mtambo maalum wa uchapishaji ambao umeunganishwa kati ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria na Mpiga Chapa wa Serikali. Vile vile, kazi ya kutafsiri Sheria mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili itaendela kutekelezwa na kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, pia, Wizara kwa kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria itaendelea na utafiti, uchambuzi, na uhuishaji wa sheria mbalimbali ikiwa ni pamoja na utafiti wa Sheria ya Vyombo vya Habari (*Media Law*), juu ya uwezekano wa kutunga

Sheria za UKIMWI - (*HIV/AIDS*), *e-Commerce na e-Government* na Uraia wa nchi mbili (*Dual Citizenship*).

D: Madai na Sheria za Kimataifa:-

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuimarisha huduma za utoaji ushauri wa Kisheria kwa Serikali na Taasisi zake katika nyanja za madai na Sheria za Kimataifa. Pia, itaendelea kuishauri Serikali kisheria katika masuala yote yanayohusu mikataba ya ndani na Kimataifa. Aidha, Wizara itaendelea kuiwakilisha Serikali katika mashauri ya madai Mahakamani na kwenye Mabaraza.

E: Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria (*Legal Sector Reform Programme*)

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2005/2006, Wizara itatekeleza Mkakati wa Muda wa Kati wa 2005/2006 – 2007/08 wa Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria (*Legal Sector Reform Programme: Medium Term Strategy 2005/2006 - 2007/2008*), ambao maudhui yake nimeyaeleza awali.

Kwa kuanzia, Wizara inaandaa muongozo wa kusimamia rasilimali za Programmu (*Financial Management Manual*) ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Ushirikiano baina ya asasi tekelezi na Wafadhili (*Memorandum of Understanding*). Hivi vyote vinalenga kuboresha upatikanaji wa rasilimali katika Sekta, kuimarisha mahusiano baina ya watekelezaji pamoja na kuweka bayana jukumu la kila mmoja katika kufanikisha azma ya pamoja ya Haki Sawa kwa Wote na kwa Wakati muafaka. Aidha, Mkakati utaendeleza mafanikio yaliyopatikana hadi sasa, shughuli zilizoanzishwa chini ya Mradi wa *Quick Start*, kama vile ujenzi wa Mahakama mbalimbali katika Mikoa ya Manyara na Arusha na zile za Watoto Watukutu. Aidha, majadiliano na Benki ya Dunia yanaendelea ili iweze kuchangia kwenye kapu la kuboresha Sekta ya Sheria (*Basket Funding*) kupitia Mradi wa *ATIP*. Vile vile, miradi ifuatayo itatekelezwa kwa pamoja chini ya Mkakati huo:

(c) Mradi wa *Improving the Legal Framework for Economic Development* ambao utakaogharimiwa na Serikali za Ujerumani na Tanzania una lengo la kujenga uwezo wa kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo katika Sekta ya Sheria na kuandaa muongozo wa usimamizi wa programu (*Legal Sector Reform Programme: Monitoring and Evaluation Manual*); kuhuisha Sheria na mabadiliko ya kiuchumi ili kuongeza kasi ya uwekezaji nchini. Pia, mradi utagharimia ushauri, vifaa vya ofisi na mafunzo ya ndani na ya nje ya nchi. Madhumuni ya mafunzo haya ni kuongeza ujuzi wa kuongoza mabadiliko (*change management*) kwa watawala wa vyombo vya Kisheria, utafiti wa kisheria na maendeleo ya kisheria; na

(d) Mradi wa *Strengthening Good Governance in Delivery of Justice* ambao unagharimiwa na Serikali ya Ubelgiji na Tanzania una lengo la kuboresha utawala bora katika utoaji haki. Mradi huu utagharimia ushauri, samani na vifaa vya ofisi na mafunzo ya ndani na ya nje ya nchi. Ushauri utalenga katika uboreshaji wa mfumo wa usimamizi na utoaji haki, wakati mafunzo yatalenga katika kuboresha uwezo wa kuzingatia

usimamizi na uwajibikaji kwa Watumishi wa vyombo vya kutoa haki hususan kubadili tabia na mwenendo ili kujenga maadili ya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilielezea jitihada zinazofanywa za kukipanua na kukiimarisha Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto ili kuweza kukabiliana na tatizo la upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Makarani wa Mahakama. Katika kutekeleza azma hiyo, Mahakama ya Tanzania imejizatiti kutekeleza mpango endelevu unaojulikana kama Upanuzi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto. Katika Mwaka wa Fedha wa 2005/2006, fedha zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa ukumbi wa miadhara (*Lecture Theatre*). (*Makofî*)

F: Mafunzo na Maendeleo ya Watumishi

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2005/2006, Wizara itaendela na juhudzi za kuimarisha ufanisi katika Asasi za Wizara kwa kuwapatia mafunzo ya kitaalamu watoaji haki ili kuboresha utoaji huduma kwa Wateja na Wananchi kwa ujumla. Ili kufanikisha dhamira hiyo, Wizara itafanya yafuatayo:-

- (a) Kuwapatia mafunzo ya vitendo Majaji, Mahakimu Wakazi, Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo chini ya Mradi wa *Business Environment Strengthening for Tanzania (BEST)*;
- (b) Kuwaongeza viwango vya elimu Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo Makarani wa Mahakama na watumishi mbalimbali katika Wizara;
- (c) Kuwasomesha Mawakili wa Serikali katika viwango vya shahada ya uzamili, katika mafunzo ya muda mfupi na watumishi wengine katika mafunzo mbalimbali ya muda mfupi;
- (d) Kuwaongeza mafunzo watumishi wa Haki za Biandamu na Utawala Bora juu ya namna ya kuboresha huduma za haki za binadamu;
- (e) Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi na motisha kwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Sekta ya Sheria katika Mwaka wa Fedha wa 2005/2006, Wizara itaendelea kutoa umuhimu katika kukamilisha uandaaji wa Sera ya Taifa ya Sekta ya Sheria.

G: Masuala muhimu ya Kitaifa

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu sote, Ukimwi ni janga la kitaifa na dunia kwa ujumla. Janga hili limekuwa likiathiri utendaji na kupunguza nguvu kazi. Katika Mwaka wa Fedha wa 2005/2006, Wizara, kwa kushirikiana na Wadau wengine itaendeleza jitihada zake za kutoa elimu ya ukimwi kwa watumishi wake ili kukabiliana

na janga la ukimwi. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Afya ili kuandaa Sheria ya Kudhibiti uenezaji wa UKIMWI. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, rushwa imeendelea kuwa tatizo kubwa katika jamii yetu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2005/2006, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi husika katika utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Rushwa. Aidha, Wizara itaendelea kuendesha warsha kwa wafanyakazi wake kuwashamasisha na kuwapa elimu juu ya mbinu mbalimbali za kupambana na rushwa katika Sekta ya Sheria na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikizingatia na kutekeleza kwa dhati sera za Mazingira na Jinsia. Hivyo, Wizara yangu itaendelea kutoa mchango katika kuhifadhi na kutunza mazingira. Aidha, masuala ya Jinsia yataendelea kuzingatiwa na kupewa umuhimu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio mengi yaliyopatikana katika Wizara wakati wa Serikali ya Awamu ya Tatu, bado Wizara inakabiliwa na changamoto kubwa. Mwaka 2000 Serikali ya Awamu ya Tatu ilizindua Mkakati wa Kuondoa Umaskini ambao ulihusisha Sekta chache za jamii na utawala kwa lengo la kuwapunguzia wananchi umaskini wa kipato na kuwaongezea uwezo wa kuboresha maisha yao na Taifa kuongeza uwezo wake wa kutoa huduma bora zaidi za jamii. Kutokana na mabadiliko ya kisera, Mkakati huo umehuishwa na kuwa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) ambapo Sekta zote zimehusishwa katika kuchangia kukuza uchumi, kupunguza umaskini na kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Ili kuweza kukidhi utekelezaji wa MKUKUTA, Serikali imetilia mkazo uboreshaji wa Sekta ya Sheria na kuipa kipaumbele kama kigezo cha kuharakisha maendeleo nchini. Jambo la msingi, ni kuifanya Tanzania iwe na uwezo wa kusuluhiha migogoro ya wananchi kwa usahihi na kwa haraka ili kuondosha kero ya wananchi ya kusubiri matokeo ya kesi zao kwa muda mrefu na hivyo kuboresha mazingira ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Wananchi watapenda kuona Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA), haukwamishwi na taratibu za Sheria zilizopitwa na wakati au zisizoweza kukidhi mahitaji yao ya kila siku, bali wanawezeshwa na kusaidiwa na taratibu hizo. Mfumo wetu wa Sheria unapaswa kutoa mchango katika kufufua uchumi na kuondoa umaskini.

Rasilimali kubwa itahitajika kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii. Kutokana na uchumi wetu kuwa mdogo, rasilimali itakayotolewa ilenye kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mkakati wa Muda wa Kati wa Programu hii. Utekelezaji wa Programu hii ulenye katika matokeo yafuatayo:

- (a) Kuongezeka kwa kasi ya utoaji haki ili kutatua migogoro ya wananchi kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa;
- (b) Kuboresha na kuimarisha huduma za Kisheria kwa maskini na wasiojiweza;

- (c) Kuwepo Majaji na Mahakimu wa kutosha kusikiliza na kutolewa hukumu haraka kwa mashauri yanayofunguliwa;
- (d) Usalama wa wananchi na mali zao uwe wa uhakika;
- (e) Mfumo wa Sheria unaozingatia haki za makundi maalum ya Wanawake, Watoto na Walemavu;
- (f) Uwezo mkubwa wa kulinda viwango vya hali ya juu vya haki za binadamu;
- (g) Kuhimili changamoto zinazotokana na mahitaji ya demokrasia yanayozidi kuongezeka;
- (h) Kumudu usimamizi wa mageuzi yanayoendelea nchini katika nyanja mbalimbali; na
- (i) Kusimamia kwa dhati mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, ili utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria (*Legal Sector Reform Programme*) uweze kuwa wa mafanikio, hapana budi utekelezaji wake uende sambamba na Programu nyingine zinazotekelezwa Serikalini. Programu zote hizi ni muhimu katika mkakati wa maendeleo ya nchi yetu. Hata hivyo, utekelezaji wa Programu hizi unategemea sana mabadiliko ya Sekta ya Sheria. Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria (*Legal Sector Reform Programme*) inatekelezwa katika mfumo wa pamoa na Wadau wa Sekta ambao wanahusika moja kwa moja na wale ambao kwa namna moja au nyingine nao wanahusika na masuala ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya Sekta hii yanapaswa kwenda kwa kasi inayoendana na ile inayofanyika katika Programu nyingine. Vile vile Programu hii inapaswa kuwa na ubora huo huo, ili maendeleo ya nchi katika Sekta mbalimbali yawiane. Hivyo, mafanikio ya utekelezaji wa Programu hiyo utapatikana kwa kujenga usimamizi na uratibu madhubuti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Jaji Amir Ramadhani Manento aliyeuleliwa na Rais kuwa Jaji Kiongozi mwezi Septemba, 2004 na Waheshimiwa Regina M. Rweyemamu, Richard E.S. Mziray, Sauda Mjasiri, Kipenka M. Musa na Mohamed C. Othman kuwa Majaji wa Mahakama Kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie hotuba yangu kwa kuwashukuru Viongozi, na Watendaji Wakuu na Watumishi wote katika Wizara yangu ambao kwa kipindi kirefu wamekuwa wakinipatia msaada mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kuiongoza Wizara. Naomba niwataje kwa majina; Mheshimiwa Jaji Mkuu Barnabas Albert Samatta, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mheshimiwa Jaji Kiongozi Amir Ramadhani Manento, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Mheshimiwa Jaji Robert H. Kisanga, Mwenyekiti wa Tume

ya Kurekebisha Sheria Mheshimiwa Jaji Anthony Bahati na Mwenyekiti wa Bodii ya Shirika la Sheria Tanzania Bibi Mwanaidi Maajar. (*Makofî*)

Aidha, nawashukuru Watendaji Wakuu wa vyombo mbalimbali viliyvo chini ya Wizara hususan Bwana Johnson P.M. Mwanyika, Naibu Mwanasheria Mkuu na Katibu Mkuu wa Wizara, Bwana Augustine. G. Mwarija, Msajili wa Mahakama ya Rufani Tanzania, Bw. Matt-Chikawe, Katibu Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Bw. Gad J. K. Mjemmas, Katibu Mtendaji, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Bibi Daria Bigeye, Kaimu Mshauri Mkuu wa Shirika la Sheria Tanzania.

Msaada wao umenisaidia sana katika kutekeleza majukumu yangu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa nchi wahisani na taasisi za kimataifa ambazo zimeendelea kutoa misaada mbalimbali kwa ajili ya kuiendeleta na kuisaidia Sekta ya Sheria nchini. Naomba niwataje kwa majina Serikali ya Canada, Denmark, Ujerumani, Ubeligiji, Ireland, Marekani, Uingereza, Finland, Norway, Uhlanzi, Sweden; na Mashirika ya Kimataifa ya Benki ya Dunia, *UNDP*, *USAID*, *UNICEF*, *GTZ*, *CIDA* (Canada) na *SIDA* (Sweden).

Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kutekeleza malengo na majukumu yake yaliyoainishwa kulingana na mwelekeo kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006 na kama yalivyochanguliwa katika vitabu nya makisio, naomba Bunge lako Tukufu likubali Wizara yangu ipatiwe jumla ya Shs.49,986,929,600 ambazo kati ya hizo, Shs. 6,107,562,100 ni fedha za nje. Mchanganuo wake ni kama ufuatao:

Mlheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ni kama ifuatavyo:-

Fungu 40 - Mahakama ya Tanzania

Matumizi ya Kawaida.....Shs.	27,877,918,500
Matumizi ya Maendeleo...Shs.	3,000,000,000
JumlaShs.	30,877,918,500
Fungu 41 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	

Matumizi ya Kawaida.....Shs.	7,234,165,900
Matumizi ya Maendeleo (ndani) Shs.	400,000,000
Matumizi ya Maendeleo (Nje) ...Shs.	6,107,562,100
Jumla	Shs.13,741,728,000
Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	

Matumizi ya Kawaida.....Shs.	2,709,058,900
Matumizi ya Maendeleo.....Shs.	-
Jumla	Shs. 2, 709,058,900

Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria

Matumizi ya Kawaida.....	Shs. 761,508,200
Matumizi ya Maendeleo.....	Shs. -
Jumla	Shs. 761,508,200

Fungu 64 - Mahakama ya Biashara

Matumizi ya kawaida	Shs. 782,716,000
Matumizi ya Maendeleo	Shs. 510,000,000
Jumla	Shs. 1,292,716,000

Fungu 90 - Mahakama ya Ardhi

Matumizi ya kawaida	Shs. 604,000,000
Matumizi ya Maendeleo	Shs. -
Jumla	Shs. 604,000,000

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2005/2006, Wizara hii imekisia kukusanya jumla ya Shs.1,728,391,432 kama maduhuli ya Serikali kwa mchanganuo ufuatao:

Fungu 40 Shilingi 460,122,000/=, Fungu 41 Shilingi 517,925,432 Fungu 55 shilingi, 344,000, Fungu 59 -, Fungu 64 shilingi 700,000,000, Fungu 90 shilingi 50,000,000, Jumla Shilingi 1,728,391,432/=.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. PASCHAL C. DEGERA (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 81(1), Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2004, naomba kuwasilisha Taarifa na Maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa kazi za Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba katika mwaka wa Fedha wa 2004/2005 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha wa 2005/2006 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ni moja kati ya Wizara ambazo Bajeti zake zinashughulikiwa na Kamati hii kama ilivyoainishwa katika Kanuni Namba 93, Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ilikuwa na Kikao tarehe 2 Juni, 2005 mjini Dar es Salaam kushughulikia Bajeti ya Wizara hii. Katika kikao hicho Kamati ilipata fursa ya kusikia Hotuba ya Waziri wa Sheria na Mambo ya

Katiba iliyowasilishwa na Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Mbunge na Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba. Maeleo ya kina ya hotuba hiyo yamo katika kitabu cha Wizara hiyo cha mwezi Mei, 2005.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, inahusisha Mafungu yafuatayo:-

Fungu 40 Mahakama, Fungu 41 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Fungu 55 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Fungu 59 Tume ya Kurekebisha Sheria, Fungu 64 Mahakama ya Biashara na Fungu 90 Mahakama ya Ardhi

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa Dira na Majukumu ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ni haki kwa wote na kwa wakati. Dira hii ina lengo la kuwa na maendeleo ya haki ya kijamii, usawa na utawala wa sheria. Aidha, dira hii ndiyo inayoongoza utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, ni pamoja na kujenga mazingira mazuri na thabiti ya sheria na kanuni ya kiuchumi na kijamii. Katika kutekeleza majukumu hayo, Wizara ina wajibu wa kusimamia utoaji haki kwa wananchi, kuhakikisha kuwa sheria na taratibu za nchi zinafuatwa, kuishauri Serikali kuhusu masuala yote ya sheria na kudumisha utawala bora, amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Kamati ilitoa jumla ya maagizo matano kama ifuatavyo:-

Kwanza uimarishaji wa usafiri kwa mahakimu. Mkakati wa kupunguza uhaba wa mahakimu katika mahakama za wilaya, ajira kwa wahitimu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, kuondoa msongamano wa mahabusu pamoja na ukarabati wa majengo ya Mahakama za Mwanzo na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa karibu maagizo yote ya Kamati yalitekelezwa ipasavyo, isipokuwa agizo moja tu juu ya Uimarishaji wa Usafiri kwa Mahakimu, ambalo pamoja na mikakati mingine, maeleo ya Wizara yalionyesha kuwa Serikali imebuni mpango wa kuwakopesha pikipiki mahakimu wa mahakama za mwanzo. Hata hivyo, imeelezwa kuwa mpango huu unakwenda taratibu sana na kwamba wakopeshaji wa pikipiki wameweka masharti magumu ambayo yanasaababisha utekelezaji wa mpango huu usikamilike kama ilivyokusudiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Kamati ilielezwa kuwa kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kama zifuatavyo:-

Kuziimarisha Kamati za kusukuma kesi (*Case Flow Management Committees*); kuendelea kupunguza mlundikano wa kesi katika mahakama zetu; kuendelea kuimarisha na kuboresha mazingira ya kazi na vitendea kazi katika sekta ya sheria, kushirikisha jamii

katika kuendesha shughuli za kisheria na kuimarishe idara ya Kabitih Wasii kuweza kuwa wakala wa Serikali na kazi nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ilioomba Kamati yangu iidhinishie jumla ya shilingi 49,986,929,600 kwa mafungu yote yaliyotajwa awali ili iweze kukamilisha shughuli zilizopangwa. Kamati inapendekeza kuwa maombi haya yakubaliwe na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kuelezea maagizo ya Kamati kwa niaba ya Bunge lako Tukufu katika mwaka wa fedha 2005/2006 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzoefu ambao Kamati yangu imepata baada ya kufanya ziara katika magereza ya hapa nchini, imedhihirika kuwa kuna idadi kubwa ya wahalifu waliohukumiwa kunyongwa, lakini wamekaa kwa muda mrefu bila kunyongwa. Hali hii imesababisha waathirike kisaikolojia na kuishi katika hali ya wasiwasi kwa kutojua hatma ya maisha yao. Kwa sababu hiyo Kamati inaagiza na kuiomba Serikali ilifuatilie suala hili na ikiwezekana imshauri Mheshimiwa Rais atoe msamaha kwa watu waliokaa muda mrefu gerezani badala ya kuwaacha waishi katika hali hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ufumbuzi kamili wa tatizo hili unakabiliwa na matatizo kadhaa ikiwa ni pamoja na masharti magumu ya mikopo ya pikipiki, Kamati inaagiza kuwa Wizara iendelee kulitafutia ufumbuzi ikiwezekana kutafuta wakopeshaji wenyewe masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, ili kwenda sambamba na Dira ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, haki kwa wote na kwa wakati, Kamati inaagiza kuwa Wizara ijithidi kuboresha maslahi ya mahakimu wote nchini pamoja na kuwapatia vivutio vya kazi zaidi hususan mahakimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwisho ya kuwasilisha Taarifa ya Maoni ya Kamati katika Mkutano wa Ishirini wa Bunge lako Tukufu. Kwa kuwa hii ndiyo taarifa yangu ya mwisho, napenda kukutakia wewe binafsi, Waheshimiwa Wabunge wote mafanikio katika uchaguzi ulio mbele yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba nimshukuru Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Mbunge na Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba na wataalam wake kwa kushirikiana vema na Kamati wakati wote tulipopitia na kuchambua Bajeti ya Wizara hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao na kwa michango yao mizuri waliyoitao walipotekeleza mojawapo ya jukumu la Kamati la kupitia Bajeti ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati waliofanya kazi hiyo ni wafuatao, Mheshimiwa Athuman S.M. Janguo, Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe wengine ni Waheshimiwa wafuatao, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Grace Kiwel, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Zahoro Juma Khamis, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Ramadhani Khalfan, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mwananne Mcemba, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Dr. Nimrod Mkono, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda niwashukuru, Ndugu Charles Mloka, Ernest Zulu na Athuman Hussein, Makatibu wa Kamati hii, chini ya uongozi wa Bwana Damian Foka, Katibu wa Bunge, kwa kuihudumia vema Kamati hii na kutayarisha Taarifa ya Kamati mapema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, natamka kuwa naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha ahsante. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED JUMA KHATIB - (k.n.y. MSEMADI WA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA): Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwa niaba ya Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ya mwaka wa fedha 2005/2006 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(b)(c) na 81(1) Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, Katiba ni Sheria mama na mkataba maalum baina ya watawala na raia ambamo pamoja na mambo mengine huainishwa wajibu wa kushirikiana baina ya pande mbili hizi katika kuiendesha nchi. Kwa kifupi kabisa ni mkataba ambamo raia wana jukumu la kuamua ni nani mionganoni mwao awe mtawala na kukabidhiwa mamlaka ya kuiongoza Serikali na Taasisi zake kwa maslahi ya Taifa zima.

Mheshimiwa Spika, Katiba inayoandaliwa kwa ajili ya maslahi ya umma haipaswi kuwa na utata au kutoa mianya kwa baadhi ya watu kufanya mambo ambayo ni nje ya maslahi ya Taifa. Katiba ya aina hii haina budi kujadiliwa ipasavyo na kuwa wazi na fasaha katika mambo yote muhimu yanayohusu uongozi wa nchi na maslahi ya raia na mahusiano baina yao au baina yao na Serikali na taasisi zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya upinzani imebaini kasoro nyingi zilizomo ndani ya Katiba:-

Katiba ya sasa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliandikwa mnamo mwaka 1977 kukidhi mahitaji ya kidikteta ya chama kimoja. Ni Katiba ambayo haikuwahusisha kabisa wananchi wakati wa kuiandika.

Tume ya Msekwa iliyoundwa kuratibu kuvunganisha vyama vya *TANU* na *ASP* ndiyo hiyo hiyo ambayo iligeuzwa ghafla baada ya Muungano wa vyama hivyo ikapewa kazi ya kuandika katiba kinyume na makubaliano ya mwaka 1964 yaliyouna Muungano. Aidha, marekebisho yote (*Amendments*) ambayo yamekwishafanyika katika Katiba iliyopo yamekuwa ni viraka ambavyo vimeshindwa kukidhi matarajio ya wadau (wananchi) kwa kuwa hayakuzingatia maoni yao kupitia Tume za Majaji Nyalali na Kisanga.

Mheshimiwa Spika, muundo na utekelezaji wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozaa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umekuwa ukilalamikiwa mara kwa mara na wananchi wa pande zinazounda Muungano huo. Hata hivyo marekebisho yote ambayo yamekwishafanyika hadi sasa kwenye Katiba iliyopo hayajazingatia kabisa kuwapo kwa tatizo hili.

Pamoja na Katiba ya sasa na sheria nyingine za nchi kutungwa na CCM, kwa zaidi ya miaka 40 sasa Serikali ya CCM imekataa kwa makusudi kuongoza kwa kufuata Katiba na Sheria hizo ila tu pale ambapo kufanya hivyo hakuathiri maslahi yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, upinzani tunaamini kuwa kuna haja ya dhati kabisa ya kubadilishwa kwa Katiba ya sasa (si kurekebishiwa), ili pamoja na mambo mengine kuweka msingi mzuri wa uendeshaji wa nchi hapo baadaye, bila kujali ni chama gani cha siasa kitachukua madaraka. Serikali ya Upinzani itahakikisha kuwa katika kipindi kifupi baada ya kuingia madarakani Taifa litakuwa na Katiba mpya ilioandaliwa na wananchi wenyewe kwa kufuata misingi ifuatayo:-

Kutakuwa na mjadala wa kitaifa unaohusisha wadau mbalimbali, kama vile watalamu wa Katiba, Vyama vya Siasa, madhehebu mbalimbali ya dini, wakulima, wafanyakazi, taasisi zisizokuwa za kiserikali, wanafunzi, makundi mbalimbali ya jamii kama walemvu, vijana, wanawake, wazee na kadhalika. Maoni yatakayokusanywa katika mjadala huu ndiyo yatakayokuwa msingi mkuu wa maandalizi ya rasimu ya katiba mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serkali ya wakati huo kwa kutambua umuhimu wa Muungano itachukua hatua madhubuti kuondoa kero zote zinazolalamikiwa katika Muungano wetu hivi sasa. Pamoja na mambo mengine itashawishi kuhakikisha kuwa:-

Katiba mpya inatamka wazi kuwa muundo wa Muungano ni ule ulioainishwa katika madhumuni ya makubaliano ya Muungano ya mwaka 1964 yaani kuwa na Serikali tatu. (*Makofî*)

Utekelezaji wa mambo yote yaliyoongezwa katika orodha ya mambo ya Muungano baada ya makubaliano ya awali ya mwaka 1964 yaliyounda Muungnao, unasitishwa mpaka ufanyike mjadala mpya wa kina juu ya mambo hayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, utawala wa sheria ni kuendesha mambo kwa kuheshimu, kulinda na kufuata Katiba na Sheria nyingine za nchi. Wananchi wana haki ya kuishi kwa amani katika mazingira ambayo haki zao zinalindwa. Jukumu la Serikali ni kuhakikisha kuwa haki hizo zipo na zinalindwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna mkakati wa kuimarisha tuliyoyaeleza hapo juu kwani tunaamini juu ya umuhimu wa kuwepo kwa sheria muafaka katika kuongoza maendeleo na ustawi wa jamii yoyote ile. Ni kutokana na imani hii ndiyo maana nia yetu ni kujenga Taifa lililozindukana, lenye kujituma, *lenye kuheshimu usawa wa watu na linaloheshimu utawala mzuri wa sheria.* (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya upinzani itachukua hatua zifuatazo ili kulifanikisha hili:-

Kwanza itafuta mara moja sheria zote za kikandamizaji. (*Makofî*)

Pili, itahakikisha kuwa Serikali inaongozwa na Katiba na Sheria katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku na siyo matamanio binafsi ya viongozi wake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ili mahakama ziweze kutimiza kikamilifu majukumu yake ya kutafsiri sheria na kutoa maamuzi ya haki, ni lazima ziwe huru kikamilifu. Aidha, ili mahakama ziwe huru kikamilifu ni lazima kubadili utaratibu wa kuwapata majaji na watendaji wengine wakuu wa Idara ya Mahakama, pamoja na kuhakikisha kuwa Idara ya Mahakama inatengewa fedha za kutosha kujiendesha kulingana na mahitaji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mahakama yetu ilianzisha utaratibu unaoitwa *alternative Dispute Resolution (ADR)* na *individual calendar*. Utaratibu huu tunadhani ni mzuri kwani ulikuwa na lengo zuri sana kiutendaji. Sasa tunamwomba Mheshimiwa Waziri atupe takwimu kiutendaji ni kesi ngapi zimepatiwa mwafaka chini ya utaratibu wa *ADR*. Kwa maana nyingine tathmini ya mfumo huo.

Aidha, mfumo wa *individual calendar* ulikuwa na lengo zuri kwani ulikuwa na lengo la kuongeza uwajibikaji kwa mahakimu na majaji kitu ambacho kingepunguza dhana ya rushwa katika Idara hii muhimu na kupunguza msongamano wa watu wenye kesi za jinai mahabusu.

Aidha ungetumika kama chombo cha kuwafanya *evaluation* mahakimu na majaji. Kambi ya upinzani inamwomba Waziri atupe takwimu mfumo huu umeisaidia vipi taasisi

nzima ya mahakama katika kutekeleza majukumu yake? Na ni nani anawajibika katika kufanya tathmini ya kazi ya majaji kwa kutilia maanani kuwa kwa sasa kuna kesi nyingi mno za madai pamoja na jinai kitu kinacholeta usumbufu kwa washitakiwa na kuibua hisia za kuwepo kwa rushwa kwenye taasisi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Idara ya Mahakama iliunda Mahakama maalum kwa ajili ya ardhi na biashara, kitu ambacho bado tuna wasiwasi nacho ni kuhusu kasi ya usikilizaji na umalizaji wa mashauri yaliyo katika mahakama hizo. Tunamwomba Waziri alieleze Bunge na wananchi tathmini ambayo mpaka sasa imeishafanyika kuhusu utendaji wa vitengo hivyo kama kweli vimekidhi matakwa ya uanzishwaji wake au la? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna jambo ambalo linatusikitisha sana, kwani toka kuanzishwa kwa Mahakama ya ardhi haijapatiwa jengo lake badala yake bado inapangisha jengo kwa shughuli nzima za kimahakama. Sasa kama Serikali inauza nyumba inashindwa nini kuliangalia suala hili la mahakama ya ardhi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mahakama ni mhimili mmoja wapo kama ilivyo Serikali na Bunge. Hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na mwakilishi wa Mahakama Bungeni kwa Mwanasheria Mkuu ye ye anakuwa upande wa Serikali na sio mwakilishi wa mahakama, tunamuomba Waziri aliangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukisikia hapa kuwa Serikali inaimarisha ukaguzi kwenye Mahakama za Mwanzo, Wilaya, Mikoa na Mahakama Kuu kwa lengo la kudhibiti na kuinua utendaji kwa watumishi wake. Lakini ukweli ni kuwa ukaguzi hauwezi kuwa na maana kama idadi ya watumishi hasa walioko kwenye *Surbordinate Courts* hasa za Dar es Salaam ni wengi kupita kiasi wakati mikoani watumishi ni wachache. Hili linatia ushawishi wa vitendo vya rushwa na ujisadi kwa kuwa watumishi ni wengi mno. Hapa kuna kitu kinachoitwa *mis-use of manpower*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, upinzani upatapo ridhaa *inshallah* Serikali itaifanya Idara ya Mahakama marekebisho ya msingi ambayo pamoja na mambo mengine:-

Kwanza, yatalenga kuihakiishia Idara ya Mahakama uhuru wa kutosha katika kuendesha mashauri na kutoa maamuzi. Ili suala hili liwe wazi na lisilo na utata wowote, itahakikisha kuwa inatoa ushawishi Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano itamke wazi kuwa Mahakama ndio taasisi yenyenye uamuzi na usemi wa mwisho juu ya suala lolote la kisheria na kuwa itakuwa ni ukiukwaji wa katiba kwa serikali kuvunja agizo, amri, au hukumu yoyote ambayo imeshapitishwa na mahakama. (*Makofi*)

Pili, Serikali hiyo itahakikisha kuwa inatoa ushawishi Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano itamke wazi kuwa uteuzi wa majaji wote (ikiwa ni pamoja na jaji mkuu) na wasajili wa Mahakama Kuu na ile ya rufani utafanywa na Rais kwa kutumia mapendekezo ya Tume ya Ajira ya Majaji na kisha kuthibitishwa na Bunge. (*Makofi*)

Tatu, itaboresha maslahi ya watendaji wa Idara ya Mahakama kwa ujumla ili kufifisha vitendo vya rushwa na ujisadi. (*Makofi*)

Nne, itaimarisha Idara ya Mahakama kwa vitendea kazi na watumishi wa kutosha wenyewe utaalamu na ujuzi unaohitajika ili kuondoa matatizo ya kiutendaji.

Tano, itafanya marekebisho ya sheria ili makosa madogo madogo yasiwe na hukumu za vifungo na badala yake yawe yanalipiwa faini tu au kufanya kazi yoyote ya maendeleo itakayoamuliwa na mahakama iwapo mtuhumiwa atakuwa hana faini ya kulipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, chini ya utawala wa Serikali hii haki nyingi za msingi zimezorota kwa kiasi kikubwa, baadhi ya hizo ni pamoa na:-

Haki ya uwananchi na ukazi. Watu wamekuwa wakinyimwa haki hii kwa visingizio mbalimbali. Operesheni vijiji kwenye miaka ya 1970, kuchomwa moto kwa nyumba na mashamba ya wananchi kule Nzasa mkoani Pwani na Serengeti mkoani Mara katika miaka ya hivi karibuni na shughuli za uvuvi kuzuiliwa katika sehemu kubwa ya kisiwa cha Mafia ni kielelezo halisi cha hali hii.

Haki ya ajira. Chini ya Serikali hii ajira haihesabiwi kuwa ni haki ya msingi. Serikali imekuwa ikishirikiana na waajiri mbalimbali kupunguza wafanyakazi na kibaya zaidi kudhulumu kiasi cha mafao ambacho wanaopunguzwa wanastahiki kulipwa. Dhuluma hii imekuwa ikiwapa wakati mgumu wanaopunguzwa kuweza kutumia mafao yao kama msingi wa kujiajiri. Migogoro iliyodumu kwa muda mrefu sasa kati ya wafanyakazi na waajiri katika mashirika kama *TTCL* na *NBC* ni kielelezo halisi cha hali hii. Wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika mwaka 1977 wamedhulumiwa mafao yao wakati wenzao Kenya na Uganda walilipwa miaka ya 1980. (*Makofi*)

Haki ya kukusanyika kwa nia ya kuonyesha kutoridhishwa na jambo lolote lile. Chini ya utawala wa Serikali hii haki hii inadhibitiwa na matashi binafsi ya viongozi wa jeshi la polisi.

Haki ya wananchi kuunda na kuijunga katika jumuia zao za kiraia. Chini ya utawala wa Serikali hii haki hii inadhibitiwa na matashi binafsi ya msajili wa jumuia za kiraia katika Wizara ya Mambo ya Ndani.

Haki ya kushiriki katika siasa. Chini ya utawala wa Serikali hii haki hii imetengwa kwa ajili ya wanachama wa vyama vyaa siasa pekee. Lakini baya zaidi ni kuwa hata hao wanachama wa vyama vyaa siasa vyaa mageuzi, hususan vile vidogo wamekuwa wakikabiliwa na tishio la kudumu la kufutiwa vyama vyao na msajili wa vyama kwa visingizio mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, moja ya malengo makuu ya upinzani ni kuleta utawala wa kidemokrasia unaoheshimu na kulinda haki za binadamu katika uhalisi wake. Kwa sababu hii, Serikali hatua zifuatazo ili kutimiza azma hii.

Itahakikisha kuwa inatoa ushawishi kwamba katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iwe na kipengele cha Tume Huru ya Haki za Binadamu na kwamba:-

Tume iwe na jukumu la kuchunguza ukiukwaji wa maadili ya haki za binadamu na kuchuua hatua zifaazo ikiwa ni pamoja na kurudisha haki hizo kwa walionyimwa na kuwafikisha mahakamani wale wote watakaoonekana kuwa na makosa ya uvunjaji wa haki za binadamu.

Tume iwe na haki ya kuwaita na kuwahoji watuhumiwa wa uvunjifu wa haki za binadamu, bila kuomba kibali kwa mtu au Taasisi yoyote, ikiwa ushahidi ulioko mbele yake utaonyesha kwamba ni muhimu kufanya hivyo au kuombwa kufanya hivyo na mwathirika au mwakilishi wa mwathirika.

Tume iwe huru kwa maana halisi ya neno huru bila kuwa na mfungamano wowote wa kisiasa na kwamba wajumbe wake watateuliwa na Rais kwa kutumia mapendekezo ya Tume ya Ajira ya Majaji na kisha kuthibitishwa na Bunge.

Tume itakuwa madarakani kwa muda wa miaka mitano na baada ya hapo uteuzi mpya utafanywa.

Mheshimiwa Spika, itahakikisha kuwa vyombo vya dola havitumiwi na wanasiwa au maafisa wa vyombo hivyo kushambulia wananchi wanaoandamana au kugoma kwa njia za zamani. Hili litaokoa maisha ya wananchi wengi amba wamekuwa wakiuwawa na vyombo vya dola bila sababu za msingi.

Itahakikisha inatoa ushawishi kuwa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itamke wazi kuwa wananchi watakuwa na haki ya kulalamikia kwa njia mbalimbali za amani kama maandamano, mikusanyiko, mikutano na migomo.

Itahakikisha kuwa mwananchi yejote, akiwa mwenyewe au kwenye kikundi, ana na haki ya kikatiba ya kuifungulia Serikali mashtaka bila kuomba idhini au kibal cha mtu yejote.

Itahakikisha inatoa ushawishi kuwa Katiba mpya itamke bayana kuwa Watanzania wote, bila kujali kuwa ni wanachama wa vyama vya siasa au la, wanakuwa na haki ya kushiriki kikamilifu katika masuala yote yanayogusa siasa katika nchi yetu na hasa ile ya kuomba kuchaguliwa katika nafasi ya kisiasa bila kupitia chama cha siasa. (*Makofii*)

Itahakikisha inatoa ushawishi kuwa Katiba mpya iezeze bayana kuwa ubaguzi wa aina yoyote ule uwe wa rangi, kabilia, dini, jinsia au hali ya kiuchumi, umbile la mtu na kadhalika katika sehemu za kazi, sehemu za starehe na katika vikundi au mikusanyiko ya aina yoyote ile ambayo ni ya kijamii, itakuwa ni kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano na kwa hivyo wakosaji itabidi wachukuliwe hatua kali za kisheria. (*Makofii*)

Itahakikisha inatoa ushawishi kuwa Katiba mpya ileze wazi kuwa mafunzo ya haki za binadamu ni lazima yawe sehemu ya mitaala ya somo la Uraia mashulenii katika ngazi za elimu ya msingi na sekondari ili kuhakikisha vijana wanakuwa katika hali ya kuelewa haki zao na za watu wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapambano dhidi ya rushwa, rushwa siyo tu kuwa ni adui wa haki, lakini pia ni adui mkubwa wa maendeleo. Rushwa ni saratani inayoua uchumi na kuwanyima wananchi haki maisha na maendeleo, kwa kumbukumbu nzuri wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani mwaka 1995 aliahidi kupambana na rushwa na aliwaeleza Watanzania kuwa kuna vigogo wa rushwa. Lakini cha kusikitisha ni kuwa mpaka sasa ni kigogo mmoja tu aliyetuhumiwa na kuffikishwa kwenye Sheria na bahati mbaya au nzuri kigogo huyo inaonyesha kuwa ilikuwa ni chuki binafsi na wale waliomtuhumu. Sisi tunachojiuliza kuwa ni kweli wale vigogo aliowasema Rais mwaka 1995 wameyeyuka hivi hivi au wamejibadilisha na kuwa wengine kabisa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi tunaamini kabisa kuwa tabia ya mtu hasa akishakuwa mtu mzima haiwezi kubadilika, kinachofanyika ni kuificha tu lakini ataendelea pindi mwanya utakapotokea. Kwa kipindi chote cha utawala wa Serikali hii tumeshuhudia yafuatayo:-

Serikali inapoteza mabilioni ya kodi ambazo hazilipwi na waagizaji wa bidhaa, matengenezo ya barabara na miundombinu mingine ni hafifu japo kuharaka inayotajwa ni kubwa dawa zilizomaliza muda wake wa kutumika zinaingizwa nchini, mitihani inavuja na kwa hivyo haipimi uwezo wanafunzi wetu, mabilioni ya fedha za walipa kodi yanafujwa kila mwaka kwa matumizi hewa, mamia ya Watanzania wanafungwa jela kila siku kutokana na kushindwa kununua haki yao mahakamani, mashirika ya umma yameuzwa kwa bei poa, mali ya asili ikiwa ni pamoja na madini yenye thamani ya mabilioni ya shilingi hutoroshewa nje ya nchi kutokana na kukabidhi mali hizo kwa wageni kwa bei poa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa chanzo kikubwa cha rushwa ni ukiritimba wa madaraka, mishahara midogo ya watendaji Serikalini, maamuzi yasiyofuata taratibu zinazoleleweka na kutowajibishwa kwa washiriki katika vitendo vya rushwa, vita dhidi ya rushwa inatafanikiwa ikiwa ukiritimba wa madaraka utaondolewa, maamuzi ya Serikali yatafuata taratibu zilizowazi na zinazoleleweka na kuwaadabisha wanaoshiriki katika rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kupambana na rushwa ni lazima tujenge mazingira ambayo yatatuahakikishia kuwa mapapa na masangara ya rushwa yanashughulikiwa kwanza kabla ya kuwashughulikia dagaa. Ili kukabiliana na ufisadi katika masuala yake yote upinzani utachukua hatua zifuatazo:-

Kuiongezea nguvu Taasisi ya Kupambana na Rushwa, yatafanyika marekebisho ya kisheria ili taasisi ya kuzuia rushwa iwajibike kwa Bunge badala ya Serikali. Mabadiliko haya yatalenga katika kuipa kinga dhidi ya hujuma inayoweza kufanyiwa na

Serikali kuvuruga shughuli zake za kiuchunguzi pale shughuli hizo zinapoonekana kuwalenga baadhi ya maofisa wa Serikali au waliokaribu na maafisa wa chama kinachotawala. Aidha, marekebisho haya yatalenga kuipa taasisi hii uwezo wa kisheria wa kumwita na kumhoji mtu yejote atakayetuhumiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa bila wadhifa au mhusika na pia kumfungilia mashtaka pale ushahidi dhidi yake utakapomwelemea.

Kuhakiki mikataba ya ubinafsishaji na uwekezaji, yatafanyika marekebisho ya kisheria yatakayohitajika ili kuruhusu uhakiki wa kazi za Tume ya Rais ya kubinafsisha mashirika ya umma na zile za Kituo cha Uwekezaji chini ya mabadiliko haya, Mikataba yote ya ubinafsishaji wa Shirika lolote la umma unaokusudiwa kufanywa na Tume hii utahakikiwa ili kubaini uhalali wa bei jinsi haki za wafanyakazi husika zilivyoshughulikiwa na mazingira ya rushwa.

Aidha, mazingira ya mikataba yote iliyofikiwa au kushindikana kuafikiwa baina ya *TIC* na wawekezaji mbalimbali itahakikiwa ili kubaini kuzingatiwa kwa kanuni, mikataba yote itakayobainika kuwa na kasoro za makusudi itafutwa na hatua muafaka za kisheria kuchukuliwa dhidi ya wahusika.

Itateua Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai wenye usongo dhidi ya rushwa.

Kuwatangaza wanaotiwa hatiani kwa vitendo vya rushwa. Wahalifu wote wa vitendo vya rushwa wanaotiwa hatiani watatangazwa hadharani kuititia vyombo vya habari vya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya muundo wa utendaji Serikalini, mabadiliko ya muundo na utendaji Serikalini kama yalivyoolezewa katika sehemu nyingine za ilani hii yamelenga katika kuondosha ukiritimba wa madaraka na kuweka utaratibu wa wazi zaidi wa kiutendaji. Mabadiliko haya yatakuwa ni silaha muhimu kabisa katika kubomoa mazingira ya rushwa.

Kuboresha maslahi ya wafanyakazi, marekebisho ya mishahara ya watumishi wa Serikali yatakayolenga katika kutoa mishahara mizuri na ya haki utasaidia kwa kiwango cha kuridhisha kufifisha rushwa katika ngazi ya chini na nyakati za utendaji Serikalini.

Kuunda Baraza la Ushauri dhidi ya ruhswa, Baraza huru la ushauri dhidi ya rushwa litakalo jumuisha viongozi kutoka katika madhehebu mbalimbali ya dini, vyombo vya habari na jumuiya mbalimbali za wananchi hususani zile zilioko kwenye mapambano dhidi ya rushwa litaundwa ili kuishauri Serikali katika mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa hayo, maoni ya Kambi ya Upinzani sina budi kusema nawashukuru Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, anawashukuru wapiga kura wake wa Jimbo la Karatu na anaomba ushirikiano nao mkubwa uendelee na kwamba anawaomba wakumbuke ya nyuma ushindi ni ule ule uliotumika miaka ya nyuma na pia mwaka huu utumike tarehe 30 Oktoba, 2005. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Sasa tunaingia kwenye mjadala wa jumla, ninao wasemaji wanne wafuataao, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Jackson Makwetta. Tutakapomaliza hao tutaahirisha mpaka saa kumi na moja ili Waziri apate nafasi ya kupitia michango ya maandishi kwa sababu naambiwa amepata minge sana.

MHE. KHALID S. SURU: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kushukuru kupata nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba. Kwa mujibu wa mawazo yangu sina kigugumizi chochote na Wizara hii kwa maana naunga mkono moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo niikumbushe tu Serikali hasa sifa za utawala bora ambazo mimi nazona, sifa za utawala bora iwapo hizo sifa za hayo mambo hayaonekani basi hata utawala bora wenyewe utakuwa mashakani. Kwa hiyo, nianze na sifa ya kwanza ambayo ni ile haki ya usawa baina ya binadamu. Katika hilo na maswali matatu ambayo Waziri baadaye atajibu.

- (i) Ni kwamba watu wote ni sawa mbele ya Sheria?
- (ii) Wanayo haki sawa?
- (iii) Hakuna ubaguzi wowote?

Mheshimiwa Spika, lakini katika utafiti wangu mimi ambao nimekuwa nikiufanya huku katika hali halisi nimegundua kwamba kiutekelezaji hatujafikia haki ya usawa unaotakiwa kwa mujibu wa Katiba. Kwa hiyo, sababu zifuatazo zinanipelekea huko, sababu ya kwanza uchache wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Wilaya utathiri vibaya utoaji wa haki kwa wananchi kwa uchache ule, kwa sababu uchache huo unasababisha Halmashauri kuchelewa na haki kuchelewa na kama haki ikicheleweshwa sana kwa kweli lazima kuna na matatizo. Kwa hiyo, sababu ya kwanza ni hiyo lazima tuajiri Mahakimu wa kutosha ili haki hizi ziweze kutolewa vizuri.

Lakini pia jambo la pili udogo wa posho za wazee wa Mahakama za Mwanzo lakini pia kucheleweshwa nako kunaathiri sana utoaji wa haki katika Mahakama zetu mbalimbali. Sasa ukimcheleweshea posho maana yake lazima kutakuwa na mazingira zingira hayo ya rushwa na kadhalika. Kwa hiyo, utoaji wa haki unakuwa wa mashaka, kwa hiyo, naiomba Serikali basi, nilikuwa naangalia hapa hata mahakimu wanaoajiriwa ni kama 40 tu, 40 hawatoshi kitu.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni mishahara midogo ya watoa haki yaani Mahakimu ambao ndio watoaji wa haki mishahara yao ni midogo na kwa sababu hiyo wakati fulani wanachangia hata kula milungula kwa maana ya rushwa. Kwa hiyo, katika maeneo hayo katika hali hiyo unategemea nini, kwa hiyo, je, haki itakuwa? Wapeni

Mahakimu mishahara ya kutosha na wale wote wanaotoa haki ili waweze kutusaidia kusimamia utawala bora na waweze kutoa haki vizuri kwa wananchi.

Jambo la nne Mahakama zenyewe ni chache sana, ni chache mimi nakumbuka kule Kondo tangu zimejengwa wakati wa ukoloni wa Mjerumani na zile zingine za ukoloni wa Mwingereza, ni hizo hizo hata kukarabatiwa hazikarabatiwi. Sasa uchache wa Mahakama nao unasababisha wananchi wetu washindwe kusafiri masafa marefu kufuata haki zao.

Kwa hiyo, wanaacha tu hivyo hivyo, kwa hiyo, tunaomba sana Mahakama zijengwe angalau kila Kata kuwe na Mahakama kwa sababu Wizara hii ni nyeti sana, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ndio inatakiwa kuwa mfano wa kutoa haki, sasa hawawezi kutoa haki kama kuna upungufu mkubwa kama huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo la tano, ni walalamikaji, wale wanaolalamika kupeleka mashauri Mahakama hulazimika kuchangia mambo yafuatayo, sasa kama wanalazimika kuchangia mambo yafuatayo sijui kama haki inaweza kutolewa vizuri.

(i) Kuwalisha chakula watuhumia wanaowalamikia, wakimlalamikia mtuhumiwa akikamatwa yule aliyelalamika ndiye anamlisha na gharama zingine mbalimbali. Sasa wakati fulani wananchi wanaogopa hata kulalamika kwa sababu wataingia katika gharama. Kwa hiyo tunaomba Serikali itatue tatizo hili, mtu akifkishwa Serikalini, Serikali imlishe sio yule aliyelalamika.

(ii) Kutoa fedha ama chakula cha walini wanaolinda wale watuhumiwa, wale walalamikaji huambiwa kwamba kwa sababu hakuna chakula hapa basi utele chakula kwa mtuhumiwa wako. Hili nalo liondolewe, lisipoondolewa hakuna utoaji wa haki, lakini pia kulipa gharama za mgambo kumpeleka Wilayani. Mahakama ikiamuru au chombo chochote kikiamuru apelekwe Wilayani lazima huyu aliyelalamika ndiye anayegharimu gharama zote za nauli na chakula na vitu vingine. Kwa hiyo, tutasababisha wananchi washindwe kudai haki zao kwa sababu ya kubanwa na gharama hizo.

Mheshimiwa Spika, sasa katika hilo sasa je, hapo utawala bora utaonekana? Je, kuna haki ya usawa kama tukiendelea na suala hilo?

Mheshimiwa Spika, jambo la sita, mahakimu kutumia pikipiki zao tena sio zao, ni za kukodi ili kwenda katika Mahakama zile zingine ambazo wamepangiwa, wanakodi kwa pesa zao mfukoni. Hivi unategemea nini na Serikali hairudishi, sasa tafuta tu mpaka pesa zake zirudi.

Kwa hiyo, tunaomba Serikali itatue tatizo hili iwakopeshe Mahakimu pikipiki wapewe wote, tumejenga uchumi, hali ni nzuri hilo ni eneo nyeti sana tuwape Mahakimu wote pikipiki wafanye kazi vizuri kwa uadilifu, lakini kama hawana vyombo vyakusafiria, uhadilifu unapungua.

Mheshimiwa Spika, jambo la saba, haki ya kuandika rufaa ya hukumu ni ya mrufani mwenyewe, lakini wananchi wetu wanyonge wengi wanashindwa kuandika kwa sababu hukumu wanazopewa zimeandikwa kwa lugha ambayo hawaelewi ya kiingereza. Hukumu zao wapewe kwa Kiswahili wasome waandike wenyewe rufani, wanababaika sana wakati fulani ni haki pengine ingemrudia lakini wanashindwa. Kwa hiyo, tunaomba Wizara hii itengeneze utaratibu, wananchi waweze kuwa na urahisishaji kabisa wakuomba rufaa wasome hukumu ikoje wapi anaona kadhulumiwa ili waweze kuandika rufaa zao. Kwa hiyo, natoa wito kwa Serikali itoe hukumu kwa Kiswahili, ili wananchi wetu, maana wananchi wetu waliowengi hawajui hii lugha ya kiingereza.

Jambo la nane, kuna hizi bodi za mahakama, sijui zina nafasi ipi katika kulinda raia dhidi ya maonevu ya dhahiri pengine wanayofanyiwa na mahakimu na kadhalika. Maana sioni makali ya hizi bodi ni kama zinakaa tu lakini sioni mabadiliko, sioni hali halisi. Kwa hiyo tunaomba majukumu hayo yaainishwe na bodi hizi zifanye kazi zionekane kweli kweli, maana sioni hata kama mahakimu wanaogopa hizi bodi. Tunataka waogope kwamba nikifikishwa kwenye bodi kuna tatizo kwa hiyo tunaomba sana Serikali iweke mkakati wa kuonyesha makali ya bodi hizi za mahakama ili zisimamie haki vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho Mahakama za Mwanzo zifuatazo kule Kondo ni chakavu sana tena juzi juzi tu wiki iliyopita ulinipa ruhusa nilikuwa kule nimeziona ni chakavu sana, zinahitaji kukarabatiwa. Mahakama ya Kondo Mjini hiyo imekuwa ni gofu kabisa ni mbovu, mipasuko mingi kabisa katika kuta, tunaomba Serikali ikarabati lakini pia mahakama ya pale ni mbaya sana ni mbovu sana, kule Busi ni mbaya ni mbovu sana na kule Kolo ni mbaya sana ni mbovu sana na kule Bereku. Naomba Mahakama hizi zikarabatiwe ndio zinaleta hata motisha kwa Mahakimu kufanya kazi, ukiwatembelea mahakamu sehemu wanakofanya kazi utawahurumia kabisa.

Mheshimiwa Spika, hizo nilizotaja ni tangu zijengwe na mkoloni mpaka sasa bado hata ukarabati hakuna. Kwa hiyo, tunaomba sana, sasa nakumbusha tu sifa zingine ambazo zinatakiwa zifanyiwe kazi na kuona kwamba wananchi wanafaidika nazo ni ile haki ya kuishi, haki ya uhuru wa mawazo na haki ya kufanya kazi, haki hizo lazima zilindwe ili wananchi wajionewako katika nchi yao ambayo ni huru.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nakushukuru sana kwa kunipa naunga mkono kabisa hoja hii moja kwa moja. (*Makofi*)

MHE. PHILEMON NDESAMBURO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipendelea, mimi nasema umenipendelea, kwa sababu nimekwishazungumza hapa Bungeni na kwa kweli, kambi ya upinzani kwa ujumla inakushukuru na tunasema kwa niaba ya kambi ya upinzani umetenda haki katika Bunge hili kwa kipindi cha miaka mitano ambayo umekuwa ndiye Spika, umekuwa ndio muhimili wa Katiba ya nchi hii na tungependa wengine wafuate hivyo wale wanaofanya kazi chini, hukujali u-CCM wako bali umejali kazi yako na ukatimiza wajibu wako wa Spika Bunge na tunakushukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa sitaki kuzungumza, nilikwisha anza kuandika tatizo langu ni Moshi. Tatizo langu ni Mkurugenzi wa Moshi Vijijini anaitwa Bwana Kitimbo na Mheshimiwa Waziri ninavyozungumza hapa mimi ningekuomba uunde timu ndogo iende ikachunguze lakini ningeomba diwani wa Kiboriloni anaitwa Vicent Rimoi, pamoja na Mwenyekiti wa Mtaa wa Mnazi awepo ambaye ataonyesha ukweli wa mipaka ya kijiji cha Moshi Vijijini na Kiboriloni nayasema haya kwa sababu yanatia uchungu katika uchaguzi wa Vijiji na Vitongoji tuliofanya mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, tulirudia uchaguzi katika Kijiji kile mara tatu, kisa kwa sababu CHADEMA ilikuwa inashinda lakini CCM ikaambiwa ni lazima ishinde. Ukafutwa uchaguzi mara tatu ili CCM iwe ni lazima ishinde na hii ni kuvunja Katiba na huyu Bwana Katimbo anajua anavunja Katiba, mwishoni baada ya kuona ujanja wa kushinda ni kuhakikisha mtaa wa Mnazi unakuwa ni sehemu ya Moshi Vijijini na mawe yapo yanaonyesha wazi mpaka uko wapi, na alivunja kwa makusudi na akabeba watu na magari akawatoa katika Kiboriloni ambayo ni Manispaa akawapeleka kule kwenye Kijiji cha Moshi Vijijini cha Kikarara wakenda kupiga kura ili washinde, na ushahidi kamili mpaka Mwenyekiti wa Moshi vijijini Kikarara anakaa Kiboliloni mtaa wa Mnazi.

Sasa uvunjaji wa Katiba wazi wazi namna hii na mtu huyu anaonekana anaendelea kukaa madarakani wananchi wanachukia mwisho wake mtakuja kukuta watu wanampiga mtu. Sisi tunataliza, na kwambia hata katika kuandikisha majina ya wapiga kura zaidi ya watu 400 wamechukuliwa katika Mtaa wa Mnazi wakaenda kuandikishwa Moshi Vijijini makusudi ni kunihujumu Ndesamburo nisishinde uchaguzi wa Moshi Mjini, lakini wapi hawawezi. Mimi naomba kwa sababu majina ya wapigakura yako kwenye *register* na yanajulikana hiyo timu tu nakuomba sana Mheshimiwa Waziri kabla ya uchaguzi haujafanyika hebu tuma mtu akaangalie hawa watu halafu usome haya majina uone matatizo ya utawala bora unavyotumika vibaya na ningeona kama natumia mambo hayo kama ni mtu ambaye hana akili kweli ningeshangaa, na sababu ya kufanya yote haya anaambiwa Mama Mkapa, mke wa Rais hawezি kutawaliwa na Chama cha Upinzani ni lazima Kijiji kile kichukuliwe na CCM. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli baada ya kushinda walichinja ng'ombe wanne wakala. Walichinja ng'ombe wanne wakafanya sikukuu wakala, maana yake ni kuwashonga wale watu waliokuja kupiga kura wakahongwa, wakala wakabariki, lakini haki bado haijatendeka na Katiba imevunjwa. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Spika, je, Waziri unaonaje hili ni sawa? Tutendeane haki tu hii nchi ni yetu wote hakuna cha upinzani katika nchi hii, sisi wote ni Watanzania na tunashirikiana, huku Bungeni mbona hatunyanyasani, mbona tunakaa vizuri, kwa nini huko chini wanafanya mambo ambayo ni ya kihuni?

Mheshimiwa Spika, tunaomba utawala bora utiririke mpaka ufile mwisho mpaka kwa Mwenyekiti wa Kijiji, kwanza makosa makubwa tunafanya Wenyeviti wa Vijiji wale na wa mitaa kuwaweka kwenye vyama ni dhambi kubwa kwa sababu hawaangalii maslahi ya wananchi kwa ujumla wangetakiwa wasiwe na chama ndiyo wangewajibika vizuri na ndiyo wangefanya kazi vizuri kwa wananchi. Kwa sababu wananchi

watanzania milioni 36 walio na vyama hawafiki hata milioni 4. Kwa hiyo, wale Wenye viti walitakiwa wachaguliwe na watu ambao ni *free* na Mheshimiwa Waziri, mimi naomba uliangalie hilo na kama linaweza kuwekwa kwenye mchanganuo wowote wa kufanya mabadiliko katika Katiba lingefanyika. Kwa kweli wale Wenye viti wasingetakiwa wawe kwenye *partisan* kwenye *party no*, wangekuwa ni watu ambao wanaangalia watu wote kwa ujumla na haki ingekuwa inatendeka. Haya yote ninayoungumza hapa leo yasingezungumzwa kama haki ingekuwa inatendeka na kama Katiba ya nchi ambayo ndiyo Sheria mama kama ingekuwa inafuatwa kwa kweli hatungefika hapa tulipofika.

Mheshimiwa Waziri, mimi sio mtaalam wa Sheria na wengi wetu sio wataalam haya mambo ya Sheria uliyoyazungumza ya Katiba ni mambo ya msingi na ni mambo ambayo yanataka watu wenyе bongo sisi tumebababisha babaisha lakini nasifia hotuba yako ni nzuri, mambo ya msingi umeyazungumza, lakini matatizo ni kwamba haya mambo ya msingi ambayo ni mazuri ya kuweza kuleta ustaarabu na heshima kwenye nchi yetu hayasambai yakaenda chini. Yanakuwa huku huku kwenye nyumba au yakienda kwenye makabati ya maofisi yanabaki kule kule ambapo mambo haya yalitakiwa yaende mpaka kwa wakurugenzi wasikie na huyu Mkurugenzi nadhani amenisikia maana yake hata Mkurugezi wa Moshi Mjini ana matatizo kwa nini anaachia Jimbo lake lichukuliwe, ni sehemu yake ilikuwa inachukuliwa.

Sasa hivi watu wa Moshi Vijijini wanadai kwa kuwa walipiga kura kule hata Shule ya Sekondari iliyoko Kiboriloni wanasema sasa ni yao, *dispensary* iliyoko Kiboriloni wanasema ni yao, *primary schools* tulizokuwa nazo wanasema sasa ni zao. Sasa tumeanza utata mbaya kwa ajaili ya mtu mmoja kutokutaka kutenda haki, kutoka kutaka kuheshimu Katiba ya nchi, kwa maslahi yake mwenyewe sijui alihongwa nini, kwa nini asifuate Katiba kwa nini afanye hivi? Naomba Mheshimiwa Waziri wakati utakapokuwa unajibu hoja, mimi sina mengi ya kusema zaidi ya hayo, mimi nilikuwa naomba tu hilo nalia kwa sababu njama za kunihujumu katika uchaguzi zimejengwa, nilizungumza hapa nilisema kule *State lodge* wanavyonizua walivyochukua watu 153 wakawahamisha, sasa nimekwambia kuna watu 400 wamehamishwa tena wamembwa waende wakapige kura vijijini na ni watu wa mjini wanalipa *property tax*, wanafanya kila kitu ukenda majina utayakuta ni wakazi wa Mnazi.

Mheshimiwa Spika nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii nakueleza kinachonumiza rohoni mwangu, ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningependa nikushukuru kwa heshima hii uliyonipa ili niseme kabla ya Mheshimiwa George Lubuleje, kwa sababu huyu ni mjomba wangu na ni mdogo wangu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuunga mkono hoja ya Wizara hii lakini kabla ya yote ningependa nijikite kwenye ile dira ya Wizara ambayo inasema haki kwa wote na kwa wakati. Mimi labda niseme kwamba niko kwenye Kamati ya Ulinzi na

Usalama na kwa hiyo, kutokana na kazi hiyo najua baadhi ya mambo ambayo yanaihusu Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ili kudumisha utawala bora ni lazima kuwe na wasimamizi wa Sheria na uchambuzi unaonyesha kwamba Wizara hii ina wanasheria wale wa ngazi za juu lakini kwenye ngazi za vijiji au Kata kwa kweli hali ni mbaya sana. Mimi natoka Njombe, Tarafa nzima ya Lupembe haina Hakimu na *nature ina-abhor vaccum*, kwa hiyo kutokana na *vaccum* hii Polisi kule wamechukua nafasi ya Mahakimu na ndiyo wanaojaribu kutafuta au kutoa haki namalamiko ni mengi sana kuna rushwa na dhuruma ya haki. Sasa kwa watu tulioamua kuendesha utawala wa sheria na tunaothamini utawala bora unawezaji kuendesha utawala bora bila Sheria kusimamiwa na Mahakimu. Najua kuna chuo cha Mahakama Lushoto lakini kwa kasi ya kufundisha Mahakimu nadhani hawa ni Mahakimu wa Mwanzo, kwa kasi ile kwa kweli tutachukua muda mrefu sana kukidhi lengo hili la utawala bora. Kwa Njombe ni kama tunaendesha *a stateless society* yaani watu wamekuwa watakatifu kiasi kwamba hawahitaji Mahakimu kwa sababu ndio wanaofanya hivi sasa, ni vijijini, ni wazee pale ndio wanaoshughulikia mambo ya vijijini hakuna Hakimu, ngazi ya Tarafa hakuna Hakimu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ngazi za Wilaya inabidi huyo huyo aende Ludewa, aende Makete arudi Njombe, kama mnavyosema wenyewe hapa kwamba, *justice delayed is justice denied*. Kwenye mahabusu kuna tatizo hilo hilo, haya Magereza yetu yana uwezo wa kuchukua wafungwa au wahalifu si zaidi ya 22,000, lakini hivi sasa wako zaidi ya 44,000 na karibu nusu yao ni watu waliopelekwa kule kwa sababu ya kutuhumiwa, wanakaa miaka mitatu, minne, mitano, bila kusikilizwa na wakati muda unawenza kwenda wakasilizwa baada ya miaka sita au saba. Ukiangalia takwimu anaonekana hana hatia baada ya kukaa mahabusu kwa zaidi ya miaka sita au mitano, unagundua kwamba, hakuwa na kosa.

Mheshimiwa Spika, sasa katika kuzungumzia Utawala Bora katika nchi yetu ni lazima tugutuke tuone uchungu kwamba, mtu anakaa miaka minne, mitano, bila kusikilizwa na baadaye unagundua hana hatia anatoka hivi hivi baada ya mateso yote yale, wengine wanafia Magerezani bila kusikilizwa. Kwa hiyo, nasema katika hili bila kujali tuko upande gani ni vizuri kwa kweli tuwe na *crash program* ya kufundisha Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ili waweze kushughulikia masuala haya. Vinginevyo kuwa na karibu nusu ya mahabusu ambaa hawasilikilizwi au hajasikilizwa kwa zaidi ya miaka miwili, kwa kweli ni jambo linaloathiri misingi ya haki za binadamu.

Kuna mtaalam mmoja alikuwa ameandika kitabu kinasema *basic needs are in danger*, ungeweza ukasema *basic needs* za haki katika nchi hii ziko *in danger* kama tutaendelea na kasi hii ya kutoa watu wanaosimamia haki. Sasa napendekeza kwamba, kutokana na hali hii kuwe na *crash program*, ikiwezekana tutumie vilevile vyuo vingine, ule mtindo kwamba, *the basic people* watatoka Lushoto kwa sababu kuna maadili ya aina yake, nadhani hata hao waliosomea mahali pengine tukatizama maslahi tungeweza kuwaajiri kuliko kuendelea na hali hii iliyopo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo tumeliona kwenye mahabusu vile vile ni kwamba, mahabusu yetu yamejaa kwa sababu hakuna Mahakimu na ukiangalia kwenye kitabu hiki ni kweli kwamba, kwenye ngazi za juu wako wengi sana. Kwa hiyo, hawa Mahakama wa mwanzo hawapo, wako hawa Majaji, wanapandishwa kila siku lakini chini hakuna. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza hilo litazamwe kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Spika, halafu hili suala la Hukumu za Kifo, ni kweli labda tutazame upya tena kwamba, ili mtu anyongwe lazima na Rais aweke saini ile kwamba na yeye anakubali anyongwe. Sasa kwa kuwa Sheria hatujaifuta, bado Mahakimu wanaendelea kuhukumu wanyongwe. Sasa kuna waharifu wengi ambaو wamehukumiwa kunyongwa lakini hii kazi ya kuweka saini kwamba, anyongwe inaonekana ni ngumu na Marais wanaona tabu kufanya kazi hiyo. Idadi ya hawa watu imekuwa kubwa sana, mimi naijua, tuliwahi kutembelea Ukonga kama Kamati, tukakutana na baadhi ya watu waliotoka kwenye maeneo yetu, wakasema mwambie Rais atunyonge hapa mnatutazama nini hapa.

Mheshimiwa Spika, mahali pengine ambapo wako wafungwa wa aina hii hata wale Askari wa Magereza hawapendi kuonana nao, kwa sababu ya kukata tamaa kwamba, wanaweza kufa wakati wowote. Kwa hiyo, maisha yao yanakuwa ni magumu sana na hawa vilevile ni jeshi la wafungwa ambaو hawatakiwi kufanya kazi ila wanakula chakula, tofauti na wale wengine. Zimewahi kuchukuliwa hatua za kupunguza tatizo hili kwa kubadilisha kifungo cha kunyongwa wakapewa kifungo cha maisha. Sasa labda tutazame hili kwamba, Marais wanaogopa kunyonga na Sheria zipo hivi hivi. Siku moja Marehemu Mwalimu Julius K. Nyerere, aliwahi kusema kwamba, alipoweka saini kwa mtu mmoja, alikaa Jumapili anashindwa kula chakula kwa sababu ya uchungu na mawazo yaliyomzonga kwa sababu ameamua mtu anyongwe. Sasa kama ni hivyo, basi tufute tubadili Sheria hii kuliko kuwa na watu waliohukumiwa zaidi ya 500, hawafanyi kazi, hawajui lini watanyongwa na saikolojia yao inakuwa mbaya sana. (*Makofî*)

Tukikiuka misingi ya haki nayo itatukiuka. Raia wa kawaida hawataki hii sentensi inavyosema kwamba, ubadalishe anasema hapana, hata mtu aliyeuawa mtu akiona anarudi tu kijiji watammaliza kule. Kwa hiyo, tuanze kuandaa watu wa kutazama hii sentensi kwa sababu ni *contradiction*, kama utawala wa Sheria si kutii Sheria, sasa unapokuwa hutekelezi Sheria siyo utawala wa Sheria maana hutii, huweki saini kwamba anyongwe, hivi ni utawala wa Sheria huo? Weka saini anyongwe, sasa kama tunaona tabu tubadilishe kusudi hawa badala ya kukaa tu wakafanye kazi. Wafanye kazi na kula kuliko kukaa tu hawajui lini, ni *condemned* lakini wanakaa tu hawajui lini watauawa, kwa nini wakae miaka zaidi ya 20 hawajauawa na hubadilishi sentensi?

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni hili la ugumu wa kumshughulikia Hakimu anapofanya maovu. Katika yale mafiga matatu ya madaraka, sisi Wabunge tunatunga Sheria, halafu kuna *Judiciary* na *State*. Sisi ndio tunaotafuta Serikali kwa watu, kama ni kuwinda sisi ndio tunaoua mnyama, sasa tunapokuwa tumeua mnyama tunagawana sawa na *Judiciary*, *Legislator* na *State*. Sasa hii *Judiciary* wanasesha wakati wa kula lakini madaraka wanaliyopewa na ugumu wa kuwaondoa na uhuru walionao kushughulikia mambo ya nchi hii ni ngumu sana. Kumwondo Hakimu tu wa Mahakama ya Mwanzo akifanya uharifu mpaka umuundie Kamati kwa *DC*, njia ndefu tu. Sasa hawa *small gods*,

ambao tumeunda Serikali watu hawatuelewi ndio wanatuapisha, sasa sijui mahali pengine labda wanaapishwa na wazee wa jadi, sijui.

Lakini kumwondoaa Hakimu aliyefanya maovu kwa kweli ni ngumu, *it is easier to go to heaven than to have a Judge removed from his position*. Ni ngumu mno na wanaendelea kutetea tu na ndio maana anaweza kuwa *reckless*, kule Kenya Rais Mwai Kibaki, alipofanya yale yalizua zogo Dunia nzima, kumwondoaa Hakimu mpaka ukapate kibali na madaraka, Mkuu wa Mkoa na madaraka mpaka sijui nani huko. Hata kwenye mambo haya ya Lushoto kuleta hawa Mahakimu kutoka nje ya hapo nadhani ni ile ile, kwa sababu ni lazima waangalie yaliyoandikwa na kwenda kinyume cha pale ni *to violate the status ambayo ni kinyume cha profession*.

Kwa hiyo, mabadiliko katika eneo hili yanahitajika. Kwa kweli ni vigumu sana na kama tunazungumzia Utawala Bora na mabadiliko katika Dunia, nadhani kwamba, *the biggest timing broke is the Judiciary. We need it, it is necessary*, lakini vilevile tunahitaji kuwa na *Judiciary* yenyeye sura ya maskini wa Tanzania. La sivyo hivi vyombo vitakuwa ni vya kutetea walio na mali na wajanja. Inapokuwa kwamba, haki inanunuliwa hakuna maana, kuna wakati *Patrol* wa Cuba aliwahi kusema kwamba, madaktari na majaji katika nchi za kibepari huwa wanahukumu fedha au kutibu fedha. Wakati katika maskini majaji na madaktari huwa wanashughulikia wenyewe matatizo na wagonjwa kwa maana kwamba, ukitikisa fedha mfukoni, unaona jaji anachangamka, ukitikisa fedha mfukoni unaona daktari anachangamka, kama huna hushughulikiwi, wanatibu pesa wanahukumu pesa na siyo matatizo. Ahsante sana. (*Makofit*)

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja hii ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba. Kwanza, nimpongeze Mwanasheria Mkuu, Katibu Mkuu, Msajili wa Mahakama ya Rufani, pamoja na wataalam wote wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati yangu kufanya kazi nzuri ya kuchambua Bajeti ya Wizara hii, kwa kweli nisingelazimika kusimama, lakini napenda nisisitize tu siyo kurudia rudia ni kusisitiza yale ambayo Kamati yangu imeeleza katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, nimekuwa nikalalamikia Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mpwapwa, lakini sasa jengo hilo linajengwa na hivi sasa limefikia kwenye hatua nzuri, kwa hiyo, naomba niishukuru sana Serikali. Jengo ambalo linatumika sasa ni la Shule ya Msingi ya Mtegeta, sasa Serikali imesikia kilio cha Wananchi wa Mpwapwa, jengo hilo linajengwa. Pili, nashukuru kwa ukarabati wa Mahakama ya Mwanzo Mpwapwa Mjini, wamekarabati vizuri sana. Sasa jengo lile linafanana na hadhi ya Mahakama kuliko hali ilivyokuwa mwanzo.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inafanya kazi kubwa na majukumu makubwa sana, lakini tatizo kubwa bajeti ambayo inatengwa ni kidogo sana, kwa mfano, shilingi bilioni 49.9 ni fedha kidogo ukiangalia na majukumu ya Wizara yenyewe, pamoja na ufinyu wa Bajeti, lakini Bajeti ijayo basi Serikali iongeze Bajeti ya Wizara hii ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la usafiri kwa Mahakimu, mwaka 1993 wakati vikao vyetu vinafanyika *Karimjee Hall, Dar es Salaam*, niliwahi kuuliza swali hili la usafiri kwa Mahakimu. Serikali ilikuwa imetoa ahadi tangu mwaka 1993, kwa hiyo, kila Bajeti, Serikali ina mikakati, ina mipango, lakini Mahakimu ni watumishi kama watumishi wengine. Watumishi wengine kwa nini inakuwa rahisi kupata mikopo isipokuwa Mahakimu tu, ndio kwamba kunakuwa na migogoro?

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naomba kwamba, Bajeti ijayo na mimi nina matarajio ya kurudi, Wananchi wa Jimbo la Mpwapwa watanirudisha tu, kwa sababu nimefanya mambo makubwa sana. Kwa hiyo, tunaomba mwaka 2006 basi tupewe taarifa ni Mahakimu wangapi wamekopeshwa vyombo vya usafiri, pamoja na Mahakama zetu za Wilaya. Mahakama za Wilaya walipata magari madogo aina ya Samurai.

Mheshimiwa Spika, lakini yale magari ni madogo sana, hayafai kabisa kwenye maeneo kama Mpwapwa kule kupanda milima na maeneo mengine. Kwa hiyo, naomba wapate usafiri wa uhakika kwa ajili ya kukagua Mahakama za Mwanzo. Mahakama za Mwanzo bila kukaguliwa itakuwa ni vigumu sana kwa Mahakimu kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusu msongamano wa mahabusu katika Magereza. Mwaka 2004, bahati nzuri Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, tulipata nafasi ya kutembelea baadhi ya Magereza hapa nchini, pamoja na Gereza la Isanga. Tulipata nafasi ya kuzungumza na wafungwa wale ambao wamehukumiwa kunyongwa na bahati nzuri, Kamati imeshatoa maoni kwamba, ni mambo gani Serikali iweze kutekeleza.

Lakini wengi katika Magereza ni mahabusu. Sasa wakati tunachambua Bajeti ya Mheshimiwa Waziri, tulitoa ushauri kwamba, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, basi wakutane na Waziri wa Mambo ya Ndani, ili waone jinsi gani wanaweza kupunguza msongamano wa mahabusu katika Magereza.

Mheshimiwa Spika, kuna makosa mengine mtu ameiba kuku, ameiba labda shilingi 1,000, ameiba kalamu, miezi sita mtu yuko mahabusu upelelezi haujakamilika, ni upelelezi wa aina gani? Mtu kachomwa kisu tayari kesi iko mahakmani inatolewa *PF3* kama *documentary evidence*, lakini unaambiwa ushahidi haujakamilika mtu bado yuko mahabusu muda mrefu tu. Sasa haki za binadamu zinawahusu hata wale, kweli ni wahalifu, lakini unapomuweka mtu mahabusu muda mrefu, kesi ndogo upelelezi haujakamilika. Kwa mfano, kesi za mauaji, nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa Mbunge mwenzangu pale alipokuwa anazungumzi suala la hukumu ya kifo.

Haki za binadamu ziko pande mbili, hakuna mtu anayeruhusiwa kuua mtu mwingine. Kwa hiyo, tuangalie haya mambo mawili, haki za binadamu zinamuhusu kila binadamu. Lakini mtu anachukua kisu anamchoma mwenzake anamuua, sasa akihukumiwa kunyongwa unasema haki za binadamu zimekiukwa. Kwa hiyo, nilikuwa

nashauri tu kwamba, maoni ya Kamati yazingatiwe ili kuona kwamba, haki za binadamu kweli zinazingatiwa kwa hawa watuhumiwa au wafungwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuboresha maslahi ya Mahakimu na Mawakili. Hili suala ni la muda mrefu, wakati umefika sasa maslahi ya Mahakimu yaboreshw na vilevile tunapozungumzia kuboresha maslahi ya Mahakimu na Mawakili, wengi tunajiuliza kwa nini wanakimbia Serikalini na kwenda sekta binafsi, lakini ni kwa sababu ya maslahi. Wanafanya kazi nzuri kwa hiyo naomba maslahi yao yaweze kuboreshw.

Mheshimiwa Spika, nirudie kidogo kuhusu ukarabati wa Mahakama, mwaka 2004, wakati tunachambua Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria, tulizungumzia sana ukarabati wa Mahakama zetu na bahati nzuri, tumepata nafasi ya kuitembelea Wilaya ya Lushoto.

Nataka niwapongeze kwamba, hivi sasa angalau tunaona maendeleo katika sekta hii. Mahakama nyingi zinaanza kukarabatiwa na vilevile Mahakama nyingi za Wilaya zimeanza kujengwa.

Meshimiwa Spika, hali iliyokuwa mwanzo ilikuwa ni mbaya sana, tuliwahi kutembelea Mahakama ya Mwanzo Manzese lakini nimeshukuru sana nimeona kwamba, Serikali sasa hivi inaweka mikakati ya kujenga hizi Mahakama na Mahakimu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, majengo wanayofanyia kazi ni mabovu, hawana usafiri na maslahi yao ni duni, kwa hiyo, hali hii inachangia kutoakutoa haki kwa wahusika.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzo, ilikuwa ni kuwapongeza tu wenzenetu, wanafanya kazi nzuri, lakini kubwa zaidi cha msingi ni kuongeza Bajeti yao ili waweze kutekeleza majukumu yao. Wanafanya kazi katika mazingira magumu, kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti lakini wanajitahidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante, kama nilivyoeleza, sasa tutawapa watoa hoja nafasi ya kupitia michango ya maandishi ili waweze kutoa majibu yao kwa pamoja wakati Bunge litakaporejea mchana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ESHA H. STIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mwanasheria Mkuu NA Maafisa mbalimbali wa Wizara hii, kwa kazi nzuri na makini alizozielezea kwenye hotuba yake ya Bajeti ya mwaka 2005/2006. Kwa furaha, naunga mkono hoja yake mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii nitazungumzia vipengele vifuatavyo: Kwanza, kuimarisha mfumo wa utoaji haki; utekelezaji wa shughuli za kiofisi umefanikiwa lakini Wananchi bado hawajafanikishiwa haki zao baada ya hukumu za kesi zao Mahakamani. Kwa mfano, wanaopata ajali (majeruhi), wanaokufa, wanaachwa wakitangatanga bila kujua wanalipwa na nani fidia zao na wanaojua wanalipwa wapi basi uzungushaji kutokana na sheria zilizopitwa na wakati zinasumbua utoaji wa haki zao na fidia.

Hali kadhalika, asilimia zinatolewa na madaktari ya walemvu wa ajali ni ndogo ikilinganishwa na mtu alivyoumia au ulemavu wa maisha alioupata. Naomba Mheshimiwa Waziri, afanye utaratibu maalumu au aanzishe kitengo cha kuwasaidia walemvu wa ajali za magari/treni na kadhalika ili kuwapatia urahisi wa kupata haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

MHE. ALI SAID SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, moja sheria ya kulazimisha kugombea nafasi za Serikali kwa kupitia Chama cha Siasa, itazamwe upya ili kutoa mwanya kwa wagombea binafsi kuruhusiwa kuingia kwenye kinyang'anyiro.

Pili, Sheria ya Uchaguzi ibadilishwe ili chaguzi za Serikali za Mitaa zisimamiwe na Tume ya Taifa ya Uchaguzi badala ya TAMISEMI.

Tatu, watendaji watakaobainika kuvunja haki za binadamu watangazwe hadharani na kuchukuliwa hatua kali ili iwe funzo kwa wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE: Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kuhusu maslahi ya Majaji, Mahakimu na watumishi walio chini ya hao niliowataja, yaboreshwe kwa maana ya kuongezwa. Huwezi kuamua haki wakati una njaa. Daima utashawishika kupata chochote na kuamua visivyo halali. Naishauri Serikali kuwa makini sana kwa suala hili muhimu ili kupunguza tatizo sugu linaloikumba Sekta ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kulundikana kwa mahabusu katika Gereza la Shinyanga Mjini, naishauri Serikali iwe makini kuangalia mahabusu waliokaa muda mrefu gerezani kwa tuhuma ya mauaji tangu mwaka 1997 bila kusikilizwa kesi zao. Watuhumiwa hao wa Kijiji cha Manyolo Wilayani Meatu walikuwa wanane, wanne wameachiliwa bila ya kesi kusikilizwa na wanenewa waliobaki bado wamo ndani, kulikoni? Naomba Serikali ilifanyie kazi, *RPC* Shinyanga analifahamu. Watuhumiwa wa kesi moja kugawanywa katika makundi mawili bila ya kesi kusikilizwa ni kuleta hisia ya

rushwa mionganini mwa jamii, hasa ikizingatiwa kuwa walioachiliwa wana uwezo wa hali ya maisha, pamoja na kwamba, nao walikaa miaka miwili gerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyolekwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Katibu Mkuu na timu nzima ya watendaji, kwa kazi ya kuiandaa bajeti hii kwa umahiri makubwa. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Aidha, baada ya kuunga mkono hoja hii, napenda nichangie katika maeneo yafuatayo kwa lengo la kuboresha hoja: Kwanza, ni kuhusu mishahara ya Mahakimu, ni midogo sana kwa mfano, Hakimu Mkazi (*Resident Magistrate*) analipwa shilingi 130,000/= kwa mwezi, baada ya makato mbalimbali anabakiwa na shilingi 80,000=/. Nyumba ya kupanga analipa shilingi 40,000/= kwa mwezi. Je, Mheshimiwa Waziri, atakubaliana nami kwamba, kiasi hicho aidha kitamfanya Hakimu apokee rushwa ili kumwezesha kuishi au itambidi afanye biashara kama vile kuuza njugu na kadhalika na kwa hali hiyo utendaji wake wa kutoa haki utaathirika?

Pili, pamoja na kupongeza juhudhi za Wizara katika kuhakikisha kuwa haki inatendeka kwa Wananchi wake, bado hali ya utoaji haki imekuwa ni tatizo kubwa. Idadi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ni ndogo mno. Hata wale wachache waliopo hawana usafiri wa kuwawezesha kuzungukia Kata mbalimbali. Serikali inasema nini kuhusu hali hiyo hasa katika Jimbo la Mbinga Mashariki lenye wakazi zaidi ya 300,000, Kata 24 na vijiji 130 na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wako watatu? Hivi kwa nini Serikali isianzishe utaratibu wa kuwapanga Mahakimu kwa kuzingatia idadi ya watu?

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha pia mpaka sasa tangu Wilaya ya Mbinga ianzishwe haijawahi kupata Hakimu wa Wilaya mwenye Shahada ya Chuo Kikuu (*LLB*), kuna tatizo gani ambalo linasababisha Wilaya kutotendewa haki hiyo ya msingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Tume ya Kurekebisha Sheria, kwa kazi nzuri wanayofanya. Nashauri Wizara sasa iletu Miswada ya Sheria Bungeni, ili Bunge litunge sheria kwa kuzingatia mapendeleko yaliyolekwa na Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, haki haiwezi kutendeka ndani ya mfumo unaorutubisha rushwa. Tume imeliona hilo, hasa kuhusiana na takrima, yaani ukarimu wa jamii ya Watanzania kwa kutunga sheria kuhusu ukarimu, ambao hata bila sheria utaendelea kuwepo. Kwa misingi hiyo, takrima ni kichefuchefu, ni pandikizi ndani ya sheria za nchi yetu, kwa hiyo, inapaswa kutoswa.

Mwisho, rushwa ya Tanzania ni mtoto wa mfumo wa utawala tulionao. Mapendekezo ya kuiondoa Taasisi ya Kuzuia Rushwa kutoka Ofisi ya Rais na kuwa na Tume Huru ya Kudhibiti Rushwa ndiyo dawa iliyobaki katika kuangamiza rushwa katika ngazi zake zote.

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wa Wizara hii, kwa kazi kubwa wanazofanya katika kusimamia haki za binadamu kisheria. Vilevile kutokana na utendaji mzuri wa Mahakama, kero ya rushwa inaonekana imepungua kwani malalamiko ya Wananchi yamepungua.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua picha iliyoko juu ya jalada ya kitabu cha hotuba hii kama ni ya mtu na ni mwanamke au mwanaume na kasimama juu ya nini na kashika fimbo au nini?

Kwa kuwa hakuna jedwali linaloonesha ujenzi wa nyumba za Mahakama na zinazokarabatiwa, naomba kujua Jengo la Mahakama ya Mvumi Makulu kama lipo katika kujengwa au kukarabatiwa?

Vile vile lipo tatizo kubwa la mlundikano wa kesi kutokana na upungufu wa Mahakimu; kwa nini Serikali isiwaajiri Mahakimu waliostaafu kwa Mkataba, wakafanya au wakaendesha hizo kesi zikaisha au zikapungua zaidi.

Suala la usafiri wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ni muhimu kwa sababu wanahudumia Mahakama zaidi ya moja. Naomba kujua kwa nini Serikali isiwakopeshe pikipiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. FATMA SAID ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Nampongeza Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Jaji Kiongozi, Mheshimiwa Amir Ramadhan Manento, pamoja na Watendaji Wakuu wote wa Wizara hii, kwa hotuba hii na kusimamia sheia za nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Katiba iangaliwe vizuri na ifanyiwe marekebisho pale inapobidi ili mfumo wa sheria ya Tanzania uweze kutoa mchango mkubwa kwenye kufufua uchumi wetu. Mfano, upatikanaji wa gesi na mafuta ni suala la Muungano, inakuwaje sasa nchi yetu haielewani kwenye suala hili? Naomba Mheshimiwa Waziri, anipatie ufanuzi Katiba inaelekeza vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Bibi Mwanaiidi Maajar, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Sheria Tanzania, kwa kazi yake nzuri ya kuandaa programu mbalimbali za kuhamasisha na kuelimisha wanawake

kuzifahamu sheria zetu na pia kusimamia marekebisho ya sheria zote zilizopitwa na wakati.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Kwanza, kuna malalamiko ya Wananchi wa Jimbo langu kwa fedha zao za mirathi kutolipwa baada ya aliyeziiba kufungwa. Nimekuandikia barua ya kukuomba uingilio kati na mara zote umenjibu kuwa utafuutilia kwa wasaidizi wako. Kwa kuwa hii ni bajeti ya mwisho kwa Serikali ya Awamu ya Tatu, je, kuna fedha zozote zimetengewa kwa waathirika hawa?

Majengo ya Mahakama za Mwanzo katika Jimbo langu yamechakaa sana. Kwenye hotuba yako umeeleza kuwa una mpango wa kufanya ukarabati. Je, katika Jimbo langu la Nzega ni Mahakama gani zimo katika bajeti 2005/2006.

Kuna upungufu mkubwa wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na hata za Wilaya, kuna mpango gani kutatua hili?

MHE. PHILIP S. MARMO: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani kwa Idara za Mahakama. Wilaya yetu sasa ina Hakimu wa Wilaya mpya na tumeletewa Mahakimu watatu wa Mahakama za Mwanzo. Sasa angalau kati ya Mahakama za Mwanzo 11 Wilayani Mbulu, Mahakama nne sasa zitakuwa na Mahakimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa saba inataja kwa kifupi sana kuhusu *Alternative Dispute Resolution (ADR)*, yaani usuluhishi wa mashauri unaofanywa na Mahakama. *May I now declare interest that is, having passed several examinations on arbitration in Tanzania and Kenya; in few weeks time, I shall be a registered member of both Tanzania Institute f Arbitration nd later Kenya Institute of Arbitration.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepitisha sheria nyingi katika miaka ya karibuni inayolazimisha kabisa usuluhisho badala ya ushauri kupelekwa Mahakamani ili mashauri yakamilike haraka na wahusika kupata nafasi ya kumchagua msuluhishi. Sheria hizo ni pamoja na zile zinazoanzisha Wakala wa Serikali kama vile *SUMATRA*, *EWURA*, *TCRA*, *TANROADS* na kadhalika. Hili ni eneo linalokua haraka na wakati umefika kwa Wizara kutambua eneo hili na kutunga sheria mpya ya *arbitration*. Usuluhishi wa aina hii sasa hivi nchini kwetu unavamiwa na wasuluhishi kutoka Kenya, Uganda na Afrika Kusini, kwa sababu makampuni makubwa ya biashara na ujenzi yanafanya kazi nchini kwetu.

Pamoja na Mahakama ya Ardhi kutokuwa na majengo ya kufanya kazi, Mahakama hii hushughulikia mashauri ya matajiri na wakazi wa mijini zaidi, kwa vile Wilayani kwenye Kata na Vijijini, hakuna Mabaraza ya Ardhi, hakuna fedha za uendeshaji. Hii dosari ni kubwa kwa vile Mahakama za Mwanzo hazipokei mashauri ya ardhi.

Uamuzi wa kuanzisha *School of Law* ni mzuri, lazima kuwe na uangalifu mkubwa katika kuiandaa *syllabus* ya *School of Law* katika enzi hizi za utandawazi na kukua kwa teknolojia ya kisasa. Masomo ya zamani ya *Traditional Schools of Law*, sasa yamepitwa na wakati. Bila shaka masomo kama vile *Book-keeping* na *Accountancy* sasa yataongezewa *Computer, Studies, Legal and Legislative Drafting* na kadhalika.

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru Wizara, kwa kueleza mafanikio ya Wizara ambayo ni ya kweli nawapongeza. Majengo mengi yamejengwa, Miswada mingi imeletwa na kuboreshwa kwa manufaa ya Wananchi. Nawapongeza kwa kuajiri Mahakimu ambao walikuwa tatizo miaka ya nyuma, sasa upungufu huo umepita, Mahakimu wanapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate ufanuzi kuhusu mambo yafuatayo:-

Kwanza, katika Jimbo langu kuna Mahakama za Mwanzo ambazo ziko kwenye ujenzi wa Mpango wa *Quick Start*, ambazo ni Mahakama za Mwanzo Longido na Mahakama ya Mwanzo Enduimet. Je, mpango huo umeishia wapi, Wananchi wa Jimbo la *West Kilimanjaro* wanategemea Mahakama ya Monduli ambayo iko mbali sana wanapita Mahakama nyingi hata Mahakama Kuu wanaenda Mnduli, ni lini litaanza kujengwa?

Pili, kwa kuwa jengo la Mahakama ya zamani liko hatarini kuanguka kwani ni lilijengwa na Wajerumani; na kwa kuwa Wananchi wamejenga Mahakama yao Longido mpaka kiwango cha madirisha na jengo lipo kwenye mpango huo wa *Quick Start*; ni lini Serikali itamaliza ujenzi huo?

Mwaka 2004 nilitoa hoja kuhusu vijana waliohukumiwa kifungo cha miaka 40 kila mmoja kwa sababu ya wizi wa mifugo. Vijana hao hawakuwa na Mawakili wa kutafsiri wakati wa hukumu yao, kwani hawajui Kiswahili. Naomba Mheshimiwa Waziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wanieleze, pamoja na familia za vijana hao, je, ni Utawala Bora watu kufungwa bila kujua hukumu yao wala kujitetea?

Mheshimiwa Naibu Spika, haki za binadamu ni pamoja na kupewa nafasi kujitetea, hao vijana ambao hawajaitetea hawakunyimwa haki zao? Kwa vile wamehukumiwa bila wazazi wao kujua kwamba wamefungwa miaka 40 na mpaka leo hawajulikani waliko, je, kitendo hicho siyo kinyume cha haki za binadamu?

Kama wamefungwa mwaka 1997 na bado wanatumikia kifungo hicho. Je, kusema muda umepita kwa vile ni muda mrefu sana tangu wahukumiwe si ni kuwanyimwa haki zao, kwa nini waendelee kuteseka kwa ajili ya muda?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate ufanuzi kuhusu jambo hilo?

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza, kumpongeza Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, kwa kazi nzuri

anayofanya katika Wizara hii bila ya kuwa na Naibu Waziri. Nawapongeza pia watendaji wake wanaompa msaada mkubwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nitauelekeza katika maeneo fulani na nina mapendekezo yafuatayo: Kwanza, kuhusu kuundwa Mahakama Maalum ya Watoto na Kesi za Ndoa. Kama ilivyoonekana umuhimu wa kuwa na Mahakama Maalum kwa wafanyakazi, ardhi na biashara na sasa kuwepo kwa Magereza Maalum ya Watoto na kuongezeka kwa makosa na kesi za watoto na malalamiko ya ndoa katika familia nydingi, ipo haja kufikiria kuunda Mahakama Maalum ya Watoto na pia kujumuisha kesi za ndoa na kesi zinazohusu ulawiti na mimba kwa watoto wanaosoma.

Faida za kuanzishwa aina hii ya Mahakama ni pamoja na kupunguza msongamano wa kesi katika Mahakama; kuongeza nafasi za Mahakama kujihusisha na kesi kubwa na makosa makubwa yanayohitaji muda mrefu wa kusikilizwa na kusaidia kuimarisha utekelezaji wa sheria mpya zinazohusu haki za watoto na wanawake, ndoa na haki za binadamu.

Pili, kuboresha Mabaraza ya Kata ambayo yanafanya kazi za kusimamia haki, kutoa maamuzi sawa na hukumu. Hata hivyo, yanaendeshwa na wazee wa kijijini wenye busara, lakini wengi hawana elimu ya sheria. Katika kuboresha kazi zao ni vema Wizara ya Sheria ikatambua umuhimu wa kuboresha Mabaraza haya kwa njia zifuatazo:-

(a) Kuwapa elimu ya sheria ndogo ndogo kama vile sheria za ardhi za vijiji, sheria za ndoa, sheria mpya za haki za watoto na kadhalika. Nia sio kuwafanya wawe Mahakimu, bali kuwapa mwanga wa kujua mabadiliko ya kisheria ya nchi.

(b) Kuboresha majengo yanayotumiwa kama ofisi za Mabaraza ya Kata. Pamoja na uwezo mdogo wa sasa kukidhi mahitaji ya majengo ya Mahakama ndogo katika ngazi mbalimbali, lazima tuwe na upeo wa mbali na kuiandaa mipango ya baadaye ya kuimarisha Mabaraza ya Kata.

(c) Ni lazima tukubali kwamba, mfumo wa Mahakama unaelekea kuanzia katika ngazi za Mabaraza ya Kata. Kwa msingi huo ni lazima kuchukua jukumu la kulipa gharama za watendaji wanaosaidia kusimamia haki na sheria katika ngazi hizo. Hivyo, Wizara lazima iandae utaratibu wa kushiriki kulipia gharama zote halisi za kuendesha mfumo wa sheria wa Mahakama au vyombo vyake vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Kongwa, wanashukuru sana kwa ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya kisasa, yenye kumbi mbili, *Rest House* na Majengo mengine.

Tunaomba taratibu za ufunguzi rasmi, zifanywe na tunakuomba Mheshimiwa Waziri, uje ujionee kazi nzuri walifanya JKT ya ujenzi huo. Nashauri JKT wapewe

kandarasi za ujenzi sehemu nyingine za nchi. Pia nashauri zitengwe fedha za kujenga nyumba ya Hakimu wa Wilaya japo moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji Mdogo wa Kibaigwa hauna Mahakama, sina hakika kama kwenye mradi wa Mahakama 51 zitakazojengwa nchi nzima, hiyo imo pia.

Tunaomba ufanuzi wa Mahakama hizo 51 na 43 zitakazokarabatiwa ni zipi na wapi zoezi hilo litafanyika. Mahakama za Mwanzo Kongwa ni chakavu mno, vilevile Mahakama za Mwanzo za Sagara, Mlali, Pandambili, Mkoka, Zoissa na kadhalika, ni chakavu mno, zikarabatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo kukopeshwa pikipiki na kuzilipia kwa unafuu wa ruzuku ya Serikali. Kila Hakimu mmoja anahudumia Tarafa, wapewe usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee wa Mahakama bado wanalamikia posho zao. Suala hili lishughulikiwe liishe kwa vile wengi wa wazee hawa ni wa umri mkubwa na wanalamikia sana madai yao ya siku za nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, wako mahabusu wengi magerezani hasa Gereza la Kongwa, ambao kesi zao haziendi kwa wakati Mahakamani, upo ucheleweshaji wa kesi mkubwa mno. Ipo haja ya kuangalia vema namna ya kuhalalisha mashauri Mahakamani, kama dira ya Wizara inavyosema: “Haki kwa wote na kwa wakati”.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ISSA MOHAMED SULEIMAN: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naIpongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri, pamoja na kazi nzuri mliyofanya Wizarani na kuifanya Serikali kuongeza uwezo wa kifedha wa Wizara hii ili ifanyi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeamua kuchangia Wizara hii baada ya kuona kasoro moja kubwa ambayo haikujitokeza popote. Kasoro hii ni Mahakama ya Kadhi. Nilidhani maelezo japo mafupi yangelikuwemo ukurasa wa 47 wa Hotuba yako pale ilipotamka changamoto ya awamu ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mahakama ya Kadhi lilishughulikiwa ipasavyo na Kamati ya Bunge inayoshughulikia Wizara hii, yaani Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kamati hii ilitumia fedha nyingi za kodi za Wananchi kwa kufanya ziara nchini Kenya, Uganda, Msumbiji na hata Zanzibar. Kamati ilikamilisha kazi yake na kuwasilishwa rasmi Bungeni. Hata hivyo, tangu mwaka 1995, suala hili limedharauliwa sio tu na Wizara, lakini kwa kutokuelezwu japo kidogo hatima yake. Naona na Serikali nayo imelipa mgongo. Je, sasa tuwe na mawazo gani na kipi kinaendelea?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu kwa Wizara hii kuona umuhimu wa Mahakama hii mbele ya jamii kwani itasaidia sana uimarishaji wa miundombinu ya utoaji

haki, maana naona imelengwa kwenye majengo tu. Pamoja na hayo, Mahakama hii itasaidia sana programu ya kuboresha sekta ya Sheria na kuridhisha waumini wa Mahakama za aina hii ambao wana asilimia kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao cha 18 cha Bunge, yalipitishwa marekebisho ya Katiba, lakini bado hakuna machapisho ya Katiba yenye marekebisho hayo. Nashauri kazi hiyo ifanywe haraka kwa sababu siyo vizuri Wabunge wapya wakaja wakapewa Katiba ya kufanya kazi ambayo imepachikwa karatasi za marekebisho.

Mwisho, hivi sasa Tanzania inaelekea kwenye Umoja wa Kisiasa wa Afrika ya Mashariki. Wakati tayari tumefikia kuwa na makubaliano ya kiuchumi na wakati huo huo tunazo tofauti za makubaliano ya kisheria ndani ya Tanzania yenyewe, yaani kati ya Tanzania Bara na Zanzibar, basi ni vizuri hivi sasa Serikali zetu mbili zikakaa na kuangalia kasoro za kisheria tulizokuwa nazo. Tukidharau hivi sasa, naamini hatima yake hatutazungumza kesi za Muungano, bali tutakuwa na maudhi ya Muungano, ambayo yatakuwa makubwa zaidi ya kero za sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na kuwatachia kila la heri wahusika wote.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, kwa hotuba yake nzuri, ambayo ameitoa asubuhi ya leo. Tunampa pongezi sana.

Naomba kuchukua fursa hii, kukumbushia tatizo la Mahakimu katika Jimbo langu, hususan katika Mahakama za Mwanzo za Sanya Juu, Barazani na Ngare-nairobi. Ombi hili ni la muda mrefu, naomba liweze kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ARIDI M. ULEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika maeneo machache katika hotuba ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba. Mchango wangu zaidi unalenga katika Mahakama za Mwanzo katika jimbo la Nanyumbu. Kwa miaka kadhaa sasa Jimbo la Nanyumbu, limekuwa na Hakimu mmoja tu aliyepo Mahakama ya Mwanzo ya Mangaka. Kutokana na ukubwa wa Jimbo la Nanyumbu, kulistahili kuwa na Mahakama za Mwanzo tatu. Mahakama hizo ni Mangaka, Nanyumbu, Nakopi na Michiga. Hivyo, kuwa na Hakimu mmoja kwa Jimbo lote la Nanyumbu ni kuwanyima haki Wananchi wa Jimbo la Nanyumbu. Hali hiyo inapelekea wakati mwingine Wananchi kuacha kuapeleka watuhumiwa mbele ya vyombo vyaa sheria kwa kukwepa usumbufu wa nenda rudi Mahakamani. Naomba Serikali ipeleke Hakimu mwingine katika Mahakama ya Nakopi ili asaidie kusikiliza kesi zinazoletwa katika Mahakama za Michiga na Nakopi ili Hakimu wa Mangala ahudumie Mahakama za Mangala na Nanyumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya majengo ya Mahakama za Mwanzo za Mangaka, Nanyumbu, Nakopi na Michiga, ni mbaya kwa kukosa matengenezo kwa muda mrefu sasa. Naomba Serikali ifanyie matengenezo majengo hayo ili yakidhi hadhi ya kuwa Mahakama. Vile vile nyumba za Watumishi nazo zifanyiwe matengenezo ili kulinda usalama wa Mahakimu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo, naunga mkono hoja hii moja kwa moja.

MHE. TALALA B. MBISE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba na timu yake, kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya Wizara na kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii. Napenda kueleza kwa kifupi, mambo ambayo nimeona yaktendeka kwenye jamii, ambayo ingefaa Wizara ikafahamu na kuyafanya uchunguzi/utafiti kuona kama kuna ukiukwaji wa taratibu au mfumo wa utendaji wa sheria.

Nimeona katika maeneo kadhaa Vijijini, Wananchi hupeleka kesi zao kwenye Ofisi za CCM za Vijiji kusikilizwa na kutolewa uamuzi na haki kutolewa. Kesi ya aina hii huchukua muda mrefu au mfupi sana kutegemea na suala husika. Mara nyingi wahusika humaliza kesi zao kwa njia ya faini na/au rushwa. Sijui ni kwa kiasi gani Wizara inafahamu hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Wizara ilifanyie uchunguzi suala hili, kwa nia ya kuondoa ujisadi ambao huenda umeota mizizi ngazi ya Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi nyingi zinatolewa kwa Wizara hii, kwa kazi nzuri sana mnazozifanya za kutoa haki za raia nchini.

Nampongeza Mwanasheria Mkuu, Katibu Mkuu, Jaji Mkuu, Jaji Kiongozi, Msajili wa Mahakama, Wakuu wa Tume zote za Haki, Waziri na Wakuu wa Taasisi mbalimbali za Wizara hii, Majaji, Mawakili, Wanasheria, Mahakimu na Wazee wa Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kufahamu wazee wa Mahakama hivi sasa wanalipwa kiasi; je, mnadhani kiasi hicho kinatosheleza na kuna mpango wowote wa kuwaongezea posho zao na madai yao ya nyuma yanalipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Haki za Binadamu, imefanya kazi nzuri sana, naomba iunganishwe na Tume ya Rushwa ili kuona mienendo ya nchi na tabia za Viongozi wanaokosa maadili mema, hasa viongozi wanaonyanyasa raia, vyombo vyetu vya Dola na tabia nchi kijumla na kushauri Rais wa nchi kuwaondoa madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya Majaji, Mahakimu, Mawakili wa Serikali na Wanasheria Nchini, bado kuna matatizo katika eneo hili. Kazi ya kutoa haki kwa raia ni ngumu sana, inahitaji utulivu, umakini, kazi ya kiroho nusu. Inahitaji watoe haki kuwa na maslahi, mafao mazuri, ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Naomba sanasana waongezwe maslahi. Wizara inasemaje? Naomba kama ipo fedha wapewe motisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, atoe idadi ya kesi za muda mrefu ngazi ya Mahakama Kuu na Rufaa kama ifuatavyo: Za miaka 50 ni kesi ngapi; za miaka 40 ni kesi ngapi; za miaka 30 ni kesi ngapi; za miaka 20 ni kesi ngapi na za miaka 10 ni kesi ngapi. Shida nini hasa, ushahidi, uchunguzi au upungufu wa Majaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kesi ya uchaguzi ya Hai - Moshi bado sijaona matokeo yake! Inakumbukwa kuwa Mheshimiwa Freeman Mboge alishtakiwa kwa kukiuka baadhi ya mambo ya uchaguzi mwaka 2000; je, kesi imefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mahakimu wakopeshwe pipipiki kwa masharti nafuu ili waweze kutembelea maeneo yao kama vile Mahakimu wa Mikese, Kingolwira, Ngerengere, Gomero, Bwakira, Mkuyuni, Tawa, Kolelo na kwingineko nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya mahabusu inazidi kiwango ambacho kinatakiwa. Kusu muda wa kukaa mahabusu kabla ya kufungwa, naomba suala hili wanaohusika na mahabusu na Magereza wakae ili watoe uamuzi wa makusudi juu ya muda wa mtuhumiwa kukaa mahabusu, kuwe na *limited time*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri na timu yake, wao kama wanasheria, wanaionaje kesi ya Babu Seya na tukio la kesi hii kwa kuanisha busara?

MHE. DR. THADEUS M. LUOGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wataalamu wote wa Wizara, kwa hotuba yao nzuri, iliyochambua mambo yote muhimu na majukumu ya Wizara. Kutokana na hali hii, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niyafikishe maombi mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kutokana na hali mbaya ya Mahakama ya Mwanzo Liuli, Mahakama imefungwa na Wananchi wa Tarafa ya Ruhuhu na sehemu ya Tarafa ya Luakei wanakosa huduma hii muhimu. Tunaomba Mahakama hiyo ikarabatiwe ili Wananchi waendelee kupata huduma ya Mahakama ya Liuli.

(b) Kama haiwezekani kukarabatiwa kwa Mahakama ya Liuli basi tuna jengo moja kubwa na imara la CCM Puulu, wanachama wako tayari kuachia sehemu ya jengo hilo na ikatumika kama Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono tena mia kwa mia, naomba mawazo yangu niliyoyatoa hapo juu yakubaliwe.

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na Wasasidizi wake, kwa hotuba nzuri.

Napenda tu nifahamu kutoka kwa Waziri ni lini hasa Mahakama za Bashanet, Ufana, Dareda, Gidas na Bonga, zitapata Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo?

Mheshimiwa Waziri, aliwahi kuitembelea Wilaya ya Babati na kujionea umbali wa Mahakama za Bashanet, Ufana na Dareda na Mahakama ya Babati, ambako kuna Mahakimu wawili tu, zaidi ya kilomita 60. Wananchi wanalazimika kusafiri kwa gharama umbali wote huo. Ahadi ya Waziri ilikuwa kutupatia Mahakimu angalau Bashanet au Ufana na Dareda kwa kuanzia, lakini bado hajatupatia hadi leo. Kama mpaka sasa hatuna Mahakimu na ni mpango wa Wizara kuajiri Mahakimu 40 wa Mahakama za Mwanzo, je, tuamini kuwa kati ya hao wachache tutapewa kipaumbele? Je, wakati tunasubiri hatua hizo za kawaida, isingekuwa vizuri Mahakimu wale wawili pale Babati (Wilayani) wakapanga ratiba ya kusikiliza kesi na malalamiko kule Bashanet, Dareda na Ufana?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hoja zangu na mapendekezo ya Wananchi kufuatwa kule waliko na Mahakimu hao wawili waliopo ili kuwapunguzia adha Wananchi, naunga mkono hoja.

MHE. LEONARD N. DEREFA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Naomba kutoa ushauri na maombi yafuatayo: Kwanza, naipongeza Wizara kwa kukarabati Ofisi ya Mahakama ya Mwanzo ya Mjini Shinyanga iliyoungua moto. Nawapongeza sana. Naomba Wizara ikamilishe kutupatia Mahakama Kuu katika Mkoa wa Shinyanga. Nashangaa kuona kwenye makisio ya maendeleo hakuna fedha ambazo zimekwisha kukamilisha upatikanaji wa Mahakama Kuu Shinyanga kutokana na kesi nydingi za mauaji mkoani kwetu ya vikongwe. Mkuu wa Mkoa aliwahi kutueleza kuwa kwa mwaka 2005/2006, Mahakama Kuu itajengwa ama watanunua Jengo la CCM lililoko *Kambarage Stadium*. Nilishukuru sana kupata maelezo, lakini napenda kuuliza kazi hii itafanyika lini?

Nashukuru kuona kuna Mahakama imeongezewa fedha mwaka hadi mwaka; mwaka 2003/2004 ilipata shilingi 16.6 bilioni; mwaka 2004/2005 ilipata shilingi 18.7 bilioni na mwaka 2005/2006 ilipata shilingi 27.878 bilioni. Kutokana na kuboreka kwa mapato ya Serikali, bajeti inatakiwa iongezwe hadi kufikia shilingi 60 bilioni na maslahi ya Mahakimu yaboreshwe, pamoja na makazi yao, kuwapatia magari na kufanya ukarabati wa Mahakama zetu nchini. Kama Mahakama haipewi nyenzo za kutosha haki inaonekana kutokuwepo. Serikali pia iwe inatoa fedha za kutosha kulipwa mashahidi ili kesi zisiwe zinakwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema posho kwa Wazee wa Mahakama zilipwe mapema. Katika Jimbo langu Wazee wa Mahakama wanadai shilingi 7152,000/. Wazee hao pia wameachiswa kazi na kuajiriwa wengine. Hata walio ajiriwa upya, nao wanalamika maana tangu wameanza hawajalipwa. Utaratibu wa sasa wa kulipa Wazee hawa ni vema ukatazamwa upya ili kutenda haki. Ni vema angalau wakawa wanalipwa *fixed amount*, kama posho, maana kesi nyingi hazikamiliki kwa haraka kuwawezesha kupata malipo yao. Kwa mwezi mzima mzee anaweza asilipwe fedha yoyote, hii inaweza kuwa kichocheo cha rushwa.

Vilevile upatikanaji wa Sheria zinazotungwa na Bunge katika Mahakama zote za Mikoa, Wilaya na Mahakama za Mwanzo, uboreshwe kabisa ili kuwafanya Mahakimu kuhukumu kwa Sheria zinazotungwa na Bunge.

Tunashangaa hukumu ya Jaji wa Haki za Binadamu kubezwa na Serikali!

Mwisho, ninawatakia utendaji mwema wa malengo mliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

MHE. DANHI B. MAKANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini wataruhusu Mawakili katika Mahakama za Mwanzo ili kuwasaidia Wananchi ambao hawajui kujitetea na kutafsiri lugha ngumu za kisheria na za Kimahakama?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama inatoa kipaumbele gani kwenye kazi za Wabunge waliofukuzwa Ubunge hususan kwa kuonewa, hawaoni kuwa kuchelewesha kesi ni kuwaadhibu wapiga kura zaidi kwa kukosa uwakilishi, mfano, Jimbo la Kisesa la Mheshimiwa Erasto Tumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kufahamu juu ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vyenye Wabunge, endapo Wabunge wakipungua na ruzuku inapungua au wakiongezeka kupitia *by-elections*, chama kinaongezewa ruzuku? Kama hivyo siyo, viongozi wa vyama mbalimbali, wasio na maadili ya uongozi wataendelea kuwaonea Wabunge wasio na hatia na hivyo kuwaadhibu wapiga kura husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na utaratibu uliopo wa Sheria ya Wabunge wa Viti Maalum, Wabunge wanne wa Majimbo huweza kutoa Mbunge mmoja wa Viti Maalum na hivyo hivyo kwa Madiwani. Je, kama Wabunge wa Majimbo watapungua au kwisha kabisa kwa kufukuzwa au namna nyingineyo, huyu Mbunge wa Viti Maalum au Diwani anapata uhalali gani kubaki Bungeni au kwenye Baraza la Madiwani?

Kwa nini chama kinachoongoza Wabunge au Madiwani kisiongezewe Wabunge au Madiwani wa Viti Maalum baada ya kushinda katika chaguzi ndogo?

(Saa 05.46 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru kwa kunitambua, adhuhuri hii na kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kazi hiyo, ningependa kutumia fursa hii kutoa salamu zangu za rambirambi kwa familia, ndugu na marafiki wa Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kupitia CCM na Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero. Namwomba Mwenyezi Mungu, azilaze roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa salamu hizo, sasa napenda nijielekeze kwenye hoja hiyo na nianze kwa kumpongeza kwa dhati, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, kwa hotuba yake nzuri, yenye mwelekeo na inayotoa matumaini kwa Watanzania. Chini ya uongozi wake, tumeshuhudia maboresho katika sekta ya sheria, ambayo yamechukua sura mpya. Ni mwanzo mzuri, tunampongeza sana kwa uongozi wake. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge, waliochangia hoja hii kwa kusema na mimi naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Mchango wangu utakuwa mfupi na nitagusia maeneo machache tu yanayohitaji ufanuzi wa masuala mbalimbali ya sheria yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu na moja la Mheshimiwa Issa Suleiman, kuhusiana na toleo jipya la Katiba. Ni kweli aliyojasema, mchango wake ni mzuri kwamba, Wananchi wa Tanzania, wanglipenda kuona marekebisho ya 14 yaliyofanywa hivi majuzi, yanavyotiririka katika Katiba ya Nchi yao. Napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi yangu karibu inakamilisha zoezi hili na muda si mrefu, toleo jipya la Katiba ya Jamhuri ya Muungano litapatikana na kwa wingi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nisisitize kitu kimoja, utoaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyo kwa sheria nyingine za nchi yetu si jambo ambalo mtu unaweza ukarudufu tu, lina utaratibu na linasimamiwa na sheria.

Kwa hiyo, naliomba Bunge lako, Waheshimiwa Wabunge na nawaomba Watanzania kwa ujumla, wawe makini sana na nyaraka ambazo zinarudufiwa, naweza nikasema nyingine ni mitaani kabisa. Kwa hili kwa sababu ni Katiba ya Nchi ni vizuri tukafuata taratibu zilizowekwa na sheria.

Mheshimiwa Herbert Mntangi, alitoa hoja kuhusu kuundwa Mahakama Maalum ya Watoto na pia masuala ya kesi za ndoa. Kuhusu ombi au pendekezo la kuwa na Mahakama Maalum za Watoto, utaratibu wa sasa uliopo unatosheleza kwa eneo hili. Tuna sheria mahsus kwa eneo hilo na ni kusudio la Serikali, kuiboresha zaidi sheria hiyo na ikabidi kutunga sheria nyingine ambayo itahusiana na eneo la watoto na vijana. Katika kusikiliza kesi zinazohusu watoto, haki za watoto huwa zinazingatiwa na Mahakama zetu, kwa hiyo, hilo sio tatizo.

Kuhusu suala la kuanzisha Mahakama ya Ndoa, nasema hatuoni kama ipo haja kwa sasa kwa sababu tunaamini Mahakama zilizopo zinatosheleza kwa suala hili. Watoto wanaopatikana na matatizo na kupelekwa Mahabusu, taratibu zetu magerezani au mahabusu zinataka kuwatenganisha hawa watoto na wafungwa ambao ni watu wazima. Sababu ni wazi tu si lazima nizisemee hapa. Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, ananikodolea macho sijui kwa nini? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze katika eneo lingine, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, alisema suala la mgombea binafsi hili limakuwa linaludiwa rudiwa. Lakini tuseme tu wazi kuwa, Serikali katika kupata maoni ya Wananchi kwenye eneo hili, Wananchi walio wengi walisema wakati wake bado haujaiva. Sasa Katiba lazima izingatie mahitaji na matakwa ya Wananchi walio wengi. Hasa kwa sasa tunasema kwenye eneo hili nisingelipenda niendelee nalo zaidi, kwa sababu nafahamu na wengi wenu mnafahamu liko Mahakamani.

Alipendekeza pia kwamba, Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ifanyiwe marekebisho kwa lengo kwamba, chaguzi katika ngazi za Vijiji, Vitongoji na Mitaa, zisimamiwe na Tume ya Uchaguzi. Mamlaka ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi yako kwenye Katiba kifungu cha 74(6), kwenye eneo hili inatamka wazi kwamba, itasimamia chaguzi za Rais, Wabunge na Madiwani tu. Nifafanue kidogo hapa. Amesema TAMISEMI ndiyo inasimamia. Waziri mwenye dhamana ya masuala ya uchaguzi katika ngazi hizi, kazi yake ni kuandaa kanuni na taratibu na kuteua watakaosimamia chaguzi hizo. Huo ndio utaratibu na hayo ndiyo matakwa ya sheria, ye ye sio Msimamizi wa Uchaguzi wa hizo. Sasa kama yapo mapungufu, nadhani tujielekeze huko tuweze kuiboresha zaidi.

Lakini pia Bunge hili hili mmekuwa mnaiasa Serikali kwa masuala mazima ya kupunguza gharama ya matumizi na mnafahamu nchi yetu ilivyo kubwa, idadi ya vijiji katika nchi yetu. Sasa ukisema Tume tunaweza kusema Tume ifanye kazi hiyo lakini pia *implications* zake tuzifahamu hasa kwa upande wa gharama. Lakini tumesema mara nyingi hapa, mtandao wa utawala tulionao nchini ndio ule ule unaotumiwa na Tume ya Uchaguzi. Sasa kama unataka uboreshwe, mimi ningelipenda tuanzie na daftari hili la kudumu la wapiga kura, tuone kwanza linafanyaje na tupate ile *confidence*, imani iimarike, tuone kiasi gani *information* iliyo katika daftari hilo kwa wakazi wa maeneo yetu vijijini na mijini, tuweze kuona kama tunaweza tukafurahisha zaidi na kuboresha utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie katika eneo hili kwa kusema, katika nchi nyingi ambazo zina mfumo wa utawala katika ngazi hiyo kama Tanzania, Tume ya Uchaguzi, haiendi chini ya Uchaguzi wa Madiwani. Huo ndio ukweli. Ninyi ni watafiti wazuri, angalieni masuala haya. Kwa hiyo, tusije tu na pupa kwa sababu mtu ana tatizo lake na kusema basi chaguzi hizi zifanywe na Tume ya Uchaguzi. Tunaipongeza Tume ya Uchaguzi, kwa kazi nzuri wanayofanya na naamini katika Uchaguzi Mkuu unaokuja, itafanya kazi nzuri na itasimamia uchaguzi ili kuhakikisha kwamba, Uchaguzi Mkuu unakuwa wa haki, huru na kweli unakidhi matakwa na mahitaji ya Vyama vyta Siasa ambavyo vitaingia katika ulingo wa ushindani wa sera.

Vile vile aliuliza kuhusu uvunjwaji wa haki za binadamu, wanaofanya hivyo kwa nini wasitangazwe hadharani. Nasema pale ambapo Wananchi wanafikisha malalamiko yao mbele ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume inasikiliza hadharani, hajifungii kwenye chumba, haisikilizi malalamiko hayo faragha. Kwa hiyo, hakuna haja ya kusema kwamba, watangazwe na wachukuliwe hatua hadharani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nielekee kwenye eneo lingine ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Ireneus Ngwatura. Tangu Wilaya ya Mbanga ianzishwe haijawahi kupata Hakimu wa Wilaya mwenye Shahada ya Chuo Kikuu (*LLB*). Inawezekana, nampa pole sana lakini ni sera ya Serikali kuwa Mahakama katika ngazi hiyo, Mahakimu wetu hao hawahitaji kuwa na Shahada ya Chuo Kikuu. Hawa Mahakimu wetu katika ngazi hii wana Stashahada tu za Sheria. Niseme lingine ambalo Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba alilisema katika kipindi cha nyuma ni Sera ya Serikali kuiondoa hii kada ya Mahakimu hawa wa Wilaya na tutafanya hatua kwa hatua kwa kadri tunavyowapata Mahakimu wenye Shahada ili tuwapeleke katika ngazi ya Wilaya. Hawa baadhi yao ni watu wazuri tu, wamejiendeleza na tungelipenda sana wajijendeleze na wale ambao watafuzu vigezo ambavyo vinawawezesha kuteuliwa na kubadilisha kazi kwa maana watakuwa *Resident Magistrates*, kwa sura hiyo basi na wao tungelipenda sana wabakie na waweze kufanya kazi hiyo. Tunawapongeza kwa kazi wanayotufanyia na ni vizuri mtambue hivyo. (*Makofi*)

Alishauri pia Tume ya Kurekebisha Sheria na Wizara ilete Miswada ya Sheria Bungeni. Hivyo, ndivyo inavyotokea. Mkiona *Written Laws (Miscellaneous Amendments)*, ni matokeo ya kazi nzuri inayofanywa na Tume hii. Mengi tunayaleta kwa namna hiyo. Wameyachambua na Serikali ikaona hili limeiva. Lakini yapo mapendekezo yanayotokana na Tume hii ambayo ina sura ya kubadilisha sera au mfumo wa utoaji haki. Sasa haya kwa sababu ni ya sera yanahitaji tena mchakato mpana ndani ya Serikali ili kuhakikisha kwamba, yanapata ule muafaka, ile *broad ownership* ya mapendekezo hayo kabla ya kuyafikisha hapa Bungeni kwa njia ya Muswada au Miswada. Lakini hili Serikali inakuwa inalifanya. Juzi Waziri aliwasilisha taarifa, zilikuwa kama saba au 10 hivi, nyingi kidogo, ambayo inaonesha kazi nzuri ambayo inafanywa na chombo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Bunge lako Tukufu lilikubali tuongeze idadi ya Makamishna kutoka idadi ya sasa ya Makamishna saba wawe tisa kwa sababu tunajua kazi inaongezeka sana. Tunahitaji tuone wanafanya kazi hii kwa kasi na hasa pia tungelipenda tuone wanapata watafiti hawa waweze kuwasaidia katika kazi hii ambayo wanaisaidia sana Serikali.

Mheshimiwa Fatma Said Ali, yeye alisema mfumo wa sheria ya Tanzania unaweza kutoa mchango mkubwa katika kufufua urchumi. Mfano, upatikanaji wa mafuta ya gesi na mafuta kwamba ni suala la Muungano, inakuwaje sasa nchi yetu hailewani katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu niseme kwamba, nakubaliana na Mheshimiwa Fatma Said Ali na namwona anaingia sasa hivi kwamba, mfumo wa sheria nchini unaweza kutoa mchango mkubwa katika kufufua uchumi. Ndiyo maana tangu Serikali ianze sera na mikakati mbalimbali ya kufufua uchumi, hatua hiyo imeendana ama na kutungwa kwa sheria mpya au kuzifanya marekebisho sheria zilizopo ili zikidhi haja na mahitaji ya wakati huu. Serikali imefanya hivyo, mtakumbuka katika sekta ya fedha, sekta ya madini, sekta ya mawasiliano na sekta nyingine nyingi. Kwa sababu bila hiyo, huwezi ukafanikisha haya ambayo kupitia Ilani ya Chama Tawala ilichoahidi kwa Wananchi kwamba, haya mtayafanya, mengine yanahitaji kutungiwa sheria au kufanya marekebisho kwa sheria zilizopo. Haya yameteklezwa na Serikali itaendelea kuyafanya hayo.

Sasa kuhusu suala la upatikanaji wa gesi asilia na mafuta yasiyochujwa kama alivyosema, ni kweli hili suala ni la Muungano na hakuna ubishi kwa hilo. Lakini niseme tu kitu kimoja kwamba, suala hili sasa hivi linashughulikiwa na Serikali zetu mbili na kwa vile utashi wa kisiasa kuhusu kuendelea kuwepo kwa Muungano wetu bado upo, naamini suala hili litapatiwa ufumbuzi hivi karibuni. Niseme pia kwamba, kama alivyosema jana Waziri wa Nishati na Madini, wakati anahitimisha hoja yake, jitihada za kuvutia wawekezaji katika sekta hii ya kutafuta na hatimaye kuchimbua mafuta, zitaendelezwa kwa nguvu zote na sheria ya sasa (*The Petroleum Exploration and Production Act of 1980*), itafanyiwa marekebisho kwa lengo hilo hilo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Fatma Said Ali, avute subira kwa hayo aliyojasema. Kama nilivyosema, nakubaliana naye katika sehemu hii ya kwanza, lakini haya ya suala la gesi na mafuta, naamini litapatiwa ufumbuzi tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Philip Marmo, sasa ye ye ni mmoja wa mabingwa katika masuala ya usuluhishi. Alisema ingelitungwa sheria basi ya *Arbitration* kwa kuwa usuluhishi wa aina hii sasa hivi nchi imevamiwa na wasuluhishi kutoka Kenya, Uganda na Afrika Kusini. Kwanza, nikubaliane naye kwa suala moja, Sheria ya Usuluhishi (*Arbitration*), ambayo ni sura ya 15 ya Sheria za Nchi yetu, inahitaji ifanyiwe marekebisho makubwa. Ni miiongoni mwa sheria ambazo Serikali inakusudia kuleta mapendekezo katika Bunge hili ili eneo hili liendane na wakati. Kwa hayo, aliyotushauri sisi tungependa sana Watanzania ambao wanapata sifa kama ye ye, wajitangaze kwanza, maana mimi sikuwa nafahamu kwamba, Mheshimiwa Philip Marmo amekwenda kiasi hicho. Sasa ni vizuri tukajitangaza, tukikaa kimya na kuwa wanyonge, ndio tunapata matatizo haya. Tunapata wataalamu, tuna tatizo limeibuka la usuluhishi, tunaanza kukuna vichwa tumtafute nani, kumbe hazina tunayo hapa hapa ndani ya nchi yetu. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Wapo lakini hawavumi.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Ndio wapo lakini hawavumi, lakini sasa ninglipenda wavume zaidi.

Aligusia pia utatuizi wa migogoro ya ardhi. Mimi niseme tu katika eneo hili, naelewa tuna matatizo lakini yameanza kushughulikiwa sana. Kwa upande wa

Mahakama Kuu kama mnavyofahamu, inashughulikia ile Mahakama ya Ardhi, lakini ni sehemu ya Mahakama Kuu. Inashughulikia Mashauri ya Ardhi yanayofunguliwa katika ngazi hiyo, pamoja na rufaa zinazotoka katika Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya. Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, inashughulikia mashauri kupitia vyombo ambavyo vipo ndani ya sheria, yanayofunguliwa katika Mabaraza ya Ardhi ya Kata na Vijiji. Sasa rufaa zinazotoka katika ngazi hii, Mabaraza ya Vijiji ya Ardhi na Kata yanakwenda kwenye Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya.

Vile vile anaunga mkono kwa nguvu zake zote, uanzishwaji wa *Law School*. Lakini akasema wafundishwe masomo ambayo yataendana na hali ya sasa (*modernization*), leo haiwezekani mkaganda katika yale ya miaka ya 1940 na 1970. Kwa hilo nakubaliana naye. Lakini kwa kuwa *Law School* itajihusisha zaidi na mafunzo ya vitendo, Serikali ingependa kutoa wito kwa Vyuo Vikuu vyote hapa nchini, vinavyotoa mafunzo ya Shahada ya Sheria, kuandaa *syllabus*, ambayo inalingana na mahitaji ya wakati huu, hasa kwa upande wa teknolojia na utandawazi na masuala mengine ambayo tunahitaji vijana wetu wakayafahamu. Hilo ni vizuri tukalifahamu, lakini ni hoja nzuri tunakuja na hiyo *Law School*. Nilitamani sana katika uongozi wangu, kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali, chombo hiki niweze nikakiona lakini naona haitawezekana katika mwaka huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi sasa katika hoja ya Mheshimiwa Mohamed Juma, alisema kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, lakini ninavyomfahamu, ye ye hiyo haikuwa hotuba yake, imeandaliwa na huyo ambaye hayumo Bungeni humu. Lakini niseme moja, ni vizuri ukweli tusiupinde hasa Tume ya Haki za Binadamu anasema haina nguvu ya kupambana na hiyo. Sasa haina nguvu kwa vipi? Hiki ni chombo, kazi yake kubwa ni kushauri, kusuluhiha na kupatanisha. Sasa unataka uipatie meno ya kufanya nini? Ije kutembea nyumbani kwako, kufanya nini? Ina sheria yake na misingi yake iko ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, anadai haki ya kuishi inavunjwa na Serikali, angalia operesheni Shinyanga, Kilombero, Zanzibar, Bulyankulu, Mwembechai na Pemba. Yote haya tunajua ni porojo tu. Serikali inathamini sana haki za kuishi popote kwa Watanzania ili mradi wanaishi kwa amani na utulivu na wanazingatia sheria. Ndiyo maana matukio hayo yalipotokea, Serikali iliunda Tume na kufuatia kujua kulikoni na mapendekezo ya matukio hayo watu wanayafahamu. Sio haya ambayo Mheshimiwa Wilbrod Slaa, unataka kulifanya Bunge hili liamini.

Haki za ajira zinavunjwa, zinavunjwa wapi? Wafanyakazi wanadhuluiwa mafao kama *TTCL*, *NBC*, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Napenda tu niseme hivi, Katiba inahakikisha haki ya kufanya kazi na sio ajira na hasa hata kwenye eneo la ajira yenye lazima pawepo na utaratibu. Kwanza pawepo na nafasi, huwezi tu ukaja hapa kwa Naibu Spika, nataka kazi, nipe ajira. Hapana, lazima kuwepo na nafasi kwa kazi unayoiomba. Ufuate utaratibu na sio hapo tu lakini ufikie vile vigezo ambavyo walitangaza kwa nafasi hiyo. Serikali inathamini na kuhakikisha haki za wafanyakazi na ndiyo maana tunasimamia kwa karibu sana migogoro ya *TTCL* na *NBC*, haikuhusu mafao ila inahusu suala la upunguzaji wa kazi wafanyakazi.

Suala la wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amelitolea maelezo ya kina hapa na nisingelipenda niyarudie, lakini ni upotoshaji tu wa wenzetu. Niseme moja la msingi. Amedai kwamba, Katiba ya sasa haikuhusisha Watanzania, hili dai si kweli Mheshimiwa Naibu Spika. Mkataba wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, uliweka utaratibu wa jinsi ya kuyashughulikia masuala hayo na Tume hiyo ndiyo iliyoweka msingi na mpaka Katiba ya mwaka 1977, ambayo ndiyo tunayo leo, ikafikiwa na marekebisho mengi yamefanywa kwa kuzingatia kuona sasa mjadala huu tuupanue na ndiyo maana Serikali inakuwa inapata maoni ya Wananchi kabla ya kuleta marekebisho hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningeliomba Waheshimiwa Wabunge, hasa hii Kambi ya Upinzani, nawaomba kabisa kauli zao ziendane na vitendo. Tumeshuhudia majuzi wakati wa Marekebisho ya 14 ya Katiba, wakati wa maamuzi ya msingi ambayo walipaswa wasikike na Watanzania waseme kwa nini hawaungi mkono, wote walitoka nje ya Ukumbi huu. Huo sio uungwana, muungwana anabaki anafia pale pale na hoja yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa sababu muda sasa unanitupa mkono. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri asubuhi hapa, huu ni Mkutano wa mwisho kwa Bunge hili katika Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tatu. Kwa wadhifa nilionao, atakapoapishwa Rais mpya na mimi naamini atakuwa ni Mheshimiwa Jakaya Kikwete, siku ya kuapishwa Rais na huyu ambaye ameshikilia wadhifa huu, naye ukomo wake ndio siku hiyo hiyo na muda huo huo unakuwa sio Mwanasheria Mkuu mpaka atakapoteuliwa Mwanasheria Mkuu mwengine.

Kwa maana hiyo, ningelipenda nichukue nafasi hii, kumshukuru kutoka chini ya sakafu ya moyo wangu, Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, kwa imani aliyoonesha kwangu, kwa kipindi cha takriban miaka 10, kwa kunikabidhi wadhifa huu. Nawashukuru na Watanzania wote kwa kunithamini. (*Makofi*)

Namshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Waziri, kwa msaada wote walionipatia katika kipindi hiki. Natoa shukrani zangu za dhati kwa watumishi wa Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, hususan Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tumefanya kazi pamoja, kwa ushirikiano na kwa mafanikio makubwa. Nimejifunza mengi sana kutoka kwao na Mheshimiwa Naibu Spika, najivunia sana kuwa na timu hiyo ya wataalam.

Nakushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru kupitia kwako, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wetu wawili na pia ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi mlivyonisaidia humu Bungeni tangu nilipoteuliwa. Nitakuwa sina fadhila nisipotambua msaada wa karibu kutoka kwa Uongozi wa Mahakama, ninawashukuru sana na wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda niwashukuru na kuwapongeza wakazi wa Manispaa ya Dodoma, kwa ukarimu wao na wametupokea tangu tufike hapa mwaka 1995, tumeshirikiana nao kwa hali na mali usiku na mchana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wabunge ambao wameamua kurudi kwa Wananchi na kuomba tena ridhaa yao, ninawatakia kila la kheri na mafanikio. Ninawaombea nia na matamanio yao yafanikiwe kama ninavyoamini na wao wananiombea mimi na kunitakia mafanikio huko niendako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, narudia kama nilivyoanza kusema, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nakushukuru kwa fursa hii uliyonipa ili niweze kujibu na kutoa ufanuzi kwa hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge leo hii wakati wakichangia mapendekezo ya bajeti ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nianze kwa kuwashukuru na kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza humu Bungeni na kwa maandishi. Waheshimiwa Wabunge waliozungumza humu Bungeni ni wafutao:-

Mheshimiwa Paschal Degera - kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala; Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib, Mheshimiwa Khalidi Suru, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Andrew Chenge. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Irenius Ngwatura, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Geroge Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Lucas Selelili, Mheshimiwa Herbert Mntangi na Mheshimiwa Danhi Makanga. (*Makofi*)

Aidha, napenda niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliota michango kuhusu Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba wakati wakichangia hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambao ni Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya. Nawashukuru kwamba wachangiaji wote wameunga mkono hoja ya bajeti ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze katika hoja mbalimbali zilizojitokeza kwa sababu hoja zimezungumziwa na wachangiaji zaidi ya mmoja, naomba

nizungumzie hoja hizo katika ujumla wake badala ya kumjibu Mbunge mmoja mmoja lakini wakati ukiruhusu nitaweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumaini Waheshimiwa Wabunge wanapenda kuona kuwa kasi ya utoaji wa haki inaongezeka na hatimaye kufikia azma ya kuwa na haki kwa wakati na kwa wote. Mengi yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ni kati ya mambo ya msingi ambayo yatashugulikiwa chini ya programu ya kuboresha Sekta ya Sheria, mkakati wa kati wa mwaka 2005/2006, 2007/2008 mkakati ambao umeelezwa katika aya ya 35 mpaka 36 ya hotuba yangu.

Mtakumbuka mkakati umelenga kuboresha maeneo makubwa katika uboreshaji wa usimamizi wa haki. Naamini katika kipindi cha miaka mitatu ijayo Sekta ya Sheria itafanya mabadiliko makubwa yatakayoongeza ufanisi na kasi ya usimamizi wa haki nchini na hasa Sheria na Kanuni mbalimbali, haki kwa wasiojiweza, haki za binadamu na za kiutawala, elimu na taaluma kwa Wanasheria, huduma katika Asasi za sheria na Uongozi, udhibiti na utaratibu baina ya Asasi zinazosimamia haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nijaribu kujielekeza katika maeneo mbalimbali ambayo yamezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mulyambatte alizungumzia suala la kuboresha maslahi ya Majaji, Mahakimu na watumishi. Wizara yangu inalijua tatizo hili na imekuwa ikilizingatia na tunaendelea kufanya kazi. Suala la pili ambalo amezunguzia ni mauaji ya watu huko Meatu mwaka 1997. Suala hili ni la kisheria na kwa sasa hivi limekuwa liko Mahakamani.

Kwa hiyo, siwezi nikazungumzia kwa wakati huu. Mheshimiwa Lekule Laizer amezungumzia kuhusu ujenzi wa Mahakama za Mwanzo Longido na Indumumeti chini ya mpango wa *Quick Start*. Mahakama hii ya Mwanzo ya Indumumeti ni kati ya Mahakama zilizoteuliwa kujengwa chini ya mradi ya *Quick start* Wilaya ya Ngorongoro. Lakini kama nilivyozungumzia katika hotuba yangu, mradi huu sasa ulikwisha Desemba mwaka jana 2004. Kwa hiyo, utaunganishwa chini ya mkakati wa mpango wa kuboresha Sekta ya Sheria.

Pia, alitoa hoja juu ya vijana waliohusika kuhukumiwa kifungu cha miaka 40 kwa makosa ya wizi na mifugo. Suala hili nilizungumzia mwaka jana 2004 lakini kwa sasa hivi ningemshauri Mheshimiwa Lekule Laizer awasiliane na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Aggrey Mwanri amezungumzia upungufu wa Mahakimu. Suala hili ni tatizo lakini tunaendelea kulishughulikia kwa kuajiri Mahakimu wapya na kuwafundisha Mahakimu wengine.

Mheshimiwa Aridi Uledi pia amezungumzia tatizo la Mahakama za Mwanzo ajira kwa Mahakamu, nasema hili tunalifanya kazi na punde tutakapopata Mahakimu wa kutosha, basi tutaweza kuwapeleka katika Jimbo lake la Nanyumbu. (*Makofii*)

Pia, amezungumzia suala la hali ya majengo ya Mahakama ya Mwanzo ya Makanga, Nanyumbu, Nakipi na Mchinga. Serikali imeanzisha utaratibu wa kurabati majengo ya kutosha kwa Mahakama zote nchini. Kwa hiyo, naomba asubiri. Nyumba za Watumishi hali kadhalika hali ikiimarika kifedha basi nyumba hizo zitajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Herbert Mntangi amezungumzia kuundwa kwa Mahakama Maalum na *Attorney General* ameshazungumzia suala hilo, amezungumzia pia kuboresha Mabaraza ya Kata. Nadhani *Attorney General* pia ameshazungumzia suala hilo. Mheshimiwa Luoga alizungumzia Mahakama ya Mwanzo ya Liuli kufungwa, naomba kwa Mahakama hiyo ikarabatiwe na wananchi wapate huduma. Ni suala ambalo pia tutalishughulikia kwa wakati muafaka fedha ikipatikana. (*Makofit*)

Kuhusu kutumia Ofisi za CCM kuwa kama ni Mahakama, utaratibu huu tunao hatuwezi kutumia Ofisi za Chama chochote kile. Mheshimiwa Damas Nakei ameomba tuongeze idadi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Ninachoweza kusema ni kwamba sasa hivi Mahakimu wapya 40 wa Mahakama za Mwanzo wamepangia Vituo na ni matumaini yangu kwamba Wilaya ya Babati itafikiriwa.

Mheshimiwa Leonard Derefa amezungumzia kuhusu Mahakama Kuu ya Shinyanga. Sasa hivi hatuna uwezo wa kujenga Mahakama Kuu, tumeanza na Bukoba pamoa na Iringa. Kwa hiyo, baada ya hapo tutafikiria kujenga Mahakama Kuu katika Mkoa wa Shinyanga. Amezunguzia pia malalamiko kwamba kuna madai Shilingi takribani milioni saba, fedha hizi zimekwishatumwa Shinyanga kwa *warrant* Na.00176496 ya tarehe 27 Mei, 2005.

Mheshimiwa Talala Bana Mbise amezungumzia kesi kupelekwa katika Ofisi za CCM za Vijiji na zinasikilizwa na kutolewa maamuzi. Namwomba Mheshimiwa Mbise atupatie basi kwa maandishi uthibitisho wa majina ya Vijiji husika ili tuweze kulishughulikia suala hilo.

Mheshimiwa Esha Stima anaomba Waziri afanye utaratibu maalum wa kuwasaidia walemvu. Utaratibu huu upo. Mheshimiwa Ali Said Salim kuhusu Wagombea binafsi *Attorney General* ameshalizungumzia hilo, Sheria za uchaguzi *Attorney General* pia ameshalizungumzia hilo.

Mheshimiwa Job Ndugai ufunguzi wa Mahakama ya Wilaya ya Kongwa hii imefunguliwa Agosti mwaka jana, 2005, tunamshukuru kwa pongezi hizo. Ujenzi wa nyumba ya Hakimu, hili tutalishughulikia pindi tutakapopata pesa za kutosha. Mahakama ya Kibaigwa kwamba ijengwe Mahakama ya Mwanzo hili suala pia tutalizungumzia kwa wakati muafaka wakati tukiwa tuna pesa. Amezungumzia pia ukaratibati wa Mahakama za Mwanzo Msalala, Mlali, Pandambili, Mkoka na Sisa. Katika mpango wa kujenga hizi Mahakama za Mwanzo kwa sasa hivi ambazo ni 51 katika awamu ya kwanza Mahakama hizi hazipo lakini tutafikiria hapo baadaye.

Ukopeshaji wa pikipiki kwa Mahakimu, utaratibu umekwishaanzishwa na Mikataba inaendelea kutungwa baina ya Mahakama pamoja wenyewe pikipiki hizo. Posho za washauri kama hawa Wazee wa Baraza bado hawajalipwa, basi ningeshauri kwamba suala hili liwasilishwe kwenye Mahakama ya Wilaya ili taratibu za malipo ziweze kufanyika. Msongamano wa mahabusu Kongwa tunategemea kwamba msongamano ulitarajiwa kupungua Hakimu wa Wilaya atakapoanza kazi.

Mheshimiwa George Lubeleje amezungumzia masuala mbalimbali, mengi kwa kweli ni kusisitiza yale ambayo Kamati yenyewe ilikuwa inawasilisha na kuunga mkono hoja yangu. Kwa hiyo, tunamshukuru kwa hayo yote ambayo ameyazungumza. Mheshimiwa Makwetta amezungumzia suala la utawala bora na matatizo ya msongamano. Suala la kuwa kuwe na *crash program* ili tuweze kupata Mahakimu tunasema hayo yote ambayo ameyazungumzia tumeyazingatia na tutayafanyia kazi. Pia, amezungumzia Sheria ya kunyonga, nadhani hili Mheshimiwa *Attorney General* ameshalizungumzia.

Mheshimiwa Ngwatura amezungumzia mishahara ya Mahakimu kuwa midogo, nasema Serikali inafanyia kazi, idadi ya Mahakimu na Mahakama za Mwanzo kuwa ni ndogo nalo hili tunalifanyia kazi. Amependekeza kuiondoa Taasisi ya Kuzuia Rushwa kutoka Ofisi ya Rais na kuwa ni Tume huru, tumelipokea hilo wazo na tutalifanyia kazi kwa wakati unaofaa.(*Makofti*)

Mheshimiwa Selelii amezungumzia malalamiko ya wananchi kwenye Jimbo la Nzega kuhusu suala la mirathi, tumefanya uchunguzi na fedha hizo, zimekwishawasilishwa mahali husika huko huko Nzega. Amezungumzia pia kuhusu Mahakama za Mwanzo kufanyiwa ukarabati, hili suala pia tutalitizama kuuwiana na bajeti ambayo tunayo. Mheshimiwa Mfaki, kazungumzia suala la tafsiri ya picha iliyopo juu ya jalada la kitabu cha hotuba yangu. Ile ni nembo yenyewe taswira ya binadamu ambaye ameshika singe na mizani na amesimama kwenye mwamba. Ameomba kujua kuhusu jengo la Mahakama ya Mvumi Makuru kama lipo katika mpango wa kujengwa au kukarabatiwa. Zimetengwa Shilingi bilioni moja kwa ajili ya ukarabati wa Mahakama za Mwanzo, suala hilo tutalizingatia.

Pia, kazungumzia suala la usafiri. Tumesema utaratibu upo na sasa hivi Idara ya Mahakama imeingia katika Mkataba na wahusika ili waweze kuwapatia usafiri Mahakimu wa Mahakama za mwanzo. Mheshimiwa Fatuma Said Ali, amezungumzia suala la mafuta hilo Mheshimiwa *Attorney General* ameshalizungumzia, Mheshimiwa Marmo, amezungumzia juu ya Sheria ya *arbitration*. *Attorney General* ameshalizungumzia. Amezungumzia kuhusu uundaji wa *syllabus* ya *law School*, *Attorney General* ameshalizungumzia,

Mheshimiwa Dr. Slaa, amezungumzia mambo mengi kuhusu Tume kutokuwa na nguvu hizo, *operation* za Shinyanga, Kilombero, zote hizo *Attorney General* ameshazizungumzia na masuala ya ajira *Attorney General* ameshayazungumzia.

Mheshimiwa Pawa amezungumzia kuhusu, kiasi gani cha wa wazee wa Mahakama wanapata? Kwa maana ya posho ni Shilingi 1,500. Je, madai ya nyuma yanalipwa? Madai yote ya nyuma yanalipwa mara yanapowasasilishwa.

Kuunganisha Tume haki za binadamu, Tume ya kuzuia rushwa swali hili liliwahi kufikiriwa lakini kwa wakati huu tumeona kwamba ni vizuri ikawa zinafanya kazi tofauti. Pia, amezungumzia kesi ya Babu Seya, hili suala liko Mahakama ya Rufaa na familia ya Babu Seya imekwishakata rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kuna hoja za Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ndesamburo, amezungumzia kuhusu mpaka wa Moshi Vijijini na Moshi Mijini, kuwekwa sawa, suala hili litaangaliwa na mamlaka inayohusika.

Mheshimiwa Suru, amezungumzia mambo kadha katika misingi ya kuimarisha utawala bora. Nasema haya yote tumeyapokea, tunashukuru kwa mawazo yake na tutayafanya kazi kuhusu uchache wa Mahakimu kama tulivyozungumza, malipo ya posho ya Wazee wa Baraza tutaendelea kuwalipa kwa mujibu wa taratibu zetu. Amezungumzia pia ukarabati wa Mahakama zilizopo na kujenga Mahakama katika Wilaya ambazo hazina majengo ya Mahakama na sasa hivi Mahakama inaanda utaratibu wa kuweza kujenga Mahakama hizo kulingana na bajeti kama itaruhusu.

Kuhusu hukumu kwamba ziandikwe kwa Kiswahili ili wahusika wasome na kuzielewa, hukumu katika Mahakama za Mwanzo zinaandikwa kwa Kiswahili ni zile tu za Wilaya, Mkoa, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa ndizo zinazoandikwa kwa Kiingereza.

Hata hivyo unaweza ukapata tafsiri yake. Haki za Bodi za Mahakama zianishwe ili zifanye kazi, haki za Bodi za Mahakama zimekwishaainishwa. Mahakama za Mwanzo Kondo Mji mpya, Busi, Kolo na Beleko ni chakavu zikarabatiwe. Katika mpango huu wa majengo 51 na ukarabati wa Mahakama za Mwanzo suala hilo litafikiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, haki ya kuishi na haki ya kufanya kazi hili suala *Attorney General* amekwishalizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi hizo ndiyo hoja mbalimbali ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge na nimejaribu kujibu hizo hoja kwa ujumla na moja baada ya nyingine, inawezekana kwamba sikuzijibu kikamilifu, lakini kama ilivyo desturi yetu tumezipokea hoja hizo tutazifanya kazi na kuwajibu kwa maandishi Waheshimiwa Wabunge wote waliotha hoja hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunisikiliza na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Nawatakieni kila kheri katika zoezi ambalo linakuja la Uchaguzi wa Oktoba. Tuombe wengi wetu turejee katika Bunge hili. Nami nawaombeni ndugu zangu mniombee niweze kurudi katika Bunge hili. Nimekwishapata baraka za wazee wa Tanga, nimeshapata baraka za vijana, nimeshapata

baraka za akina mama, nimeshapata baraka za mafundi wangu, kwa hiyo, ndugu zangu naomba mniombee kila la kheri tuweze kukutana katika Ukumbi huu wakati ukifika.
(*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 40 - MAHAKAMA

Kifungu 1001 - <i>Administration And General</i> Tshs. 5,734,644,300/=
Kifungu 2001 - <i>High Court</i> Tshs. 1,308,323,400/=
Kifungu 2002 - <i>Court Of Appeal Dar es salaam</i> Tshs.1,640,272,300/=
Kifungu 2003 - <i>Arusha Zone</i> Tshs. 993,205,500/=
Kifungu 2004 - <i>Dar es salaam Zone</i> Tshs.1,759,322,300/=
Kifungu 2005 - <i>Dodoma Zone</i> Tshs.803,138,400/=
Kifungu 2006 - <i>Mbeya Zone</i> Tshs.1,468,512,400/=
Kifungu 2007 - <i>Mtwara Zone</i> Tshs. 749,880,900/=
Kifungu 2008 - <i>Mwanza Zone</i> Tshs.1,189,482,300/=
Kifungu 2009 - <i>Tabora Zone</i> Tshs. 1,424,252,700/=
Kifungu 2010 - <i>Tanga Zone</i> Tshs. 619,331,600/=
Kifungu 2011 - <i>Primary Courts</i> Tshs. 4,425,090,700/Kifungu 2012 - <i>District Courts</i> Tshs. 3,625,496,000/=
Kifungu 2013 - <i>Kagera Zone</i> Tshs 681,160,200/= Kifungu 2014 - <i>Ruvuma Zone</i> Tshs 732,607,800/= Kifungu 2015 - <i>Moshi Zone</i> Tshs. 723,197,700/=

(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

**FUNGU 41 - WIZARA YA SHERIA NA
MAMBO YA KATIBA**

Kifungu 1001 - *Administration And General* Tshs. 1,903,532,000/=

MHE. DANHI B. MAKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nina maswali machache tu, niko katika Mshahara wa Mheshimiwa Waziri hapa. Sio *Administration! 2001 sub-vote Basic Salaries* hapo. Kama hamjui sheria angalieni vizuri kwenye Katiba zenu.

MWENYEKITI: Endelea Mheshimiwa Danhi B. Makanga, ni hapo hapo.

MHE. DANHI B. MAKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo tu ya ku-clarify kidogo ambayo niliyachangia kwa njia ya maandishi. Nilikuwa nimeuliza Sheria ambazo tumezipitisha hapa, sheria ya ruzuku kwa Vyama vy'a Siasa na sheria ya Viti Maalum ambayo tulipitisha hapa. Nilisema kama imepitwa na wakati lakini sikusikia Waziri au Mwanasheria kama anaijibu kwamba wanaifanyia kazi gani. Ni kama zimepitwa na wakati kwa sababu tunajua sheria ya uchaguzi mwaka 2000, kwamba Wabunge wa Majimbo wanane wanatoa Mbunge wa Viti Maalum mmoja na hivyo hivyo kwa Madiwani. Hao Wabunge sasa wanatokea kwamba wamefukuzwa na Chama fulani, huyu wa Viti Maalum anafanya nini humu ndani wakati hawa wengine wameshaondoka?

Lakini vile vile hata ruzuku, hawa Wabunge ndiyo wanakipa ruzuku Chama hiki, lakini baada ya kuondoka, Chama bado kinaendelea kula ruzuku. Sasa na huyu Mbunge ambaye katika *by-elections* zinazotokea kuanzia Udiwani hata Ubunge, Chama kinachoongeza Viti hakipewi nafasi ya kuongeza ruzuku au kuongeza Viti maalum, maana yake ni nini? Hii inawapa viburi Viongozi wa Vyama wasio na maadili ya Uongozi, kwa sababu kumfukuza Mbunge au Diwani hakuathiri mapato yao. Ndilo hilo ambalo nilikuwa naliuliza. Tunafanya nini? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, nilikuwa nauliza, Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu kuhusu Mahakama Kuu Shinyanga, sisi hatutafuti hela za kujenga Mahakama Kuu, tayari miaka mingi tulishapata majengo ya Jaji ya kuishi na majengo ya *High Court* pamoja na Wakili wa Serikali, yako majengo ya kutosha. Tulishaandika barua na Jaji Mkuu alishanijibu mimi *personally* kwamba hivyo vitu anakuja kuvifungua lakini leo karibu miaka mitatu, minne. Kwa hiyo, nafikiri abadili, kama ni kuja kukarabati majengo tuliyonayo, hiyo tutakubaliana, lakini siyo kuweka Bajeti ya kujenga kabisa. Hayo ndiyo ambayo nilitaka nipate ufanuzi wake.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubali kabisa kwamba Mheshimiwa Danhi B. Makanga alileta mchango wake kwa njia ya maandishi, lakini katika kipindi cha majeruhi, ndiyo maana nadhani hatukupata fursa ya kuitolea maelezo. Lakini niseme kitu kimoja tu mbele ya Kamati yako Tukufu kwamba hizi sheria *they are not Cast Iron* kwamba zimeandikwa katika mawe. Zimetungwa na Bunge hili na pale ukweli unapothibitika, Serikali haiwezi ikasita kurudi na kuliomba Bunge liweze kufanya marekebisho.

Tukianzia hii ya viti maalum, tumekuwa na mawasiliano tangu mwaka 1995 na Tume ya Uchaguzi. Lakini Tume ya Uchaguzi ilichukua tafsiri ambayo tulisema sawa kwamba wanasema una idadi hiyo ya Viti maalum hata kama hatimaye Mheshimiwa Mbunge wa Chama fulani anaitwa mbele ya haki au anafukuzwa uanachama, ni ile ambayo ilitangazwa na Tume mara tu baada ya matokeo ya Uchaguzi Mkuu na ndiyo wamekuwa na msimamo huo. Ni kweli anachoeleza Mheshimiwa Danhi B. Makanga, unaona ina vi-unfairness, lakini ili tujibu hoja hiyo, kwa vile uamuzi wa Tume ulijikita katika jinsi Katiba ilivyoandikwa, basi ni vizuri basi kama hoja hiyo itadhibiti basi tujielekeze katika kuiangalia vizuri sheria hiyo kwa upande wa Viti Maalum kwa sababu msingi wake uko kwenye Katiba.

Kwa Madiwani kama anavyosema kwa misingi ile ile ni vizuri tukaiangalia. Ya ruzuku, *formula* ile si ya Tume ya Uchaguzi, ni ya Msajili wa Vyama vya Siasa na inategemea na idadi, lakini (*logic*) mantiki unaiona ni ile ile. Kama huna Mbunge, ulianza kupewa ulikuwa na Wabunge watatu, wote siyo Wabunge wa Chama chako, hiyo ruzuku unaitaka ya nini? Ndiyo hoja tu anayosema Mheshimiwa Danhi B. Makanga. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani ni vizuri haya masuala tuyaangalie na kipindi muafaka Serikali iweze kuyafanya marekebisho. (*Makofi*)

Hili la mwisho nitamwachia Mheshimiwa Waziri mwenyewe aweze kulitolea maelezo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, Kuna watu wana ugonjwa wa moyo, mtatupasua! (*Kicheko*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba suala la Mahakama Mkoa wa Shinyanga limekuwepo kwa muda na tangu alipokuwepo Mheshimiwa Babu kama Mkuu wa Mkoo ule. Mimi binafsi pamoja na Jaji Mkuu tulitembeli Shinyanga, lakini baada ya kutathmini majengo yale, tukaona kwamba hayafai kwa hadhi ya Mahakama Kuu. Kwa hiyo, kwa sasa hivi kiwanja kimekwishapatikana na utaratibu wa jengo jipya unafanyiwa kazi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Makanga avute subira kuhusu suala hili. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* Tshs. 17,201,700/=
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* Tshs. 17,201,700/= Kifungu 1003 - *Policy and Information Service*... Tshs. 556,998,600/= Kifungu 2001 - *Administrator General* Tshs. 681,302,400/= Kifungu 2002 - *Public Prosecution*..... Tshs. 2,228,007,000/= Kifungu 2003 - *Legislative Drafting*..... Tshs. 546,503,900/=
Kifungu 3001 - *Civil and International Affairs*.... Tshs. 578,179,400/=
Kifungu 4001 - *Constitutional Affairs* Tshs. 422,440,900/=

(*Vifungu Viliviyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote*)

FUNGU 55 - TUME YA HAKI ZA BINADAMU

Kifungu 1001 - *Administration And General* ... Tshs. 2,709,058,900/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote*)

FUNGU 59 – TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Kifungu 1001 - *Administration And General* ... Tshs. 761,508,200/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

FUNGU 64 – MAHAKAMA YA BIASHARA

Kifungu 1001 - *Administration And General* Tshs. 782,716,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

FUNGU 90 – MAHAKAMA YA ARDHI

Kifungu 1001 - *Administration And General* Tshs. 591,814,700/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

MAKADIRIO YA MAENDELEO

FUNGU 40 – MAHAKAMA

Kifungu 1001 - *Administration And General*... ... Tshs. 160,000,000/=

Kifungu 2001- *High Court*... Tshs. 100,000,000/=

Kifungu 2002 - *Court Of Appeal* Dar es salaam....Tshs. 590,000,000/=

Kifungu 2011 - *Primary Courts*... Tshs.1,000,000,000/=

Kifungu 2012 - *District Courts*... Tshs. 150,000,000/=

Kifungu 20013 - *Kagera Zone*... Tshs.1,000,000,000/=

(Vifungu Vilivytajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko yoyote)

FUNGU 41 – WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA

Kifungu 1001 -
Administration And General... ... Tshs. 6,307,562,100/=
Kifungu 4001 - *Constitutional Affairs*... Tshs. 200,000,000/=

(Vifungu Vilivytajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko yoyote)

FUNGU 64 – MAHAKAMA YA BIASHARA

Kifungu 1001 - *Administration And General*... ... Tshs. 510,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

T A A R I F A

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Sheria na Mambo ya
Katiba ya Mwaka 2005/2006 yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 12.12 jioni Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi
Tarehe 14 Julai, 2005 saa tatu asubuhi)*